# MAANDALIO KWA MASOMO YA MWAKA WAKANISA

Josef Imberg

# MAANDALIO KWA MASOMO YA MWAKA WA KANISA

**Yametungwa**
**na**

**Josef Imberg**

© Rune Imberg 2021
Only to be reprinted / copied after permission through
*Evangelisk Litteraturmission - Scriptura, Sweden*

Chapa ya kwanza:
Matongo Bible School
SONDU, Kenya, 1968.

Chapa ya pili:
Alvesta, Sweden, 1991.

Chapa ya tatu:
Alvesta, Sweden, 2003.

© Copyright:
Judith Imberg
S-342 31 Alvesta
Sweden.

Printed in Sweden by:
ToreSäll InfoMedia AB
Växjö 2003

# YALIYOMO

## MILANGO INAYOTANGULIA


| | | |
|---|---|---|
| I | Kuhubiri ni nini? | 5 |
| II | Kujiandaa kuhubiri | 6 |
| III | Mashauri mema machache | 9 |
| IV | Masomo yenye sehemu | 10 |
| V | Matumizi ya kitabu hiki | 11 |


## MASOMO YA MWAKA MMOJA WA KANISA


| Somo | Ukurasa | Somo | Ukurasa | Somo | Ukurasa |
|---|---|---|---|---|---|
| Mt 2:1-12 | 30 | Mt 25:31-46 | 120 | Lk 21:25-36 | 14 |
| Mt 4:1-11 | 46 | Mk 7:31-37 | 96 | Lk 23:33-48 | 56 |
| Mt 5:1-12 | 126 | Mk 16:1-7 | 58 | Lk 24:13-35 | 59 |
| Mt 5:20-26 | 84 | Lk 2:1-20 | 20 | Yn 1:14-18 | 28 |
| Mt 6:24-34 | 102 | Lk 2:21 | 26 | Yn 1:19-28 | 18 |
| Mt 7:15-21 | 88 | Lk 2:33-40 | 24 | Yn 2:1-11 | 34 |
| Mt 8:1-13 | 36 | Lk 2:41-52 | 32 | Yn 3:1-15 | 74 |
| Mt 8:23-27 | 38 | Lk 5:1-11 | 82 | Yn 3:16-21 | 73 |
| Mt 9:1-8 | 108 | Lk 6:36-42 | 81 | Yn 4:46-53 | 110 |
| Mt 9:18-26 | 116 | Lk 7:11-17 | 104 | Yn 6:1-15 | 50 |
| Mt 11:2-10 | 16 | Lk 8:4-15 | 42 | Yn 8:31-36 | 124 |
| Mt 15:21-28 | 48 | Lk 10:23-37 | 98 | Yn 8:46-59 | 52 |
| Mt 17:1-9 | 86 | Lk 11:14-28 | 49 | Yn 10:11-16 | 61 |
| Mt 18:1-10 | 122 | Lk 14:1-11 | 105 | Yn 12:1-16 | 54 |
| Mt 18:21-35 | 112 | Lk 14:15-24 | 78 | Yn 14:23-31a | 72 |
| Mt 20:1-16 | 40 | Lk 15:1-10 | 80 | Yn 15:26-16:4 | 70 |
| Mt 21:1-9 | 12 | Lk 16:1-9 | 90 | Yn 16:4b-15 | 64 |
| Mt 22:1-14 | 109 | Lk 16:19-31 | 76 | Yn 16:16-22 | 62 |
| Mt 22:15-22 | 114 | Lk 17:11-19 | 100 | Yn 16:23b-30 | 66 |
| Mt 22:34-46 | 106 | Lk 18:9-14 | 94 | Yn 20:19-31 | 60 |
| Mt 23:34-39 | 22 | Lk 18:31-43 | 44 | Mdo 1:1-11 | 68 |
| Mt 24:15-28 | 118 | Lk 19:41-47 | 92 | | |

I.

# KUHUBIRI NI NINI?

Kuhubiri ni nini, ikiwa tunalifuata Neno la Mungu? Kuhubiri ni kutangaza habari njema, tena habari kubwa sana, yaani kutoa habari kutoka Bwana Mungu mwenyewe. Kazi ya mhubiri ni kuzitoa habari zile ambazo amepelekwa nazo. Mhubiri ni mjumbe tu. Mjumbe hawezi kutoa habari anazozifanya mwenyewe. Ni lazima mjumbe asikike vema, ili watu wayashike maneno yanayosemwa, tena ayaseme maneno yale yale tu aliyotumwa kuyatangaza.

Kazi ile ya kuhubiri ni kuwa *"sauti ya mtu aliaye"* **(Isa 40:3). Lk 3:4; Yn 1:23.** Manabii walikuwa wajumbe, yaani sauti za Mungu. Walikuwa watangulizi wa Bwana Yesu katika kutoa mapenzi ya Mungu. Yohana Mbatizaji alikuwa mjumbe wa namna hii.

Yesu mwenyewe asema ya kuwa kazi yake ni kuhubiri. **Mk 1:38; Lk 4:18.** Lakini hafanani na wahubiri wengine, kwa maana anaweza kuhubiri habari zake mwenyewe. **Yn 5:46; 6:29; 6:35,40.** Yeye ni Neno. **Yn 1:1.** Baada ya kufufuka kwake na kupaa kwake mbinguni anahubiri, akitumia mitume wake. **Lk 10:16.** Yesu ndiye anayehubiri katika kila mhubiri wa kweli. Anahubiri kwa njia ya kila neno la kweli linaloweza kuamsha imani. **Rum 10:17.**

Yesu aliwatuma wanafunzi wake, ili wahubiri. Hakuna anayeruhusiwa kuhubiri, isipokuwa ametumwa na Kanisa kuifanya kazi ya kuhubiri. Siyo kazi ya kila mtu kuhubiri. **Yak 3:1.** Tena, kuhubiri si kutoa habari za kila namna zinazotujia kichwani ama moyoni. Kuhubiri kwa kweli ndiko kutangaza habari za ufalme wa mbinguni, jinsi Bwana Yesu alivyowaagiza wajumbe wake. **Lk 8:1; 9:2; 9:11; Mt 28:18–20; Mk 16:15–16.**

Basi tuhubiri nini? Ufalme wa Mungu tu. **Mdo 19:8; 28:23; 28:31.** Au, kwa maneno mengine: Wokovu kwa nguvu ya msalaba wake Yesu. **1 Kor 1:18; 2 Kor 5:19.**

Kwa hiyo ni lazima tuyapime mahubiri yetu yote katika nuru ya maneno haya. Je, mahubiri yetu ni ya kweli kufuatana na Neno la Mungu? Kama siyo, je, tunakosa wapi na namna gani?

Mwishoni tuyafikiri sana maneno ya Dr Martin Luther juu ya kazi ya kuhubiri:
*"Hatuwezi kufanya kazi nyingine kuliko kuwa kinywa cha Bwana Yesu Kristo na chombo chake. Kwa vyombo hivi yeye mwenyewe atalihubiri Neno lake. Kwa njia hiyo analitoa Neno lake, litoke wazi, kila mmoja apate kulisikia. Lakini kazi hii, ikiwa mtu anayesikiliza atasikia nguvu ya Neno katika moyo wake, siyo kazi ya mhubiri, bali ni* ***kazi ya imani*** *na* ***kazi ya Roho Mtakatifu****. Ni kazi inayofanywa kufuata mapenzi yake na hekima yake ya juu."*

# II.

# KUJIANDAA KUHUBIRI KUFANYWE KWA NJIA GANI?

Kwanza tukumbuke ya kuwa sisi sote ni watu wenye tofauti nyingi. Ukitazama watu wawili wanaofanya kazi fulani, utaona ya kuwa wanaifanya kwa njia mbalimbali. Kama mhubiri mmoja anajiandaa kwa njia fulani, labda huwezi kuifuata njia ile. Labda nyingine inakufaa zaidi. Kwa hiyo, ni vizuri ujaribu mashauri mema yote yanayotolewa hapa, na baadaye kutambua ni njia gani inayokufaa zaidi wewe.

Lakini kwanza ni vizuri uzijue hatari kuu zinazomkuta kila mhubiri.

*NJIA ZISIZOFAA KATIKA KUHUBIRI*

Kuna njia fulani ambazo zinaonekana mara nyingi katika makanisa, ingawa ni njia mbaya. Twazitaja hapa mwanzoni, ili uweze kujiepusha nazo, kwa maana ikiwa umeingia katika njia hizo mbaya, itakuwa vigumu kuziacha tena. Njia hizi zote zatokana na njia maskini za kujiandaa.

1) Kama umekwisha soma somo la siku ile, hujui vizuri utahubiri nini, au utalieleza jinsi gani somo lako; kwa hiyo unasimulia tena somo lako kutoka mwanzo, na labda safari nyingine tena, na baadaye "hubiri" lako linakoma. Lakini kulisimulia somo lako mara mbili tatu hivi, si kuhubiri!

2) Kama umeeleza kidogo maneno machache ya somo lako, unarukia somo jingine unalolipenda zaidi. Labda hurudi tena kwa somo lako la kwanza! Wakristo wanatambua upesi hila ya namna hii! Lakini, kama unahubiri mara nyingi katika mwaka mmoja juu ya somo unalolipenda, na kuacha masomo mengine, ambayo ni kazi yako kuyahubiri, basi wewe ni wakili mbaya. Tazama **Lk 12:42**: *"...awape watu posho kwa wakati wake."*

3) Kama unawasimulia wasikilizaji hadithi mbalimbali, ambazo hazihusiani sana na somo lenyewe, labda watu watapenda kusikiliza hadithi zinazowavuta, lakini ni kazi yako kuwapendeza kwa njia hii katika nyumba ya Mungu?

- - - - - - -

Ili kuepuka njia hizi tatu na makosa mengine makubwa, ni lazima kujiweka tayari kuhubiri, maana yake: kufanya kazi ya kweli ya kuliandaa hubiri lako, ili ujue hata mwanzoni utasema nini katika kila sehemu, na hubiri lako litakoma wapi na kwa njia gani.

Hubiri linalofaa linahitaji kazi nyingi, kabla hujaanza kuandika lo lote. Linahitaji kazi nyingi unapoandika maandalio yako. Linahitaji kazi nyingi hata wakati ambapo maandalio yameandikwa. *Wasioandaa sana kuhubiri kwao, hawawezi kulihubiri Neno la Mungu.*

*KAZI YA KUANDAA HUBIRI MOJA INAWEZA KUFANYWA KWA NJIA HII*

Tumesema ziko njia mbalimbali, lakini hakuna anayeweza kuacha au kudharau mambo yafuatayo. Ingawa njia zetu hazifanani, lakini mambo yafuatayo yawemo kwa kadiri fulani katika njia ya kila mhubiri anapojiandaa.

1) Angalia katika Kalenda ya Kanisa ni siku gani utakapohubiri na somo lako utakalohubiri ni somo gani. Kuangalia huku kufanywe mapema sana.

2) Lisome somo lenyewe. Lisome pole pole, na kwa kuangalia kila neno. Lisome somo lile mara mbili, hata mara tatu, labda zaidi. Wahubiri wengine wapenda kulisoma hata mara kumi au zaidi. Kwa njia hii somo lenyewe litaingia kichwani na moyoni na kukaa humo. Kusoma huku kufanywe mapema sana katika juma, labda Jumatatu ama Jumanne inayotangulia Jumapili utakapohubiri. – Baadaye unaweza kuliacha kidogo somo lile, siku moja ama mbili, lakini si kuliacha kabisa. Hata ukifanya kazi nyingine, au kusafiri, au kupumzika, unaweza kulifikiri na kuwaza juu yake. Somo lenyewe na Neno la Mungu litaendelea kufanya kazi yake katika moyo wako siku hizi za kati.

3) Siku nyingine (siyo Jumamosi usiku!) uanze kufanya kazi ya bidii juu ya somo hili. Sasa utaanza kulifahamu zaidi. Itakuwa lazima kuchungulia Biblia yako huku na huku. Soma maneno yote yanayofanana na kuhusiana na somo lako (*"references"*). Ukiwa na kitabu cha *"Concordance"* (kinachoonyesha *"references"*) unaweza kupata msaada humo.

Katika kusoma kwa njia hii ni vizuri, au ni lazima, uandike maneno ya ukumbusho (*"notes"*). Si lazima kufuata orodha fulani au *"heading"* fulani. Andika mawazo yako na mambo uliyoyaona Biblianí jinsi yalivyokufikia. – Baada ya kufanya kazi hii na kuumaliza muhtasari wako, unaweza kuiacha kazi hii muda fulani. Mawazo mengine yaweza kukufikia katika wakati wa katikati.

4) Sasa unaweza kuangalia zaidi maandiko yako. Ni lazima uyalinganishe tena na somo lako na Neno la Mungu. Fikiri juu ya kila sehemu na kila jambo kama ni fundisho la kweli la Kikristo, na kama linapatana vizuri na Neno la Mungu. Kama una shaka juu ya jambo fulani, kama ni fundisho la Kikristo la kweli ama siyo, basi fungua kitabu cha Imani (ama Katekisimo, ama kitabu kingine kinachofaa) na kutazama kinasema nini juu ya swali lako. Ikiwa huwezi kupata hakika, liache jambo lile. – Katika kuyachungulia na kurudia maandiko yako utafumbua hata mawazo mengine yanayofaa kulieleza somo lako.

5) Sasa unaweza kuyarudia tena maandiko yako na kuona ni taratibu gani inayoweza kufaa. Kama ni lazima, unaweza kuyatilia nambari mambo uliyoandika. Tena unaweza kuona ni maneno gani yanayoweza kuwa maneno ya juu (*"heading"*, *"theme"*, *"topic"*) ya hubiri lako. Kama

umeipata *"heading"* unaweza kuyapanga zaidi mawazo na maneno katika maandiko yako. – Vingine ni maneno fulani katika somo lenyewe ambayo yaweza kufaa kama *"heading"*. Vingine unaweza kujumlisha habari zote katika maneno machache yaliyo kiini, yaani jambo la ndani kabisa, cha somo zima.

6) Sasa unapojua *"heading"* yako na sehemu zilizo kuu, unaweza kuandika hubiri lako. Hapa kuna njia mbili. Unaweza kuandika hubiri kamilifu, yaani hubiri kama litakavyohubiriwa, kila sentensi na kila neno. Vingine unaweza kuandika sehemu zilizo kuu (*"sections"*) na sehemu nyingine ndani yake (*"sub-sections"*). Ukiona unapolipanga hubiri lako ya kuwa litakuwa refu zaidi, ni lazima kuchagua mambo mengine yaliyo makubwa na yenye maana sana, na kuacha mengine.

Ingawa labda umeandika kama "mifupa" tu katika maandalio yako, ni lazima ujue kabisa unataka kuhubiri nini katika kila sehemu, usijaribiwe kanisani kukiri au kutoa "maneno-maneno tu"

7) Kabla hujaanza kulitoa hubiri lako kanisani itakuwa lazima kufanya kazi fulani nyumbani mara nyingi, kama mara tatu nne hivi, au zaidi:

Kuyasoma na kuyachunguza maandalio yako. – Kuyahubiri kama kichwani ama moyoni mwako, ili uweze kulitoa pasipo kutazama sana karatasi zako za maandalio. – Lakini ingawa huzitazami karatasi zako, yafuate maandalio yako! Ikiwa unaacha orodha iliyoandikwa na kujaribu njia nyingine, utapotea upesi na kuhubiri ovyoovyo.

8) *Kabla hujaanza* katika sehemu yo yote hapa juu (1-7), na *pamoja na kufanya kazi zote hapa juu* (1-7) ni lazima *uombe*. Pasipo kuomba kwa Mungu huwezi kuhubiri vema. Maombi yako yawe maombi ya kuugua **(Rum 8:26-27)** unapoendelea kazini. Twaweza kuomba kwa njia hii kila mahali na kila wakati **(1 The 5:17)**. Tena tuombe kwa maombi ya taratibu, ili Mungu apendezwe kuibariki kazi yetu na Neno lake kufunguliwa mbele yetu. *"Kuomba kweli, ndiyo nusu kazi."* (Martin Luther) Katika kuomba kwako, omba ya kuwa uongozwe kwa kisima cha kweli, upate maneno ya kweli. Omba ya kuwa mawazo na maandalio yote yanayotoka nafsini mwako tu yashindwe au kusahauliwa. Omba ya kuwa Mungu alipatie nafasi Neno lake katika mioyo ya wasikilizaji, na ya kuwa aitimize mwenyewe kazi yake takatifu. **(Flp 1:6)**

# III

# MASHAURI MEMA MACHACHE KWA WAKATI UTAKAPOHUBIRI HUBIRI LAKO KANISANI

1) Ujifunze *kusoma vizuri somo lako* kutoka kitabu cha Biblia. *Kazi hiyo ifanywe nyumbani* katika siku zinazotangulia ibada.

2) Katika kuhubiri, lieleze *somo lile lile lililoagizwa Kalendani*, siyo somo jingine ama mambo mengine mengine.

3) *Ujiandae* mbele; wakati unaposimama kanisani si wakati unaofaa kufikiri utahubiri nini.

4) *Tamka maneno yako kwa upesi unaofaa*, yaani usitumie haraka katika kusema maneno. Hasa katika kanisa kubwa ni lazima kukumbuka, usinene upesi.

5) *Tamka maneno yote* sawasawa, watu wayasikie vema.

6) *Pima sauti yako*, isiwe ya juu, wala ya chini, bali iwe ya hali ya kati inayosikika vema zaidi.

7) Kama umeandaa hubiri lako kwa kuandika maandalio marefu ama mafupi, ni lazima *uwe na utaratibu katika maelezo yako*; vingine wasikilizaji hawawezi kukufuata, wala kuyakumbuka maelezo yako.

8) *Yafuate maandalio yako uliyoyaandika*. Kama unatoka nje, labda utapotea kabisa. Huwezi kuhubiri kwa kufuata mawazo yanayokufikia kichwani pale pale unaposimama.

9) *Usirudie–rudie* mambo ambayo umekwisha kuyasema. Ukifanya hivi, wasikilizaji wataona mara moja ya kwamba mawazo yako yamekwisha kumalizika.

10) Katika yote unayofanya, moyo wako unaweza *kuendelea kuomba*, Mungu aibariki kazi yako.

# IV

# HABARI ZA MASOMO AMBAYO INAONEKANA YA KUWA SEHEMU ZAKE HAZIHUSIANI

Masomo mengi ya Kalenda yana sehemu mbili au tatu, au zaidi. Mara nyingi ni waziwazi jinsi sehemu hizi zinavyohusiana, kwa maana kuna wazo moja kuu ama shabaha moja inayounganisha sehemu zote. Tazama k m **Lk 15:1–10**. Humo kuna sehemu mbili. Ingawa zinahitilafiana, lakini zimeunganishwa na shabaha moja, yaani kuueleza upendo ule unaotafuta kilichopotea. Shabaha ile si waziwazi kwa kadiri ile katika **Lk 15:11–32**, lakini hata kule kuna nia moja iliyo dhahiri.

Lakini kuna masomo yenye sehemu ambazo hazifanani. Ingawa twajaribu sana, lakini hatuoni nia inayounganisha sehemu zote katika hubiri moja. Somo namna hii ni **Lk 18:31–43**. Hapa ni waziwazi ya kuwa kuna sehemu mbili zilizohitilafiana. Kwa nini waliotengeneza masomo ya Kanisa (Kalenda) hawakuligawa somo hili, liwe masomo mawili? Jibu ndilo hili: Tangu zamani walimu wa Kanisa wameona ya kuwa sehemu hizi mbili ni somo moja tu. Wameona ya kuwa kweli kuna shabaha moja katika sehemu hizi mbili. Shabaha ni hii: *"Anayepanda Yerusalemu kuteswa, ndiye anayeweza kutuokoa nasi katika maumivu na mateso yetu."*
Mifano mingine ya masomo ya kabila hilo ndiyo **Mt 6:19–23; Mt 8:1–13; Mk 9:14–32; Lk 6:36–42; Lk 19:41–48.**
Ili kusaidia katika kazi ya kuhubiri masomo namna hii twatoa hapa

*MASHAURI MACHACHE KWA MHUBIRI ATAKAYEHUBIRI JUU YA MASOMO YENYE SEHEMU AMBAZO HAZIHUSIANI KWA MAWAZO YAKE*

1) Kama *inaonekana* ya kuwa sehemu hazihusiani, *usifanye mahubiri mawili ama matatu*, moja juu ya kila sehemu.
2) Jaribu *kulifahamu jambo lile kuu* ama neno lile kuu linaloziunganisha sehemu zile.
3) *Usijaribu kwa hila au mchezo wa maneno* kuunganisha sehemu ambazo hazihusiani kwa mawazo yako.
4) Kama huwezi kuona jinsi sehemu zile zinavyohusiana kweli, ni afadhali kuacha sehemu fulani na kushika nyingine na kuhubiri juu ya sehemu ile tu ambayo umeifahamu. Lakini lisome somo lote linaloonyeshwa katika Kalenda ya Kanisa. Katika kuanzisha hubiri lako unaweza kusema: *"Leo tuangalie hasa habari za ..."* (yaani sehemu ile utakayoihubiri).
5) Kama umeshindwa mwaka mmoja kuhubiri somo kamili namna hii, fanya bidii kulifahamu baadaye, ili uweze mwaka mwingine kulishika somo zima.

# V

# MATUMIZI YA KITABU KIFUATACHO

1) Maandalio yafuatayo *ni mfano tu*, siyo mahubiri yenyewe. Kwa hiyo, maana ya kitabu hiki si ya kuwa mhubiri atanakili yaliyoandikwa na kuyahubiri. Akifanya hivi, ingekuwa vibaya sana.

2) Ni lazima kila mhubiri *afanye kazi ya bidii mwenyewe*, yaani kusoma Neno la Mungu huku na huku katika Biblia ili kulichungulia sana somo lake, tena kuwaza juu ya somo na utume wa Jumapili ama sikukuu ile atakayohubiri. Tena ni lazima aandike maono yake na mawazo yake yaliyomjia katika kazi yake.

3) Kama amekwisha fanya kazi namna hii, anaweza kuilinganisha kazi yake na mfano unaopatikana hapa. Labda ataona ya kuwa amekosa upande fulani. Labda atapata mawazo mapya yanayofaa, akisoma mashauri yetu katika kitabu hiki. – Hivi kitabu hiki kinaweza kuwa msaada kama kitabu kingine, ambapo tunatafuta msaada katika kazi yetu. – Lakini anayeiba kazi kamili kitabuni, badala ya kuifanya kazi yake mwenyewe, huyu anafanya vibaya.

4) Mara kwa mara utaona ya kuwa maandalio yafuatayo ni marefu, pengine marefu sana. Kwa maana, ukiingiza nyama kati ya mifupa iliyowekwa katika maandalio, yaani kueleza zaidi kila jambo kwa maneno yako, yatakuwa mahubiri marefu. Lakini tumeifanya kazi yetu namna hii kwa kusudi. Yaani ukikitumia kitabu hiki kama tulivyosema hapa juu (katika nambari ya 3), utaona labda jambo moja linalokusaidia mwaka huu; mwaka mwingine utaona jambo jingine linaloweza kuingia vizuri katika mpango wako.

5) Katika mifano ifuatayo tumefuata njia mbalimbali za kupanga mahubiri. Njia moja inafaa kwa somo moja, njia nyingine inafaa kwa somo jingine.

Ukitumia kitabu hiki, labda unaweza kujaribu mwenyewe njia mbalimbali, kadiri zinavyokufaa katika kueleza masomo fulani.

Lakini shabaha yetu iliyo kuu iwe kuhubiria watu njia ya wokovu, na kumtukuza Bwana wetu Yesu Kristo, na kuieneza sifa yake kati ya watu.

Itendwe hivi kila mahali katika jina la Bwana!

# MAANDALIO KWA MASOMO YA MWAKA MMOJA WA KANISA

## SIKU YA BWANA YA 1. KATIKA MAJILIO

**(Mt 21:1–9)**

*Maelezo juu ya somo.*

1) Habari hizi ndizo habari za safari yake Yesu alipopanda kwenda Yerusalemu kuteswa na kufa. Somo hili linapatikana mara nyingine katika mwaka wa Kanisa, yaani katika Jumapili ya Mitende (Palm Sunday). Lakini Kanisa linalitumia somo hili kwa njia nyingine pia, yaani kuonyesha jinsi Bwana Yesu anavyoendelea kulifikia Kanisa lake na kufika kwa kila mmoja anayelisikia Neno lake.

2) Tunapohubiri juu ya somo hili ni vizuri kuonyesha ya kuwa Yesu ni Masihi (Kristo) kweli kweli, kwani anayatimiza Maandiko Matakatifu na maneno ya manabii juu ya Masihi.

3) Tena ni lazima kuonyesha ya kuwa Yesu anaendelea kufika hata siku hizi, kwa maana anafika hata kwetu kutuletea neema yake. Neema hiyo inatufikia katika Kanisa lake, na katika Neno la Mungu, na katika Sakramenti za Kanisa. Ili tukumbushwe sana juu ya mambo haya, habari zote zilizo kubwa zinasomwa, na kuhubiriwa, na kufundishwa katika mwaka mmoja, unaoitwa Mwaka wa Kanisa (Church Year), kutoka Advente (Majilio) moja mpaka Advente nyingine. Yesu hafiki kwetu wakati wa Advente tu, la, hufika kila siku, kila mara tunapomkaribisha na kumfungulia milango ya mioyo yetu (**Ufu 3:20**). Kazi ya Advente ni kutukumbusha sana juu ya majilio ya Yesu katika Kanisa lake, tena kutukumbusha ya kuwa Yesu atakuja tena katika hukumu yake ya mwisho.

Mafupisho ya hubiri juu ya somo hili:

### TAZAMA, MFALME WAKO ANAKUJA KWAKO

*1) Ndivyo zilivyosema ahadi za Mungu kwa sauti ya manabii.*

a) Neno hili lilikuwa limesemwa kwa watu wa Israeli mara nyingi.
b) Neno hili lilisemwa tena siku hii katika mji wa Yerusalemu, Bwana Yesu alipoingia huko. Basi neno hili lilitimizwa.
c) Wanafunzi wake Yesu walipoyafuata maagizo yake kwa habari ya punda na safari, yote yalitimizwa, kama yalivyokuwa yamesemwa katika Maandiko.
d) Mwenye punda na mwana–punda alipokubali kuwatoa kwa matumizi yake Yesu, hata mtu huyu alisaidia, yote yatendeke kufuatana na Maandiko.

e) Watu waliposhangilia na kutoa matawi ya mashamba, na mavazi yao, na kumwimbia Yesu HOSANA, basi kwa hayo yote Yesu alikaribishwa kwa kupatana na Maandiko.

*2) Tazama, mfalme huyu anakuja jinsi gani?*

a) Hakuna farasi wa kifalme. Hakuna gari la vita. Hakuna dhahabu, wala fedha, wala mapambo mazuri ya fahari. Kwa maana huyu hakufika kwa kusudi la kifalme wala kiserikali.
b) Punda ni mnyama wa mtu maskini. Hakuna tandiko zuri juu yake. Nguo za mavazi tu. Yaani huyu ni mtu mpole, kwa hiyo amepanda punda.
c) Yanayotukia sasa ni matengenezo tu ya matukio mengine yatakayofuata baadaye kidogo. Ndipo atakapoonyesha ya kuwa ni mtu mpole, siye mfalme wa ulimwengu huu (**Yn 18:36**). Sasa Yesu anaingia mji wa mateso na kufa kwake. Anaposalimiwa na mashangilio ya HOSANA anakaribishwa kuingia ufalme wake. Siku chache baadaye sauti kali zitasikika humu Yerusalemu zikilia *"Msulibishe, msulibishe"*. **Lk 23:21.**

*3) Tazama, mfalme wako anakuja tena!*

a) Maandiko yanaendelea kutimizwa katika Kanisa la Yesu. Haya yanatukia katika kila kanisa na kila usharika katika kila ibada. Lakini hasa yanatukia katika Siku ya Mitende (Palm Sunday) na Pasaka, Yesu anapoendea mateso yake na kufa kwake kwa ajili yetu.
b) Lakini Yesu anataka kuingia makanisa yetu, na nyumba zetu, na mioyo yetu. Basi, wapi punda, ambaye Yesu anaweza kumtumia ili kuingia sana hapa kwetu? Ni nani anayeweza kutoa punda wake? Ama ni nani anayeweza kuwa punda, ili Yesu aweze kuingia hapa katika mioyo ya watu?
c) Wapi watu wanaokata matawi na matunda ya mashamba yao, ili kumletea Bwana Yesu zawadi za kumkaribisha na sadaka zinazomfaa?
d) Wapi watu wanaoimba na kushangilia ili kumkaribisha Bwana Yesu na kuweka hata mavazi yao kama zawadi na sadaka kumshukuru na kumsifu?
e) Huyu anayekuja ni mfalme wako wa kweli. Je, umemngoja? Umemtengenezea njia kwa toba ya kweli moyoni mwako? Uko tayari kutoa hata mali yako, ili yeye aingie kwako kama mfalme? Katika Advente hii anataka kuingia kwako, autawale moyo na mwenendo wako na kila jambo. Basi, umkaribishe kwa njia hii: *"Mimi niko hapa. Karibu kwangu, Bwana Yesu!"*

# SIKU YA BWANA YA 2. KATIKA MAJILIO

**(Lk 21:25–36)**

*Maelezo juu ya somo.*

Katika masomo yote namna hii, yaani masomo yanayotoa habari za kurudi kwake Yesu, ni lazima kukumbuka mambo fulani, hasa ndiyo yanayofuata hapa.

1) Katika msemo wake juu ya kurudi kwake Bwana Yesu ameunganisha habari za shida zile zitakazotokea kabla ya anguko la Yerusalemu (na shida hizo *zimekwisha tokea*,kwa maana Yerusalemu ulianguka mwaka wa 70 A D ulipotekwa na Warumi) na shida zitakazotangulia kurudi kwake katika wingu. Yesu ameweka pamoja na kuunganisha habari hizi kwa kusudi fulani. Pengine shida zile zinafanana kwa ugumu wake, tena ni lazima kwetu kukesha na kungoja shida za mwisho, kama ilivyowapasa Wakristo wa wakati wa mitume kungoja matokeo yale mabaya juu ya Yerusalemu. *Shida zile za Yerusalemu zinaweza kufundisha Wakristo wa nyakati zote*. Ni lazima tukeshe, tuwe tayari, tusishikwe na hofu ama ghafula, shida inapofika. Tena, ingawa shida hizi zote ni kubwa sana, Yesu anataka kutufundisha juu ya ufalme wa mbinguni usioweza kutetemeka.
Kwa ajili ya habari hizi zilizowekwa pamoja ni lazima kuangalia, tusiseme maneno ama mambo fulani juu ya siku ya mwisho ambayo yamesemwa juu ya mji wa Yerusalemu tu. Pengine ni vigumu sana kujua kama neno fulani limesemwa juu ya Yerusalemu ama juu ya wakati wa mwisho. Tusipoweza kutambua haya, ni afadhali kunyamaza tu. Lakini bila shaka tunaweza kukaza jambo hili: *"Kesheni basi ..."* **Mk 13:35–37.**

2) Tunapata alama ama dalili zinazoonyesha ya kuwa majira yamekaribia (**Lk 21:8**). Lakini hatuwezi kusema sawasawa mwaka ama siku Bwana Yesu atakaporudi. **Mt 24:36.** Dalili za kufika kwake zinaweza kutusaidia tu, tuwe tayari kila mwaka na kila siku. Lakini haziwezi kupendeza mioyo yetu ya kibinadamu inayotaka kujua kabisa siku na saa. **Lk 21:7–9.**

3) Tunapohubiri juu ya kufika kwake Yesu katika wakati wa mwisho, tusisahau kuhubiri vile vile kufika kwake katika Kanisa lake kila mwaka, kila juma. Kwani Yesu anatufikia kila siku katika Neno na Sakramenti zake, na katika maombi yetu, na katika ushirika wa Wakristo wanapokutanika katika jina lake. **Mt 18:20.**
Inawezekana kuhubiri juu ya somo hili kwa njia ifuatayo.

## BWANA YESU ATARUDI

*1) Siku ile itawashika kwa ghafula wasiomjua Bwana Yesu.*

a) Siku ile itafika kwa ghafula, kama mtego unasavyo.
b) Watu wengi wanajiweka hapa ulimwenguni, kama ungekuwa mji unaodumu. Hilo ndilo kosa lao kubwa. **Ebr 13:14.** Wengine wanajua kweli ya kuwa Bwana wao atarudi, lakini wanajaribu kusahau neno hili na kujifurahisha kwa ulafi na ulevi na masumbufu ya maisha haya (mst **34; Mt 24: 48–51**).
c) Kujiweka hivi ni kosa kubwa sana, kwa maana hata mbingu na nchi zitapita.

*2) Siku ile itakuwa kama majira ya mavuno kwao wanaompenda Bwana Yesu.*

a) Nyakati na mimea duniani zinaweza kutufundisha, yaani katika wakati wa baridi ama wakati wa kiu ya nchi tunangojea kwa hamu nyingi wakati wa mvua ama wa mavuno (mst **29–30**). Wakati ule unapofika, tunafurahi kabisa. **Isa 9:3; Yn 4:35–36.**
b) Ndivyo rafiki zake Yesu wanavyongoja ya kuwa yeye atarudi. Kungoja kwao si jambo la hofu, bali ni jambo la shauku, kwa sababu wanangojea wokovu wao (mst **28**).
c) Wakristo hawa wakiangalia dalili zile za kurudi kwake Yesu, wanazifurahia, zinapoanza kutokea. Wanajiweka tayari zaidi **(Mt 25:4)** na kuomba: *"Na uje, Bwana Yesu"*. **Ufu 22:20.**

*3) Siku ile italeta hukumu.*

a) Makosa na upumbavu wao wasioamini zitaonekana zaidi.
b) Lakini hawawezi kujificha. Siku ya hukumu yao itafika, ingawa wanajaribu kuisahau. **Lk 23:30; Mt 24:48–51.**
c) Dalili zimewekwa katika jua, na mwezi, na nyota, zikionyesha ya kuwa kurudi kwake Yesu ni karibu. Dalili nyingine ni katika matukio yatakayotukia watu wa dunia. Wakristo wanaweza kuona dalili hizi na kuzilinganisha na Neno la Mungu. Wanategemea Neno la Mungu ya kuwa ni kweli (mst **33**). Wanajiweka tayari kwa maombi, wanakesha, wanaangalia maisha na mioyo yao (mst **34**) ili wapate kusimama vizuri mbele ya Mwana wa Adamu.
d) Wanajua ya kuwa wokovu wao unawafikia kutoka nje, yaani kutoka kwa Mungu (mst **28**). Wakiamini na kuomba na kukesha, ni kwa sababu wanamtaka Yesu, awaweke tayari kwa mavuno yake, yaani siku ile ya furaha atakapokuja (mst **27**). Hakuna hofu katika Mkristo anayemngoja Bwana wake kwa imani. **1 Yoh 4:17.**

# SIKU YA BWANA YA 3. KATIKA MAJILIO

### (Mt 11:2–10)

### MWOKOZI NA MTANGULIZI WAKE

*1) Mwokozi anatanguliwa na mjumbe wake.*

a) Imesemwa na manabii ya kuwa Masihi (=Kristo) atatanguliwa na mjumbe. **Isa 40:3–5; Mal 3:1–6.** Pengine mtangulizi huyu anaitwa Eliya, maana yake: ataonekana na kutenda kwa nguvu na roho ya Eliya wa Agano la Kale. **Lk 1:17.**
b) Mjumbe huyu atakwenda mbele yake Masihi na kumtengenezea njia.
c) Yohana ni Mtangulizi huyu. Hakuonekana kwa njia ya kupendeza watu (mst **7–10**). Kusudi lake lilikuwa kumtengenezea Yesu njia tu.
d) Yohana anatembea *"mbele ya uso"* wa Kristo, yaani anamwona kwa macho yake, aweze kumshuhudia mbele ya watu: *"Tazama, Mwanakondoo wa Mungu."* Kwa ajili ya jambo hili Yesu anamwita Yohana mkubwa kuliko wengine katika wazao wa wanawake (mst **11**), kwa maana hakuna mwingine katika Agano la kale aliyepata kumwona Yesu. **Ebr 11:13,39–40.**

*2) Mtangulizi huyu hawezi kuokoa, anatengeneza njia tu.*

a) Amewaonyesha watu dhambi zao. **Lk 3:7–14.**
b) Watu wengine walifikiri ya kuwa labda Yohana ni Mwokozi, lakini alikana hayo kabisa. **Lk 3:15–18.** Hawezi kuokoa, anatangulia tu.
c) Kweli ameshuhudu vizuri. Hata alipokaa gerezani alionyesha ya kuwa Kristo ni nani. Hakuweza kusema hayo mwenyewe, kwa sababu amefungwa, lakini alimwomba Yesu kutoa ushuhuda wake mwenyewe.

*3) Baada ya Mtangulizi anafuata Masihi mwenyewe.*

a) Yesu ameanza kazi yake mbele ya watu. Wengine hawakufahamu ya kuwa kazi yake ni kazi gani.
b) Yohana anapeleka neno kwa Yesu, akiomba ushuhuda kutoka kwake: *"Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?"* Ni kama kuuliza: Je, wewe ni Kristo, au tutangoja Kristo wa kweli afike?
c) Basi, Yesu alimfurahisha rafiki yake na mtangulizi wake, akisema: *MIMI NDIYE.* Hakusema neno lile lile, bali alisema: *Haya ndiyo matendo yangu* (mst **5**). Na matendo haya, ndiyo matendo ya Masihi!
d) Matendo haya ni matendo ya wokovu. Yanapatikana kwao wanaoamini. Ni habari za Agano Jipya. Yohana ni wa Agano la Kale. Kwa hiyo anaitwa mdogo: *"Aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye."* (mst **11**).

*Application:* Yesu anataka kufika kama Masihi na Mwokozi, hata sasa. Kuna mtangulizi wake. Ndiyo Sheria ya Mungu inayohubiri kama Yohana Mbatizaji, kwa maana inataka kukuonyesha dhambi zako. Ukiuliza: *"Tu-fanye nini?"* (Lk **3:10**) ni lazima kujua ya kuwa sheria haiwezi kukuokoa, wala huwezi kujiokoa mwenyewe kwa matendo mema. Lakini iko njia ya wokovu. Yesu mwenyewe anasema: *Tazama matendo yangu ya kusaidia vipofu, na viwete, na wenye ukoma, na viziwi, na wafu.* Kwa hiyo hata wewe unaweza kupata msaada katika umaskini wako, kwa sababu Mwokozi yuko hapa kupokea maskini na wenye dhambi.

# SIKU YA BWANA YA 4. KATIKA MAJILIO

**(Yn 1:19–28)**

## KUMTENGENEZEA KRISTO NAFASI

*1) Yohana Mbatizaji alifanya kazi namna hii.*

a) Alikuwa sauti ya mmoja aliaye nyikani: *"Inyosheni njia ya Bwana."*
b) Alifanya kazi hii kwa kuhubiri Neno la Mungu na kuieleza Sheria ya Mungu mbele ya watu. Kwa njia hii aliwaonyesha dhambi zao. **Lk 3:7–18.**
c) Kazi hii ilikuwa kazi Kisheria. Haikuweza kuokoa watu. Kwa hiyo alikana kabisa, watu walipomwuliza kama yeye ni Masihi.
d) Ubatizo wa Yohana si ubatizo kamili. Ulikuwa kama ahadi ya mambo yatakayokuja baadaye, yaani katika yeye atakayeanzisha ubatizo wa kweli. Ndio ubatizo katika Roho wa kweli. Ubatizo wa Yohana ulikuwa mzuri na mwema kwa wakati wake, lakini Yesu alipouamuru ubatizo wake, ule wa Yohana ulikoma.

*2) Kazi hii ya kumtengenezea Kristo nafasi inaendelea hata sasa.*

a) Yohana Mbatizaji amekufa. Hayuko sasa. Lakini ni kazi ya kila mhubiri kufanya kama Yohana alivyofanya: Kuihubiri Sheria ile kali, inayovumbua kabisa dhambi za watu.
b) Kazi hii inafanywa katika moyo wa kila mmoja anayesikiliza vizuri, Neno la Mungu linapohubiriwa. Mtu huyu atakata tamaa juu ya hali yake mwenyewe, akiuliza: *"Mwalimu, tufanye nini sisi?"* **Lk 3:12.**
c) Sasa Neno la Mungu limetengeneza nafasi kwa Kristo. Miungu ya uongo imebomolewa, sasa moyo ni mtupu. Ama Bwana Yesu aweza kuingia, ama roho zile mbaya zaweza kurudi tena. **Mt 12:44.**
d) Kazi hii ya kutengeneza nafasi, *sio wokovu*. Ni kazi ya Kisheria tu. Sheria inaweza kutengeneza nafasi kwa kuharibu yale ya zamani. Sheria inaweza kuwa Kiongozi kwa Kristo. **Gal 3:24.**

*3) Yesu anataka kuingia humu, alete wokovu na amani.*

a) Yohana Mbatizaji hakuweza kuleta haya (mst **27**). Mhubiri wa siku hizi hawezi vile vile. **Mdo 3:6.** Lakini katikati yetu anasimama huyu anayeweza (mst **26**). Kama Neno Takatifu ni katikati yetu, Yesu ni katikati yetu vile vile. **Mt 18:20.**
b) Yesu anaweza kuleta wokovu na amani, kwa sababu ana mamlaka ya kutoa ondoleo la dhambi. **Mk 2:9–11.** Yaani Yesu mwenyewe amekufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kama dhambi zimeondolewa, basi kuna wokovu, na amani, na furaha.
c) Ile furaha ya wokovu ni yake anayesimama karibu naye Kristo na kuisikia sauti yake. **Yn 3:29.**
d) Siku hizi, ambazo ni siku za kujiweka tayari kwa Kristmasi, kazi ya matengenezo inafanywa katika mioyo, ili kumtengenezea Bwana Yesu nafasi. Kwa hiyo, umkaribishe nawe, umtengenezee nafasi, apate kuingia katika nafasi ya moyo wako, na kuleta wokovu kwako, na furaha na amani.

# SIKUKUU YA KUZALIWA KWA YESU KRISTO (CHRISTMAS DAY)

**(Lk 2:1–20)**

*Maelezo juu ya somo.*

1) Tunapohubiri juu ya somo namna hii kuna hatari fulani inayotega wahubiri wengi. Hatari ndiyo hii: Mhubiri anapoona ya kuwa mwinjilisti Luka ameweka mbele yetu picha nzuri sana inayoweza kupendeza watu, anajaribu kuongeza uzuri wa picha zaidi, akisema ilitokea hii, ilikuwa namna hii n k. Lakini njia ile si kuuongeza uzuri wa picha, bali ni kuiharibu picha nzuri iliyowekwa na Luka. Kwa maana Luka amesimulia habari zile zote, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Hakuandika jambo lo lote lisilofaa. Sisi hatuwezi kuondoa lo lote, kama vile hatuwezi kuongeza lo lote.

2) Kwa hiyo ni kazi yetu kueleza somo lile kama lilivyo. Basi, maana ya somo hili ni nini? Mtoto yule alipozaliwa huko Bethlehemu, kweli ilitukia nini hapa duniani?
Tunaweza kujumlisha kifupi habari zote kwa njia hii:
a) Ahadi zilizotolewa zamani (katika Agano la Kale) ya kuwa Mungu atampeleka Masihi aliye Mwokozi wa watu, zilitimizwa huko Bethlehemu. **Ebr 1:1–3.**
b) Watu wale waliokuwako (Mariamu, Yusufu, wachungaji na wengine) hawakufahamu mara moja ukubwa wa mambo yale yaliyotukia.
c) Maana inayoonekana zaidi na zaidi ndiyo hii: Mungu ametufikia, yaani yumo katika mtoto huyu.
d) Basi, kuzaliwa kwake Yesu ni sehemu kubwa sana katika kazi ya Mwenyezi Mungu kuokoa watu wa ulimwengu huu. Kuzaliwa kwake Yesu ni kama mwanzo wa mambo mengi yatakayofumbuliwa zaidi na zaidi baadaye. – Yanayofuata ni mafupisho ya hubiri juu ya somo hili.

## TWENDENI MPAKA BETHLEHEMU, TUKALIONE HILO LILILOFANYIKA

*1) Tuone ya kuwa Mungu ametimiza ahadi zake kwa manabii.*

a) Ahadi nyingi zilitimia, Yesu alipozaliwa katika mji wa Bethlehemu. Nyingine hazikuwa tayari kutimia huko, k m ahadi juu ya kuteswa na kufa kwake.
b) Lakini tuone jinsi ahadi nyingine zilivyotimia huko Bethlehemu. **Ebr 1:1–3; Kum 18:15; Isa 7:14; Isa 9:6; Mik 5:2.**

*2) Tuone ya kuwa Mungu amemtuma aliye Mwokozi wa ulimwengu wote.*

a) Neno hili limefichwa kwa watu wengi, kwa sababu wanafikiri juu ya nchi takatifu kama nchi ndogo isiyo na maana sana, na Bethlehemu kama kijiji kilichofichwa. **Mt 2:5–6.**
b) Somo letu linatuonyesha ya kuwa ni kosa kufikiri hivi. Mambo yote makubwa hata ya ulimwengu huu yametukia na kutendwa huko karibu. Mwokozi amezaliwa mahali ambapo zinakutana nchi nyingi kubwa. Watu wa Misri na Sham, Asiria na Babilonia na Uajem, Ugriki na Rumi, wametembea huko alipozaliwa Mwokozi. Yerusalemu na Bethlehemu na Galilaya ni kama mahali pa katikati kabisa. Tunakumbushwa juu ya mambo hayo tunapopata habari za Kaisari Augusto na ufalme wake, na mamlaka yake juu ya "watu wote wa ulimwengu", yaani ulimwengu uliojulikana siku zile.

*3) Sasa ni furaha kuu mbinguni na duniani.*

a) Malaika wote wanafurahi, kwa sababu kazi ya wokovu imeendelea mbele sana. Mwokozi amezaliwa. Wale watakatifu waliongojea wokovu katika Agano la Kale wanafurahi. **Ebr 11:13, 39–40.**
b) Watakatifu wanafurahi hapa duniani, kama Mariamu na Yusufu. Wanafurahi kwa hofu,kwa maana wamepata hazina kubwa mikononi mwao, waitunze vizuri.
c) Wachungaji ni Washiriki wa kwanza katika Agano Jipya waliofurahia kuzaliwa kwa Mwokozi. Walifurahia Mmoja atakayeshinda dhambi zao, na umaskini, na hofu, na kifo, yaani mambo yale yaliyowasumbua wao kama sisi.
d) Nasi tumeitwa sasa kushirikiana na Wakristo wote wa duniani katika kumfurahia na kumsifu Mwokozi huyu, ili tuweze kumfurahia mwishoni mbinguni pamoja na malaika na watakatifu wote.

# SIKUKUU YA PILI YA KRISMAS (S:T STEPHEN'S DAY)

**(Mt 23:34-39)**

*Maelezo juu ya somo.*

Siku hii kuna hatari mbili katika kuhubiri kwetu: a) Tunaweza kuhubiri sawa na ile siku iliyotangulia, yaani Christmas Day, na kuhubiri juu ya Christmas na kuzaliwa kwake Yesu. Lakini kuhubiri hivi ndilo kosa. Kwa maana siku hii ya S:t Stephen ina maana yake ya pekee, ambayo imetupasa kuionyesha. b) Tunaweza kuhubiri sana juu ya somo letu, hata tusahau kuiunganisha siku hii na siku ile iliyotangulia, yaani Christmas Day. Lakini kuacha kabisa mambo ya Christmas, tunapohubiri siku ya S:t Stephen, ni kosa jingine. – Kwa hiyo, hubiri linalofaa linaeleza somo la siku hiyo, lakini pamoja na hayo linakaza uhusiano uliopo kati ya Christmas Day na S:t Stephen's Day. Inawezekana kuhubiri kwa njia ifuatayo.

## MASHAHIDI WAKE YESU KRISTO

*Dibaji:* Mungu ataka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. **1 Tim 2:4.** Kwa maana alimtoa Mwana wake wa pekee, aliyekuja hapa duniani Kristmasi ya kwanza. Utume mwema huu ulisikiwa huko Bethlehemu na wachungaji na wengine. Neno hili la Kristmasi, yaani kuzaliwa kwa Mwokozi, ni lazima litangazwe po pote duniani, kwa Wayahudi na mataifa. Lakini mashahidi hawa wa Yesu watakuta nini katika kazi yao?

*1) Mashahidi waifanya kazi ile kama walivyoagizwa.*

a) Yesu anapeleka *"Manabii na wenye hekima na waandishi"* (mst **34**), maana yake: wafanya kazi wa namna mbalimbali, watakaolitoa Neno la wokovu na kuonyesha watu ya kuwa Mwokozi kweli amefika ulimwenguni.
b) Anataka kuwakusanya watu, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake (mst **37**). Hiyo ndiyo picha ya wokovu na usalama na amani katika Kanisa lake Yesu Kristo na katika ufalme wake mbinguni.
c) Watakutangaza kurudi kwa Yesu kuhukumu watu. Yesu ndiye *"ajaye kwa jina la Bwana"* (mst **39**).

*2) Mashahidi wawe tayari kumshuhudia Bwana Yesu hata kwa uzima wao.*

a) *"Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea."* **Yn 1:11.** Kama walivyompokea Yesu, ndivyo watakavyowapokea mashahidi. Basi,

kulitangaza Neno la Mungu, mara nyingi ni kukuta hasira ya watu. Pengine watu watawaua mashahidi.
Yesu, aliye Neno, alizaliwa Bethlehemu, baada ya siku chache upanga wa mfalme ulimtafuta. Yesu, aliye Neno, alisulibiwa kwa ajili ya utakatifu wake na kwa ajili ya ubaya wa ulimwengu. – Stefano alipata kumshuhudia Bwana Yesu hata kwa kufa kwake. – Mtume Yakobo alikufa kwa ajili ya Neno. **Mdo 12:2.**
b) Yesu anaonyesha ya kuwa haiwezekani kufanya vita vyake hapa duniani pasipo ushuhuda wa damu (mst **34–36**).
c) Si kazi bure. Mashahidi wanapokufa kwa ajili ya Neno na imani wanaweza kuangalia mbinguni kama Stefano, **Mdo 7:56**, na kumwona Kristo utukufuni. Ni ushuhuda kwa wengine ya kuwa utume mwema ni kweli na ya kwamba shahidi hakufa bure.

*Application.* Nasi tumeitwa kuupokea ushuhuda wa mashahidi; nasi tumeitwa kuwa mashahidi kwa wengine.
a) Basi, umelipokea Neno la Kristmasi kwa njia gani, liwe neno tamu tu, au liwe Neno juu ya Mwokozi?
b) Kama ni Neno la wokovu, huwezi kukaa nalo kwa siri, bali litakushurutisha kutoa ushuhuda mbele ya ulimwengu.
c) Kama wewe bado tayari kutoa hata damu yako na uzima wako kwa ajili yake Yesu, hujampokea bado kweli kweli kama Mwokozi. Kama ni hivyo, umwombe Bwana Mungu ya kuwa Yesu azaliwe kweli katika moyo wako, kwa njia ya imani, awe Mwokozi wako kweli kweli. Omba tena, ya kuwa kwa Neno lake na Roho yake aithibitishe imani yako, uwe tayari hata kufa kwa ajili yake Yesu. Ndivyo mashahidi wengi wa zamani walivyofanya. Labda utaitwa nawe kuutoa ushuhuda ule.

# SIKU YA BWANA YA 1. BAADA YA KRISMAS

**(Lk 2:33–40)**

*Maelezo juu ya somo.*

Katika somo namna hii kuna hatari za namna mbili. a) Kusifu wazee wote kwa ajili ya wema na akili zao. Lakini si maana ya somo hili, kwa maana hawa wawili, Simeoni na Ana, walikuwa wazee *katika kulijua Neno la Mungu* na *katika tumaini la Israeli* na *katika imani ya kweli.* b) Kuhubiri sana juu ya *mtoto* huyu mchanga aliyeletwa hekaluni. Lakini katika hubiri letu imetupasa kufundisha hata juu ya Bwana na Mwokozi wetu. Kwa maana maneno yaliyonenwa juu ya mtoto Yesu yamenenwa juu ya kazi yake yote. c) Hatari hizi mbili pengine zinakwenda pamoja, tuseme kama mhubiri anatoa hotuba juu ya "wazee na watoto jinsi wanavyoweza kukutana na kushirikiana vizuri". Lakini hayo siyo nia ya somo hili! Bali hubiri letu liwe juu yake Yesu anayetimiliza maneno ya manabii anapofika hapa duniani.

## KUMTAMBUA BWANA YESU KRISTO

*1) Watakatifu hawa wawili walimtambua Yesu.*

a) Walikaa nyumbani mwa Mungu siku kwa siku, mwaka kwa mwaka.
b) Walikaa katika nuru ya Neno la Mungu, wakiongozwa na Neno katika kila jambo.
c) Walingoja faraja ya Israeli (mst **25**) na ukombozi kwa Yerusalemu mst **38**).
d) Walikuwa watu waliozoea mambo ya ufalme wa Mungu, kwa njia ya ibada, na kufunga na kuomba (mst **37**).
e) Kwa hiyo waliweza kumtambua Yesu, alipoletwa hekaluni, ingawa alikuwa bado mtoto mchanga.
f) Kwa hiyo wanaweza kutusaidia sisi sote wa nyakati nyingine kumtambua Bwana Yesu, ingawa anaonekana katika unyenyekevu na umaskini. **Flp 2:7.**

*2) Wanaomtafuta kweli Bwana Yesu wanaweza kumtambua.*

a) Haiwezekani kwa kila njia ama kila mahali, la!
b) Wanaomtafuta hekaluni, na katika Maandiko Matakatifu, na katika sakramenti na maombi, hawatafuti bure, bali watamtambua.
c) Hawa wanamtambua Yesu ya kuwa ni Masihi na Mwokozi, ingawa wengine wanasema: "Ni kama mtoto tu", au "Ni mwalimu mjinga" au "Hana elimu inayofaa katika nyakati zetu za maendeleo makubwa" n k.
d) Kwa watu wanaomtafuta kwa njia hizi anajidhihirisha kama Mwokozi wa kweli.

*3) Lakini haitoshi kumtambua Yesu ya kuwa yeye ni nani. Ni lazima kumpokea kama Mwokozi.*

a) Simeoni na Ana walijua mambo haya (mst **34–35,38**).
b) Asiyesimamishwa naye Yesu ataangushwa (mst **34**).
c) Upanga ulimchoma hata Maria mamake, mpaka alipomkubali Yesu kama Mwokozi (mst **35**). **Yn 19:25.**
d) *"Ishara itakayonenewa"* ni kufa na kufufuka kwake Yesu. **Lk 11:29.** Wanaokubali kufa na kufufuka kwake Yesu kama kazi ya wokovu na kuyaamini hayo wenyewe, wanaokoka. Bali wanaokataa wanapotea. **Flp 3:18–19.**
e) Kwa hiyo ni lazima upanga wa Neno (mst **35, Efe 6:17**) lipate kutuchoma mioyo yetu, tupate kuamka na kugeuka. Ndiko kuamini na kuokoka kwa ajili yake Yesu aliye faraja ya Israeli na ukombozi wa Yerusalemu.

# SIKU YA MWAKA MPYA
# (NEW YEAR'S DAY)

**(Lk 2:21)**

*Maelezo juu ya siku hii.*

Katika Mwaka wa Kanisa kuna siku nyingine iliyo siku ya kwanza, ndiyo Jumapili ya kwanza ya Advente (mwishoni mwa Novemba ama mwanzoni mwa Desemba). Lakini Kanisa linaangalia hata mwaka mpya wa ulimwengu huu. Kwa maana sisi sote tunaona jinsi wakati unavyokimbia upesi. Tunaona ya kuwa ni lazima kuchungulia mambo yalivyokuwa katika wakati uliopita na kukumbuka wajibu wetu katika siku zijazo.
Lakini hata mwaka mpya wa ulimwengu huu utawekwa katika nuru ya Neno la Mungu, na ufunuo ule uliomo katika Yesu Kristo. Kwa hiyo ni vizuri sana ya kuwa somo la siku hii ni somo juu ya jina lile *Yesu*. Kwa maana tusipoingia katika mwaka huu mpya katika jina lake Yesu Kristo, mwaka huu hauwezi kufaulu, wala hauwezi kuleta mbaraka.

## JINA LAKE YESU

*1) limekuwako tangu milele.*

a) Jina hili linapatikana katika Agano la Kale. Halionekani kwa umbo hili *Yesu* (*Yesu* ni jina la Kiyunani kama majina mengine katika Agano Jipya). Lakini linapatikana kama *Yoshua* (*Yoshua* ni jina la Kiebrania kama majina mengine katika Agano la Kale). Ni jina lile lile. Maana yake ni *Bwana anaokoa* ama *Bwana ni wokovu*.
b) Haya yanaleta maana kubwa: Bwana Yesu amepokea jina sawa na yule kiongozi wa Israeli aliyewaingiza watu wake katika nchi ya ahadi.
c) Lakini Yesu ni mkubwa kuliko Yoshua. Huyu aliingiza watu katika nchi ya ahadi hapa duniani, lakini Yesu anaingiza watu wa makabila yote katika nchi ya ahadi mbinguni.
d) Yoshua hakuimaliza kazi yake, *"maana kama Yoshua angaliwapa raha, (Mungu) asingaliinena siku nyingine baadaye. Basi imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu."* **Ebr 4:8.**
e) Lakini Yoshua hakutangulia kulitumia jina hilo. Wa kwanza ni Yesu. Ametajwa katika ahadi ya **Mwa 3:15**. Tena Biblia inasema ya kuwa Mungu amekuwa na nia hii tangu mwanzo kuvijumlisha vitu vyote katika Yesu. **Efe 1:10; Flp 2:9.**
f) Yesu alipofika hapa duniani alipewa jina hilo, *Yesu*, maana yake, *"yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."* **Mt 1:21.**

*2) maana yake ni kutuongozasote, tutubu.*

a) Maana hii haionekani mara moja. Lakini Mwokozi anaweza kuokoa wenye dhambi tu. Wanaofikiri wenyewe ya kuwa wana haki, hawahitaji wokovu. **Lk 15:7.** Yesu amefika kwa kazi iyo hiyo tu, ya kuokoa wenye dhambi.

b) Hapa tukumbuke ya kuwa *wokovu* una pande mbili. Upande huu ni wokovu ule uliotengenezwa naye Yesu Kristo alipokufa msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Upande huu ni wokovu utakaokuwa wako, ikiwa unamwendea Bwana Yesu Kristo kwa kutubu na imani. Kwa hiyo tunasema *"siku ya wokovu ndiyo sasa"*, **2 Kor 6:2**, ingawa Yesu aliutengeneza wokovu kamili zamani sana.

c) Siku hii, iliyo siku ya kwanza ya mwaka mpya, inaleta nafasi nzuri kuuchungulia mwenendo wako katika mwaka uliopita. Je, ulikuwa mwenendo katika Yesu na katika njia ya wokovu? Na mwaka huu utakuwaje? Labda ni mwaka wa mwisho. **Lk 13:8–9.**

*3) ni kimbilio salama.*

a) Mwanzoni mwa mwaka mpya watu hufikiria siku zijazo. Kama shida zitatokea, waende wapi kutafuta msaada? Je, kwa rafiki, au kwa wakubwa fulani, au wategemee mali na pesa? Au wajifiche mahali palipo salama? Makimbilio yote namna hii ni bure, kama shida zitatokea kweli.

b) Kuna kimbilio moja tu linalofaa. *"Mungu wa milele ndiye makazi yako, na mikono ya milele i chini yako."* **Kum 33:27.** Makazi (kimbilio) haya yanapatikana kweli katika mwaka huu, kwa maana unaweza kumkimbilia Mungu katika Neno lake, katika maombi yako, katika sakramenti, na katika ushirika wa Wakristo. Haya yote ni kwa ajili yake Yesu Kristo, yanapatikana katika jina lake tu. Ni jina linalofaa tangu milele. Kuna wokovu katika jina hilo tu. **Mdo 4:12.** Kwa hiyo umwendee kwa toba ya kweli katika mwaka huu mpya.

# SIKU YA BWANA YA 2. BAADA YA KRISMAS

**(Yn 1:14–18)**

## UTIMILIFU WAKE YESU KRISTO

*1) Yesu Kristo anatufunulia Mungu ni nani.*

a) Torati ilitolewa kwa mkono wa Musa (mst **17**).
b) Yesu anaiendeleza kazi hii, yaani anadai utii wa kweli, na utakatifu wa moyo. **Mt 5:17–18,20,22,28,39,44,48.**
c) Kwa hiyo anaifunua kweli yenyewe, yaani kweli juu ya Mungu, ya kuwa yeye ni nani, na kweli juu yetu, ya kuwa sisi ni wa hali gani. Anaonyesha ya kuwa sisi ni wenye dhambi, kwa maana hatuwezi kuibadili mioyo yetu. **Yer 13:23.**
d) Kwa njia hii anaifunua neema vile vile. Kwa maana mashtaka magumu ya Sheria yanamwongoza mwenye dhambi kwake Kristo. **Gal 3:24.**

*2) Yesu Kristo anatushirikisha naye Mungu, tupate neema kwake.*

a) Neema na kweli ni mamoja katika Yesu. Kwa hiyo anahitilafiana kabisa na watu. Watu wanakaza sheria pasipo neema (njia ya kifarisayo), au wanakaza neema pasipo sheria: *"... wabadilio neema ya Mungu wetu kwa ufisadi."* **Yud, mst 4.**
b) Kwa sheria yake Mungu anataka kutuongoza, tuipokee neema yake. **Hos 11:4.**
c) Anayeipokea neema hii ataona na kupokea neema kubwa tena, *"neema juu ya neema"*. Anayempokea Yesu na neema yake anaona vizuri zaidi dhambi zake mwenyewe. **Lk 5:8; 1 Tim 1:15.** Hata hapa ni lazima kuikimbilia neema. Kwa njia hii Mkristo aliyepokea neema nyingi ataomba neema tena kwa ajili ya udhaifu wake.
d) Wanaoendelea hivi katika neema wanaona *"neema juu ya neema"* au *"jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu."* **Rum 11:33.**

# SIKU YA BWANA YA UFUNUO (EPIFANIA)

**(Mt 2:1–12)**

*Maelezo juu ya somo.*

Iko hatari kubwa hapa, yaani tunaweza kujaribiwa kuleta mawazo yetu juu ya nyota na mamajusi na safari yao. Lakini kama wahubiri hatuna ruhusa kuingiza maono yetu yasiyo mafundisho ya Neno la Mungu. Tuhubiri yaliyomo katika Neno la Mungu tu!
Katika makanisa mengi ya dunia sikukuu ya Epifania ni *sikukuu ya kazi ya mission*, yaani Wakristo wanakumbuka jinsi mamajusi walivyofika kutoka nchi za mashariki kumwona Yesu, kwa hiyo wanajikumbusha ya kuwa ni wajibu wao kuletea hata wengine Injili ya Wokovu. – Nasi tukumbuke upande wetu ya kuwa tuna wajibu huu, kwa sababu Neno limetufikia. Tumepokea habari njema bure, basi tuwe tayari kutoa bure. **Mt 10:8.**

## NJIA YA KUUPOKEA WOKOVU ULIOFUNULIWA

*1) ni kuupokea mwito wa Mungu.*

a) Mwito wa Mungu unaweza kufika kwa njia mbalimbali. Watu huitwa kwa msaada wa kazi ya mchungaji, mwinjilisti, mwalimu wa skuli, au kwa msaada wa rafiki ama Mkristo mwingine anayemkaribisha kumwendea Mungu. Mamajusi waliitwa kwa njia ya pekee. Hatujui wengine walioitwa kwa njia ile. Kwa hiyo tusifikiri ya kuwa tutaitwa kwa nyota ama ndoto ama kadhalika. Mungu anatuita sisi kwa njia za kawaida, yaani kwa Neno linalohubiriwa, ama kama mwanafunzi mmoja akimwita mwenzake.
**Yn 1:37,42,46.**
b) Kama tumeitwa naye Mungu, ni lazima kuutii mwito huu.
c) Mara nyingi italeta shida na mateso kuufuata mwito wa Mungu. Mamajusi waliiacha nchi yao na jamaa zao. Mathayo alitoka kazini, **Mt 9:9**, kwa ajili ya mwito wake Yesu, Ibrahimu alitoka nyumbani mwa babake. **Mwa 12:1.**
d) Ingawa tunaruhusiwa kukaa katika nchi yetu na nyumbani mwetu, lakini tumeitwa sote kuacha ushirika wa dhambi na walimwengu.**Lk 9:62.**

*2) ni kupitia shida nyingi.*

a) Walimwengu wataanza kuwa adui wetu. Herode alikuwa adui wa ufalme wa Mungu; ingawa alisema ni rafiki ya mfalme mpya (mst **8**) alitaka kumharibu pamoja na mamlaka yake.
b) Hata makuhani na walimu wa Neno la Mungu walikuwa maadui wa Neno katika mioyo yao. Mungu aliwaambia mamajusi wasishirikiane nao.
c) Anayetaka kuwa Mkristo atakuta walimu wa Neno la Mungu, labda hata

wachungaji na maaskofu, wanaochukia na kupinga Neno la Mungu. Wana jina la Kikristo tu. Wamevaa mavazi ya kondoo tu, lakini ni mbwa–mwitu wakali. **Mt 7:15.** Hapa walioitwa wajiangalie. Wafuate Neno la Mungu kuliko watu. **1 Yoh 4:1.**
d) Pengine utaingia katika shaka za moyo na mawazo mabaya. Ni kama nyota iliyokuongoza inajificha, unaanza kuulizauliza watu (mst **2** na **9**). Lakini ukitumia Neno la Mungu na kulitegemea, shida itakwisha, na nyota ile itakuongoza tena, mpaka ufike kwenye mahali pa Yesu (mst **9**).

*3) ni ile ile ya kulifuata Neno la Mungu.*

a) Watu wengi wanahoji, wakikataa Neno. Wanasema ni ujinga. Ndivyo wengine walivyosema juu ya safari ya mamajusi. Lakini hawa waliifuata nuru ya nyota, hata wakamwona Kristo.
b) Kama umeitwa na Mungu, wengi watajaribu kulinyima Neno la Mungu kutoka moyo wako na kuiharibu imani yako. Watajaribu kukuonyesha njia nyingine. Lakini lifuate Neno la Mungu tu. Hakuna njia nyingine. **2 Tim 3:15–16.**

*Application.* Kama umeitwa na Mungu, endelea tu kulitumia Neno lake. Nyota inayong'aa imo katika Neno. Linaweza kukusaidia, hata ufike kwake Kristo. Shida labda zitatokea, uwe tayari tu kuzivumilia kama mamajusi. – Na kama umemwona Kristo na wokovu wake, ni kazi yako kumshuhudia yeye, wengine wavutwe kwake, ambao hawajaona bado njia ya wokovu. Kwa maana wote wameitwa kutoka gizani na kuingia katika nuru ya ajabu ya Kristo. **1 Petr 2:9.**

# SIKU YA BWANA YA 1. BAADA YA UFUNUO

**(Lk 2:41–52)**

*Maelezo juu ya somo.*

Hatari hapa ni kuhubiri juu ya *mtoto mzuri* au *mtu aliyeanza mapema, na kwa hiyo alifaulu katika kazi yake*. Mwinjilisti Luka hana kusudi kutoa habari za namna hii! Bali anataka kuonyesha ya kuwa hata katika utoto wake Yesu aliufunua utukufu wa Baba yake na ya kuwa alikaa karibu naye Mungu kuliko mtu ye yote duniani.
Kwa hiyo tushike hasa mambo haya matatu: a) Yesu anaonyesha ya kuwa ametoka kwa Mungu, kwa hiyo anaweza kuufunua utukufu wa Mungu. b) Yesu anafunua haya katika Hekalu na kwa kuyaeleza Maandiko. c) Hata siku hizi Yesu anaendelea kuyafunua mambo ya ufalme wa Mungu, katika Hekalu (yaani Kanisa lake Takatifu) na kwa kutueleza sisi Maandiko Matakatifu.

## KAMA YESU YUKO HEKALUNI

*1) anazitimiza ahadi za Mungu.*

a) Kijana Yesu anasimama katika Hekalu, akiwa mtu kama sisi, lakini Mungu alikuwa katika kijana huyu, yaani ni Mwana wa Mungu.
b) Hivi Mungu alizitimiza ahadi zake kwa Ibrahimu, na Musa, na Daudi, na manabii. Yaani huyu kijana atakuwa mtu wa imani wa kumshinda Ibrahimu, na mtu wa Sheria wa kumshinda Musa, na mfalme mkubwa kuliko Daudi (**Lk 1:32; Mt 22:45**), na kuhani mkuu wa kumshinda Haruni na Melkizedeki, na nabii mkubwa kuliko Eliya na Isaya.
c) Kama mtoto wa siku 8 alikuwapo Hekaluni, lakini sasa anaanza kuonyesha yeye ni nani.
d) Ndivyo ilivyo hata sasa: Kama Yesu yuko Hekaluni, basi anatimiza Maandiko. Anatuonyesha utukufu wa Baba yake. Yaani *"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele."* **Ebr 13:8.**

*2) ukubwa wake umefichwa kwa watu walio wengi.*

a) Hata Mariamu na Yusufu wameshindwa kufahamu jinsi Yesu alivyokuwa (mst **50**).
b) Wengine waliokuwa pamoja nao safarini au Hekaluni walishindwa vile vile.
c) Yesu anapokaa pamoja nasi Hekaluni, walio wengi wanashindwa kumfahamu. Hawauoni utukufu wake. Labda wanamshtaki na kusema amekosa katika mambo fulani, kama Mariamu alivyomshtaki (mst **48**).
d) Ingawa sisi tunashindwa kumfahamu, yeye anafunua utukufu na upendo wa Mungu. Kosa ni letu. Kama tutamfahamu na kumwita Mwokozi wetu, ni lazima macho yetu yafumbuliwe, na mioyo yetu ifumbuliwe vile vile. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu. Pasipo kazi hii hatuwezi kumwona Yesu. **Lk 24:31; 24:45; Yn 9:30; Mdo 16:14; 26:18.**

*3) ni lazima kumtafuta.*

a) Inaonekana kama maneno haya yanapingana. Lakini utukufu wake Yesu unaoonekana Hekaluni umefichwa kwa macho ya walimwengu. Hata Mariamu na Yusufu na wengine wa jamaa ya Yesu walishindwa kuuona utukufu wake kwa muda fulani. **Mt 13:57.** Waliomwona ni wale waliokuwa vipofu na viwete na wenye dhambi, kwa sababu walikuwa na njaa na kiu ya kumwona. Kwa watu namna hii alijifunua.
b) Ndivyo ilivyo hata sasa. **Mt 5:6; 8:2; 9:12; Lk 19:10; Yn 11:40.**

# SIKU YA BWANA YA 2. BAADA YA UFUNUO

**(Yn 2:1–11)**

*Maelezo juu ya somo.*

a) Hapa ni lazima kukumbuka ya kuwa katika Israeli na Agano la Kale *divai ni mfano wa furaha*. Anayeweza kubadili maji ya kila siku yawe divai, huyu amebadili hali ya watu kabisa. Ufalme wa Mungu umefika kati ya watu.
b) Mabalasi, yaliyokuwa sehemu ya kazi ya Wayahudi kujitakasa (kutawadha) yakajazwa na divai ya Masihi na ya Ufalme wa Mungu. Kazi hii ya Yesu inafanana na kazi yake ya kuwalisha makutano kwa mkate na samaki. Kwa mfano ulioonekana alitoa habari za ufalme wa mbinguni.
c) Kwa mwujiza huu Yesu ameonyesha ya kuwa yeye ameingia badala ya Mafarisayo. Badala ya masharti yao ya kujitakasa wenyewe, ameleta ufalme wa furaha, maana yake ni wokovu kwa njia ya neema. *"Akaudhihirisha utukufu wake."* Utukufu wake, ndio utukufu wa Masihi na utukufu wa ufalme wa Mbinguni.

## JINSI YESU ANAVYOFUMBUA FURAHA YA MBINGUNI

*1) Anaifumbua nyumbani na katika jamaa za watu.*

a) Yesu angaliweza kujipatia mwenyewe njia ya furaha, lakini alikataa kufanya hivi (**Mt 4:1–4; Ebr 12:2**) ili kutengenezea watu wokovu.
b) Aliingiza furaha yake katika jamaa hii ya Kana, tangu mwanzo wa jamaa hii, yaani tangu siku ya arusi.
c) Ingawa yeye alikuwa mgeni katika nyumba ile, alionekana kama Bwana wa nyumba na yule anayekaribisha karamuni. **Ufu 3:20.**
d) Kama Yesu yupo, furaha ya kweli ipo, huzuni haiwezekani. **Mt 9:15.**

*2) Anaifumbua furaha ile katika miujiza (ishara).*

a) Miujiza si njia ya kujipatia sifa ama mamlaka juu ya watu.
**Mt 4:5–7.**
b) Yesu alipo, ndipo mamlaka ya mbinguni ilipo vile vile. **Yn 2:11; 2:23; 11:40.** Yesu anapotaka kuonyesha utukufu wake wa mbinguni, anaweza kufanya miujiza.
c) Miujiza hiyo haifiki kwa mapenzi ya watu. Yesu alikataa kufanya miujiza huko Nazareti (**Mt 13:58**), mbele ya mfalme Herode (**Lk 23:8–9**), alikataa hata maombi yake Mariamu (mst **4**). Anaifanya miujiza kwa wakati unaompendeza yeye tu. Kwa hiyo utukufu wa mbinguni utaonekana wakati fulani, wakati mwingine hauonekani.

*3) Anaifumbua furaha ile katika Kanisa lake.*

a) Mambo haya yote ya furaha yaonekana kila siku katika Kanisa lake, yaani Kanisa ni jamaa kubwa ya Yesu. Katika Kanisa kuna Neno, sakramenti, maombi, ondoleo la dhambi, ushirika wa kweli, uzima, amani na wokovu.
b) Labda Yesu anakaribishwa katika makanisa yetu kama mgeni, lakini akipata nafasi atajidhihirisha kama Bwana mkubwa.
c) Kwa hiyo ni kazi ya Kanisa kueneza furaha ile ya arusi, **Mt 9:15**, yaani furaha ya milele na furaha ya mbinguni, kati ya watu.

*Application.* Kila mmoja amealikwa kuhudhuria Arusi Kuu. – Je, unazuiliwa na mambo gani kushirikiana katika furaha hiyo? Usipokubali kupokea mwito huu, kweli hutaona furaha ya mbinguni.

# SIKU YA BWANA YA 3. BAADA YA UFUNUO

### (Mt 8:1–13)

### IMANI HODARI

*1) Imani hodari inaanza katika shida.*

a) Mwenye ukoma alikuwa najisi. Alikuwa amefukuzwa kutoka ushirika wa watu safi (**Law 13:45–46**), alikuwa kama mfu. Huyu mtu katika **Mt 8** alimsihi Yesu kutoka shida kubwa mno.
b) Shida ya akida haikuwa yake hasa. Lakini alijishirikisha naye mtumishi wake, hata akiona shida ya mtumishi kama shida yake mwenyewe.
c) Watu hawa wawili walishurutishwa na shida zao kumwendea Yesu na kuomba msaada wake.
d) Nawe, kama utamwamini Yesu, hutaanza kuamini unaposhinda vizuri mwenyewe. Imani itaanza kidogo unapomsihi Bwana Yesu kutoka shida yako.

*2) Imani hodari inaanza kama imani dhaifu.*

a) Mwenye ukoma alianza kuamini kwa udhaifu mwingi. Amesikia habari zake Yesu, alimtafuta katika mkutano wa watu. Alipoingia kati ya watu alivunja sheria, lakini shida yake ilimshurutisha. Alimsihi Yesu kwa ombi la mwenye imani ndogo: *"Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa."*
b) Akida aliomba msaada kwa mtumishi wake. Alikuwa tayari kufukuzwa: *"Mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu"*, lakini shida yake ilimshurutisha kumwomba Yesu.
c) Wote wawili, walipomsihi Yesu kutoka shida zao, walisikia jibu lake la neema: *"Nataka; takasika"*, na *"Nenda zako, na iwe kwako kama ulivyoamini."*
d) Ndivyo imani inavyoumbwa katika moyo wako. Si kwa bidii zako, wala kwa maendeleo yako siku kwa siku. La, unapomwomba Yesu kutoka udhaifu wako, baada ya kukata tamaa juu yako mwenyewe, Yesu asema Neno lake imara: *"Iwe kwako kama ulivyoamini."*

*3) Mwenye imani anakaribishwa kwenye meza ya Yesu mbinguni.*

a) Maana yake si ya kuwa anachagua watu wenye imani hodari tu. Yesu alikula chakula na wenye dhambi, ingawa walikuwa na imani ndogo tu. **Lk 15:1–2.**
b) Yesu anapokea wenye dhambi hata sasa. Ndivyo tunavyopokewa kwenye meza ya Bwana kanisani. Huko kuna ondoleo la dhambi kwa watu wanaohangaika kwa ajili ya dhambi zao.
c) Meza hii ya neema duniani ni kama mfano wa meza ya mbinguni (mst **11**). Watakaofika kwenye meza ya Mungu mbinguni si watu wenye uhodari, bali ni watu waliomsihi Yesu kutoka shida kubwa.
d) Imani hii si kazi ya watu. **Yn 3:27.** Ni kazi ya Neno imara, tena ni kazi ya Roho Mtakatifu. *"Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo."* **Rum 8:26.** Roho anatueleza Neno la Mungu. Anatusaidia kumsihi Kristo. Kwa njia hii imani ya kweli inaumbwa.

# SIKU YA BWANA YA 4. BAADA YA UFUNUO

### (Mt 8:23–27)

### KUOKOLEWA KATIKA TUFANI NA FADHAA

*1) Bahari na tufani zinaweza kutuogofya.*

a) Neno la Mungu halifichi hatari zetu kubwa. Linatufundisha wazi juu ya hatari zinazoweza kutukuta.
b) Neno linatoa habari za bahari na tufani ya kuwa zinaleta hatari kwa watu na kuwatisha sana. **Zab 89:9; Yon 1:4; Lk 21:25.**
c) Lakini ingawa bahari na tufani na mawimbi ni hatari zenyewe, ni hasa mifano katika Biblia, ili kuonyesha hali ya mtu au makabila ya watu, kwa kuwa hawana raha ama amani, bali wanafadhaika. **Isa 57:20; Yer 49:23.**
d) Hali hii, kama mawimbi ya bahari, imo hata katika mioyo ya watu. **Zab 42:7.**

*2) Aliyeiumba bahari ndiye aliye Bwana wa bahari na mawimbi.*

a) Anaweza kuziamuru. **Zab 89:9; 65:7.**
b) Kama Baba Mwenyezi alivyo na mamlaka juu ya ulimwengu mzima, naye Mwana anayo mamlaka hii (mst 27). **Yn 10:25; 10:30; 10:37; 14:9.**
c) Kwa hiyo Mwana, aliyeshirikiana na Baba katika kuuumba ulimwengu (**Yn 1:3**), ndiye anayeweza kukemea bahari na mawimbi, hata uvumi ule uliomo katika mioyo ya watu, akawatulize. **Yn 14:1; Kol 3:15.**

*3) Kuokolewa katika tufani na fadhaa, ndilo jambo la imani.*

a) Itawezekana kuokoka, kama Yesu yu pamoja nasi chomboni (mst **23, 25**).
b) Kama yeye yuko, hakuna tufani ambayo itaweza kutushinda. Hakuna mawimbi ama shida zinazopita uwezo wake Yesu. Kama Yesu yuko pamoja nasi, tunayo sikuzote njia ya kumwomba, atusaidie (mst 25).
c) Hii ni kweli hata juu ya mahangaiko ya mwisho. **Lk 21:25; Mt 24:9–14.** Katika dhiki zile watakaookolewa, ndio walio na imani. **Yn 11:25, 26,40.**

# SEPTUAGESIMA

**(Mt 20:1–16)**

*Maelezo juu ya somo.*

Kwa somo hili Yesu hasemi ya kuwa sisi tutengeneze mambo ya kazi na mishahara kama mwenye shamba na msimamizi wake walivyofanya. Yaani somo hili si mafundisho juu ya ukulima au mambo ya ulimwengu, wala si mafundisho juu ya haki ya wafanya kazi kupokea malipo yaliyo haki. Mafundisho juu ya njia nzuri kulipa wafanya kazi yameandikwa **Lk 10:7; Yak 5:4–6; 2 Tim 2:6 n k.**
Katika somo hili Yesu anafundisha juu ya ufalme wake na neema ile inayotawala huko. Wanaoingia huko wanaingia kwa neema tu, hakuna njia nyingine. Anayetaka kuingia kwa ajili ya haki yake hawezi kuwamo. **Mt 22:12.**
Kwa hiyo, tunapohubiri juu ya somo hili tusichanganye mambo ya ufalme wa Mungu na mambo ya kazi na malipo katika ulimwengu huu. *Somo hili ni mfano* unaoonyesha Mungu anafuata taratibu gani katika ufalme wake.

## NEEMA KUBWA YA MUNGU

*1) Kwa neema yake kubwa anaita watu mara nyingi, waingie ufalme wake.*

a) Mwenye shamba alitoka mara nyingi kutafuta wafanya kazi.
b) Ndivyo Bwana Mungu anavyoita watu, ili waingie ufalme wake.
c) Habari hizi za ufalme wa Mungu, ndizo habari njema: *"Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari."* Mwito huu umefanywa mara nyingi. **Mt 23:37.**

*2) Kwa neema yake kuu Mungu anatoa yote yanayopatikana katika ufalme wake.*

a) Watu hutoa kidogo kidogo, kwa maana wanataka kushika sehemu iliyo kubwa wenyewe, au wanapenda kidogo tu.
b) Mungu hatoi sehemu ndogo ndogo. Hawezi kukata uheri ama furaha za ufalme wake sehemu sehemu na kutoa kwa kila mmoja sehemu ndogo, au kwa mmoja sehemu kubwa na kwa mwingine sehemu ndogo. Hawezi, kwa sababu upendo wake ni kamili.
c) Anapoufungua mlango wake wa neema, anatoa utukufu wote wa mbinguni na wokovu kamili.
d) Anayegombana na Mungu juu ya *haki* inayokosa katika haya (mst **11**), hajui haki ni nini. Kama haki itafuatwa, basi tutoke ufalme wake, yaani hatuna ruhusa kuwamo! Kama tutaingia na kuwamo, ni kwa wema wa Mungu tu.

*3) Inawezekana kuchelewa kuipokea neema ile.*

a) Ingawa wengine walianza kufanya kazi yao shambani saa 11 jioni, hatuwezi kufikiri ya kuwa tutaingia ufalme wa mbinguni tunapokaribia uzee wetu. Hatujui kama tutafika uzee. Wengine watakufa kama vijana, wengine kati ya ujana na uzee. – Ya kuwa wafanya kazi waliingia hata saa 11 inaonyesha ya kuwa Mungu anapokea wenye dhambi, ingawa wamechelewa, kama alivyompokea yule mnyang'anyi msalabani.
b) Lakini watu wasingoje saa ile ya mwisho. Wakati ule mioyo inaweza kuwa migumu. Labda haiwezekani kugeuka ama kuamini siku ile. **Mdo 19:9; Ebr 3:13.**
c) Unapoitwa, iwe saa ya asubuhi ya maisha yako, au saa 9 au 11 ulipo mzee, usichelewe kusikiliza. Kwa maana siku ya leo ni siku ya wokovu. **2 Kor 6:2.** Siku nyingine moyo utakuwa mgumu, au utakuwa umekamatwa kabisa ulimwenguni, au mlango umekwisha fungwa. **Mt 25:10.**

# SEXAGESIMA

### (Lk 8:4–15)

### KULIPOKEA NENO LA MUNGU

*1) Njia isiyofaa.*

a) Njia isiyofaa ni kulipokea kama wale wanaoitwa *karibu na njia*. Kwa maana mbegu zilikanyagwa, ndege wakazila. *Njia*, maana yake ni watu wenye mioyo migumu. Wanapolisikia Neno la Mungu, hawaliangalii, bali Shetani anapeleka watumishi wake, waliondoe Neno kama mbegu njiani.
b) Njia isiyofaa ni kulipokea kama wale wanaoitwa *mwamba*. Kwa maana ulikuwapo udongo haba tu juu ya mwamba, kwa hiyo mbegu ziliota upesi, na kukauka na kufa upesi. – Ndivyo ilivyo katika watu fulani. Wanasikiliza kwa furaha mwanzoni, hata inaonekana ya kuwa kazi ya Mungu inaendelea katika mioyo yao, kumbe, imekufa tena kwa haraka. Kwa nini? Mara nyingi ni kwa sababu wameona ya kuwa Ukristo unaweza kuleta shida na mateso na matata (mst **13**).
c) Njia isiyofaa ni kulipokea kama wale wanaoitwa *kati ya miiba*. Hapa udongo ni mzuri, kwa hiyo mbegu zinaota vizuri, lakini vitu vibaya vinaota vizuri pia. – Watu hawa ni wale wanaotaka kuwa Wakristo, lakini wanataka kuendelea katika mambo ya ulimwengu vile vile. Wanashughulika na utajiri na furaha za ulimwengu. Mambo haya yananyonga uzima wa imani. – Watu hawa wanaonekana mwanzoni wanaupenda ufalme wa Mungu, lakini kama ni lazima kuchagua baadaye, mambo ya ulimwengu yanashinda, kama miiba ishindavyo mimea.

*2) Njia inayofaa.*

a) Ni kulipokea Neno kama Neno la Mungu, kwa maana ndivyo lilivyo kweli kweli (mst **11**).
b) Katika kulisikiliza Neno tuangalie sana mioyo yetu, kwa maana labda ni kama *njia*, yaani Neno haliwezi kuingia, linakaa nje tu.
c) Katika kulisikiliza Neno na kulisoma nyumbani, tuepuke wale ndege wanaotaka kuziondoa mbegu. Ndege ni watu wanaopelekwa na Shetani kusumbua maombi yetu nyumbani. Ndege ni mawazo na mashughuli yale yanayotusumbua hata katika maombi na ibada zetu kanisani.
d) Kama tunaona ya kuwa majaribu yanaanza kutuogofya na kutuzuia katika imani yetu, tumkimbilie Mungu zaidi na zaidi ili kuomba msaada wake.
e) Udongo mzuri, ndio moyo uliotengenezwa na Neno na Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuifanya mioyo yetu iwe mizuri sisi wenyewe. Lakini tunaweza kumwomba Mungu, ya kuwa Roho yake afanye kazi hii katika mioyo, iwe udongo mzuri, Neno lake litakapoweza kuota na kuleta mavuno mazuri. **Isa 55:10–11.**

*Application. "Mwenye masikio, na asikie."* **Mt 11:15; Lk 8:18; 11:28.**

# QUINQUAGESIMA (ESTO MIHI)

**(Lk 18:31–43)**

*Maelezo juu ya somo.*

Somo hili ni mojawapo katika yale yenye sehemu mbili zinazohitilafiana sana, ambayo tumeeleza shida yake katika fungu la pekee (taz mlango IV). Kama tunashindwa kuziunganisha sehemu hizi mbili kwa njia inayofaa katika hubiri letu, basi tunaweza kuhubiri hasa juu ya sehemu ya kwanza, inayoonyesha ya kuwa Yesu anaeleza safari yake ya kwenda Yerusalemu kuteswa na kufa.
Kwa kifupi tunaweza kusema hivi: sehemu ya kwanza na sehemu ya pili zinaunganishwa na lile neno "mateso". Yaani Yesu anaendea mateso yake, na katika safari hii anakuta mtu aliye na mateso makubwa. Au tuseme hivi: Katika shida na taabu zetu tunaweza kupata msaada kutoka Bwana Yesu tu, kwa sababu ametutangulia katika njia ya shida na taabu alipopanda kwenda Yerusalemu.

## TUKIWA PAMOJA NAYE YESU KATIKA NJIA YA MATESO,

*1) tunaona ya kuwa mara nyingi maana ya mateso imefichwa kwetu.*

a) Ndivyo ilivyokuwa kwa wanafunzi walipopata habari za mateso yake Yesu (mst **34**).
b) Sisi tunaona mateso ni mabaya tu, hayana maana kwetu. Labda tunamshtaki Mungu au kunena kama Petro. **Mt 16:22.** Pengine tunashindwa kufahamu maana ya mateso kwa ajili ya kiburi au ukubwa wa mioyo yetu. **Yn 21:18.**
c) Yule kipofu alikuwa ameshindwa kufahamu maana ya upofu wake, lakini ni upofu wake uliomwongoza, hata akamwendea Kristo!
d) Tukishindwa kufahamu, ni kwa sababu hatukufundishwa Neno la Mungu kadiri ya kutosha. **Yn 14:9.**

*2) tunafahamu ya kuwa mateso ni sehemu kuu ya utimilifu wa Maandiko.*

a) Maandiko yanasema waziwazi ya kuwa Masihi atateswa. **Mwa 3:15; Isa 53; Zab 22; Mt 26:53–54; Lk 24:27.**
b) Yesu anapotolewa katika mateso, anajitoa kama kafara kuu ili kuokoa watu wote. **Yn 11:51–52.**
c) Kafara hii ndiyo iliyo kubwa kuliko nyingine zote. **Efe 5:2.** Kafara nyingine hazihitajiwi baadaye. **Ebr 10:12–14.** Kwa hiyo Yesu ameshinda katika mateso yake na kufa kwake maadui wale wakubwa wanaoitwa Shetani, na dhambi, na mauti. **1 Kor 15:54–57.**

*3) Mwishowe tutamsifu Mungu kwa ajili ya mateso yake Yesu, tena kwa ajili ya mateso yetu sisi wenyewe.*

a) Yule kipofu alipata sababu kubwa kumtukuza Mungu. Kwa hakika alimshukuru hata kwa ajili ya upofu wake, kwa maana ndio uliomwongoza na kumfikisha kwake Kristo.
b) Mateso yetu, mara nyingi ndivyo viongozi vinavyotushurutisha kumwendea Kristo. **Mt 9:12.**
c) Kama macho yetu yasipofumbuliwa, tutaendelea kumshtaki Mungu na kupapasapapasa. Macho yetu yakifumbuliwa tutaona ya kuwa matendo yake yote ni neema, **Zab 25:10**, na ya kuwa yeye ndiye anayeweza kutubariki hata katika taabu zetu na kututengenezea kutoka kuzuri, **Zab 121:8**, na kutusaidia tufike kifiko cha milele. **Flp 3:14; 1 Pet 1:9.**

# SIKU YA BWANA YA 6. KABLA YA PASAKA

**(Mt 4:1–11)**

## KUMSHINDA SHETANI KATIKA MAJARIBU

*1) Katika jambo la chakula cha roho.*

a) Mtu anahitaji chakula kwa mwili na roho. Hata Yesu aliona njaa. Lakini njaa ile haikuwa sababu ya kutosha kubadili mawe yawe mikate.
b) Yesu aliona ni jambo kubwa zaidi, roho ipate chakula chake. Chakula hiki ni Neno linalotoka katika kinywa cha Mungu.
c) Yesu alijaribiwa kulitumia Neno la Mungu (yaani nguvu ya Neno hili) ili kuushibisha mwili wake. Lakini alikataa, kwa maana alikuwa na Roho Mtakatifu kwa kadiri ya kuweza kulishinda jaribu hili.
d) Nasi tunaye Roho Mtakatifu tangu ubatizo wetu, kama tumesalia neema ya ubatizo. Katika neema hii ya ubatizo na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na kwa silaha za Neno tunaweza kumshinda Mjaribu.

*2) Katika jambo la kulitumia Neno la Mungu.*

a) Mjaribu alisema: *"Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini."* Alitaka Yesu athibitishe kwa mwujiza ya kuwa ni Mwana wa Mungu. Lakini kama Yesu angaliufanya mwujiza huo, angaliufanya kwa kumtii Shetani! Yesu hakufanya miujiza alipoagizwa na Shetani ama watu waliofuata mapenzi yao tu. **Lk 23:8–9.**
b) Mjaribu alitaja maneno kutoka Maandiko, lakini sehemu sehemu tu. Aliacha mengine yenye maana. Ndivyo Shetani anavyolitumia Neno la Mungu.
c) Mjaribu hasemi kwetu waziwazi ya kuwa Biblia ni mbaya. Lakini anasema: Lifuate neno hili, ama hili. Anaacha mengine yasiyompendeza. Anataka sisi tulifuate Neno la Mungu kwa sehemu zinazotupendeza au kumpendeza yeye.
d) Wanaotaka kumshinda Mjaribu, wawe tayari kuyatumia Maandiko yote, kama Yesu alivyofanya.

*3) Katika jambo la kuchagua mfalme wetu, ambaye atatutawala.*

a) Shetani alishindwa mara mbili. Ndipo alipobadilisha madaraka yake. Alianza kutumia uongo. Yeye mwenyewe ni baba ya uongo. **Yn 8:44.** Anatoa ahadi kumpa Yesu nchi zote za ulimwengu pamoja na utukufu wa ulimwengu. Lakini vitu hivi si mali yake, hana mamlaka kutoa vitu hivi kama zawadi. **Zab 24:1.**
b) Kwa hiyo, kumsujudu ni kusujudu mwizi na mwasi na mwongo. Tena ni kusujudu malaika mbaya, aliyeumbwa na Mungu mwanzoni na baadaye kufanya fitina mbinguni na kutupwa nje. **Ufu 12:9.**

c) Nasi tunajaribiwa kuabudu vitu vilivyoumbwa, kama pesa na mali na umalidadi, ama watu walio viumbe kama sisi. Jaribu lile likifika, ni lazima kufumbua hila ya yule nyoka mzee, kama Yesu alivyoifumbua na kumshinda.
d) Tukimshinda Shetani kwa Neno la Mungu na kwa maombi, atatuacha, lakini *"kwa muda"* tu. **Lk 4:13.** Anayesalia Neno na silaha zote za kiroho, **Efe 6:11–18**, atamshinda Shetani na kuokoka. *"Mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka."* **Mt 24:13.**
e) Msaada wetu mkuu katika majaribu yetu ni kushinda kwake Yesu, kwa maana ndiye aliyejaribiwa kama sisi, bila kufanya dhambi. **Ebr 4:15.**

# SIKU YA BWANA YA 5. KABLA YA PASAKA

**(Mt 15:21–28)**

## JINSI IMANI INAVYOSHINDANA NA KUSHINDA

*1) Kuipigania imani.*

a) Imani haiwezi kuzaliwa au kuumbwa pasipo shida au uchungu. Labda ni shida ya mtu mwenyewe. Pengine ni shida kwa ajili ya mtu mwingine, kama mwanamke huyu alivyoshughulika kwa ajili ya binti yake mgonjwa. Pengine ni shida ya mwili, pengine ni shida ya roho. Mara nyingi shida zetu ni kwa ajili ya dhambi.
b) Imani haiwezi kuzaliwa pasipo maombi ya moyo: "*Unirehemu, Bwana* ..."
c) Pengine inaonekana ya kuwa mtu wa shida anashughulika na kuomba bure. Yesu ananyamaza (mst 23). Kwa hiyo shida inaongezeka tu. Hakuna msaada. Mungu ananyamaza, ni kama hayuko! **Zab 83:1.**
d) Haya yote yanaonyesha zaidi udhaifu wetu. Hapa tunaanza kuona kusudi la Mungu. Yesu aliponyamaza, alimshurutisha mwanamke kuona waziwazi udhaifu wake na kuomba kwa bidii kubwa zaidi. Ndivyo Mungu anavyotufundisha unyenyekevu (mst **26–27**). Kutoka huko chini utaomba kwa bidii na unyenyekevu zaidi. **Zab 130:1–3**. Imani ile tu, iliyojaribiwa na kupimwa mpaka chini katika msingi wake, itaweza kuwa imani imara. **1 Pet 1:7; Yer 11:20.**

*2) Imani ishindayo.*

a) Inawezekana kushinda, kama mtu amenyenyekezwa, na Kristo ametukuzwa. Ni lazima Yesu awe msingi wa imani yetu. **1 Kor 3:10–15.** Hakuna kitu ndani ya mtu mwenyewe kinachofaa kama msingi.
b) Mwanamke huyu hakutegemea haki yo yote ndani yake mwenyewe. Hakudai kitu. Aliomba tu kwa nafsi yake yote, aliomba kwa ajili ya rehema yake Kristo (mst 27).
c) Inawezekana kushinda, kama Mungu anaona ya kuwa mtu amepata mafundisho ya kutosha na kuyakubali mafundisho haya. **Hos 11:8–9.**
d) Imani ishindayo inawezekana kwa wakati unaompendeza Mungu. **Isa 49:8; 2 Kor 6:2; 12:9.** Na katika haya yote, maana si ya kuwa tushinde sisi, bali ya kuwa Kristo aimalize kazi yake ya kushinda katika mioyo yetu. **Flp 1:6; 2:13; Yn 15:5; 1 Pet 5:10.**

*Application.* Kama umeshindwa mpaka sasa katika imani na Ukristo wako, labda ni kwa sababu hujaona bado udhaifu wako na dhambi zako. Labda umepigania ukubwa wako na maendeleo yako. Kwanza Mungu anataka kukunyenyekeza, baadaye ataweza kukukweza kwa wakati wake. **1 Pet 5:6.** Kama maombi yako yameshindwa, labda hujaomba bado kutoka vilindini. **Zab 130.** – Basi, tumia Neno la Mungu, uombe, uingie skuli ya unyenyekevu, nayo imani ya kweli itaumbwa katika moyo wako, nawe utamshukuru Mungu kwa ajili ya ushindi wa Yesu katika moyo wako.

# SIKU YA BWANA YA 4. KABLA YA PASAKA

**(Lk 11:14–28)**

## MASHINDANO YA MABWANA WAKUBWA WAWILI

*1) Huyu "mwenye nguvu" ni nani?*

a) Ni Shetani. Tangu mwanzo wa wakati ametengeneza fitina na uasi kati ya watu na katika mioyo yao. Wengi wametekwa na roho huyu mbaya. Ana silaha nyingi zenye nguvu kuwalinda mateka yake (mst **21**).
b) Wanaokaa katika utumwa wake hawajui maisha mengine. Utumwa wao unaitwa mara nyingi 'uhuru'. **Mwa 3:4–5.**
c) Kama wakati wao umekwisha, bwana wao anawatupa. **Mt 27:4.**

*2) "Mwenye nguvu kuliko yeye" ni nani?*

a) Ni Kristo. Kristo ni utimilifu wa ahadi ya Mungu katika siku ya anguko, **Mwa 3:15**, ya kuwa atamtuma *"uzao wa mwanamke"*. Ahadi hii ilitimizwa, Yesu alipozaliwa, **Gal 4:4**, ili kuwakomboa wafungwa.
b) Yesu alifika kulishambulia boma la Shetani (mst **22**). Lakini silaha zake si silaha za vita ya kawaida. **2 Kor 10:3–4.** Silaha ni za kiroho. Yaani Yesu alifanya vita iliyo kubwa alipoteswa na kufa. **Isa 53; Yn 11:51–52.**
c) Neno lililo kuu katika Ukristo ni ya kuwa Yesu amemshinda Shetani kwa kufa kwake na ufufuko wake. **1 Kor 15:54–57.**

*3) Ingawa Yesu amemshinda Shetani, mapigano yanaendelea hata sasa.*

a) Kweli Yesu amemshinda Shetani, lakini adui huyu anaendelea kutu–sumbua jinsi awezavyo mpaka wakati wake wa mwisho. **Ufu 12:12.**
b) Kwa kuwa Yesu amemshinda 'mwenye nguvu', wokovu unapatikana kwa watu. **Ufu 5.** Lakini kama watapewa wokovu kamili wa mwisho, ni lazima waingie vitani upande wake Yesu, ili kushinda kwake Yesu kumalizike hata katika mioyo yao. **Flp 1:6.**
c) Vita hii baina ya Yesu na Shetani inaendelea kila siku. Hakuna anayeweza kujiweka kandokando na kuyatazama tu mashindano hayo. Asiye upande wake Yesu ni kinyume chake. **Mt 12:30.**

*Application.* a) Ni lazima uone vizuri kama umefungwa katika boma la Shetani au umepewa uhuru katika Kristo. b) Huwezikujiweka huru mwen–yewe, kwani Shetani ni mwenye nguvu. c) Kama umewekwa huru, ni lazima ushirikiane katika vita ile inayoendelea siku zote. d) Katika vita hii umtegemee mshindi mkuu, yaani Yesu Kristo. Unapompigania yeye na kupigania wokovu wako, ufanye vita kwa silaha za kiroho tu, hasa kwa Neno la Mungu, na maombi, ili ukiisha kuyatimiza yote, upate kusimama. **Efe 6:13.**

# SIKU YA BWANA YA 3. KABLA YA PASAKA

**(Yn 6:1–15)**

*Maelezo juu ya somo.*

Somo hili lina kama pande tatu. Linatoa habari za chakula chetu cha kila siku, kwa maana pasipo chakula tutaona njaa, kama watu wale walivyoona njaa huko jangwani. Pili linatoa habari za mwujiza ule wa Yesu alipolisha watu wengi mno kwa mikate mitano na samaki wawili. Tatu linatoa habari za Yesu kama Chakula cha Uzima, kwa maana hapa anatoa habari zake mwenyewe, akionyesha ya kuwa yeye mwenyewe ni nani na ya kuwa yeye tu anaweza kuwapatia watu Uzima wa milele.
Katika kuhubiri kwetu ni vizuri kuangalia pande hizi tatu za somo, tusisahau kuzieleza. Lakini si lazima kuzieleza kwa kipimo kilicho sawa kwa zote. Inawezekana kukaza zaidi upande mmoja (na mwaka mwingine labda kukaza upande mwingine), lakini pande zote tatu zinatakiwa, ili somo lifahamiwe vizuri na wasikilizaji wetu.

## NJAA NA MKATE

*1) Kuna njaa za namna mbalimbali hapa duniani.*

a) Watu wanaweza kuona njaa za namna mbalimbali (chakula, vinyweo, mali, michezo n k), kwa sababu wanataka kuzipendeza tamaa zao.
b) Mungu ametuumba, miili na roho. Kwa hiyo anatuangalia katika mahitaji yetu. **Mt 6:25–34.**
c) Hata Kanisa la Mungu linaangalia mahitaji ya kimwili. **Mdo 6:1–4; Rum 12:5; 12:20; Yak 2:16.**
d) Kuna njaa ya roho pia. Wanaoangalia miili yao kupita kiasi wanasahau mahitaji ya roho. Neno la Mungu linakaza njaa ya roho zetu. **Amo 8:11; Lk 10:41–42; 12:20.**

*2) Kuna mikate ya namna mbalimbali.*

a) Mungu ndiye anayetoa mkate unaoweza kuilisha miili yetu.
b) Yesu ametufundisha kumwomba Mungu kila siku atupatie chakula chetu cha kutosha (riziki yetu). **Mt 6:11.**
c) Yesu aliwahurumia watu katika njaa yao ya kimwili. **Mt 14:16.**
d) Ndipo wengi walianza kumpenda Yesu na kutaka awe mfalme wao (mst **15**). Walitaka chakula cha miili tu, ili kuishi maisha ya uvivu. Hawakuomba kile chakula cha roho kilichotolewa naye Yesu.
e) Lakini mikate ya kawaida haiwezi kuishibisha roho. **Isa 55:2; Mt 4:4; Yn 6:27.**

*3) Yesu ndiye Chakula cha Uzima.*

a) Tusifikiri ya kuwa Yesu alitembea huku na huku, akishibisha watu wote walioona njaa ya mwili.
b) Ingawa anaangalia mahitaji yetu na kuliagiza Kanisa lake kushibisha wenye njaa, **Mt 14:16**, hakufanya mwujiza (ishara, 'miracle') wa mkate mara nyingi. Aliufanya mara mbili tu. **Mt 14:15–21; 15:32–39.**
c) Kusudi lake lilikuwa kuonyesha mamlaka yake, yaani kuonyesha

- ya kuwa yeye ni Masihi,
- ya kuwa yeye ni Mungu,
- ya kuwa yeye anajua kutushibisha kweli kweli,
- ya kuwa yeye ni Chakula cha Uzima wa milele,
- ya kuwa yeye tu anastahili ya kuwa tumwamini katika mambo yote.

d) Tena mafundisho yote juu ya Mkate na Chakula (**Yn 6**) ni mafundisho juu ya Chakula cha Bwana na ondoleo la dhambi. **Yn 6:33–35; 6:47–58.**
*Application:* a) Kwa kweli unajua mahitaji ya mwili wako. b) Unajua vile vile mahitaji ya roho yako? c) Hapa Yesu anaonyesha ya kuwa ndiye anayeweza kutushibisha kweli kweli. d) Kazi ya mkate (chakula) ni kukupatia uzima wa kimwili. e) Kazi yake Yesu ni kukupatia Uzima wa milele. Kwa hiyo anajiita Chakula cha Uzima wa milele. Pasipo kumjua Yesu, huwezi kuupata Uzima, bali utakuwa mtoto wa kifo na upotevu. f) Ilikuwa mwujiza mkubwa kulisha watu wapata 5000. Lakini ni mwujiza mkubwa zaidi kukuokoa wewe mwenye dhambi, yaani kuishibisha roho yako milele. Yesu anapenda sana kuufanya mwujiza ule katika moyo wako.

# SIKU YA BWANA YA 2. KABLA YA PASAKA

**(Yn 8:46–59)**

**NENO LA KWELI**

*1) Neno la Kweli ni Neno lake Kristo.*

a) Mlango huu ni mlango wa mashindano kwa njia ya maneno kati ya Wayahudi na Yesu, hata wakataka kumwua (mst **59**). Kwa nini walifanya hivi? Kwa sababu alijidai ya kuwa amefika kutoka kwa Mungu.
b) Yesu alimtangulia Ibrahimu (mst **56–58**). Alishirikiana naye Baba katika kuuumba ulimwengu. **Yn 1:3; Kol 1:16; Ebr 1:2.**
c) Kwa ajili ya Umungu wake Yesu hana dhambi (mst **46**). **1 Pet 2:22.**
d) Kwa ajili ya haya yote anaweza kusema habari za kweli juu yake Baba, **Yn 15:15**, na kutoa maneno yaliyo ya kweli tu (mst **46–47**). **Yn 17:17; 14:6; 18:37.**
e) Kwa ajili ya haya yote haiwezekani kumtenga Yesu na Neno la Mungu. Yesu ni katika Neno, na Neno la kweli limo katika yeye, au yeye ni Neno. **Yn 1:1; 1 Yoh 1:1.**

*2) Neno la Kweli linaunganisha na kutenga watu.*

a) Haya ndiyo mafundisho yake Yesu mwenyewe (mst **47**): wanaosikia nao wasiosikia.
b) Je, watu wote hawakuumbwa naye Mungu? Kweli wameumbwa naye, lakini kwa njia ya dhambi tengano kubwa limeingia kati yao.
c) Mipaka ya kuwatenga watu inaonekana kwa vile wanavyolitenda Neno la Mungu, na vile wanavyompokea Kristo.
d) Wayahudi walitaka kuyashika Maandiko na kumkataa Yesu. Watu wengi wa siku hizi wanamtaka Yesu, bali wanalikataa Neno. Haiwezekani hata kidogo. Yesu na Neno ni mamoja. **Yn 8:51; 14:10; 14:23; 17:14.**
e) Kumchagua Yesu ni kulikubali Neno la Mungu. Kulipinga Neno ni kumtukana Yesu (mst **47** na **49**).

*3) Neno la Kweli linaokoa.*

a) Wokovu unapatikana kwa vile watu wanavyolipokea Neno la wokovu. **Rum 10:14–17.**
b) Anayeeleza na kulikaza Neno ndiye Roho Mtakatifu. **Yn 14:26.**
c) Kazi ya Neno na ya Roho Mtakatifu inasaidia hata kufani (mst **51**).
d) Kulishika Neno, maana yake si ya kuwa tungeweza kuzitimiza amri zote, bali ni kukaa na kuvumilia katika ulinzi na uongozi na baraka za Neno pasipo kutoka. Tena ni kuzitegemea ahadi zote za Neno. Sisi tukilishika Neno kwa njia hii, Neno litatushika sisi. **Yn 10:28.**
e) Neno hili linatoa ahadi kwa Kanisa la Yesu Kristo. Likidumu katika Neno la kweli, *"wala milango ya kuzimu haitalishinda."* **Mt 16:18.**

# SIKU YA BWANA YA MWISHO KABLA YA PASAKA (SIKU YA MITENDE)

**(Yn 12:1–16)**

## JINSI WANAFUNZI WANAVYOWEZA KUMSHUHUDIA BWANA WAO

*1) Walio wengi wanapata nafasi kumshuhudia kwa njia ambazo hazionekani sana.*

a) Ni hatari kujaribu kuonekana wenyewe. Jambo lililo kuu si kuonekana, wala kuleta sadaka zinazoonekana sana. **Mt 6:1–4.**
b) Mmoja tu katika somo letu alitoa sadaka kubwa. Wengine walitoa sadaka zao siku kwa siku. Naye Martha alileta sadaka yake kwa huduma ya kila siku. **Lk 10:40.**
c) Ingawa Mariamu alitoa sadaka kubwa mno siku hiyo, alizoea kumshuhudia Bwana Yesu kwa njia isiyoonekana sana: *"Aliketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake."* **Lk 10.39.**
d) Ushuhuda wa mwanafunzi unaofaa hasa ndio huu: kumsikiliza Yesu katika Neno, na maombi na ibada, na Chakula cha Bwana. Kuyadharau mambo yale na kujaribu kutoa sadaka kubwa mno, ama kumshuhudia kwa mahubiri au maneno matamu mbele ya watu, ndio unafiki tu. **Mt 15:8.**
e) Hata katika mambo na njia za kumshuhudia Bwana Yesu ni vizuri kuanzia mambo madogo ambayo ni ya watu wote na kila siku. Ni kuituliza *"nafsi yangu, na kuinyamazisha"*, si *"kujishughulisha na mambo makuu."* **Zab 131:1–2.**

*2) Wanapata nafasi kumtolea sadaka.*

a) Sadaka inayofaa haifanywi kwa njia ya kushurutishwa, *"maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu"*. **2 Kor 9:7.**
b) Sadaka inayofaa haifanywi kwa sababu mtu anadharau nafasi za kila siku na kwa hiyo kutaka kutoa sadaka kubwa.
c) Anayetoa sadaka kubwa sana safari moja, ndiye aliyezoea kutoa sadaka za kawaida za kila siku.
d) Kwa akili za kibinadamu ni vibaya kumtolea Kristo ama Kanisa lake sadaka kubwa: *"Mbona marhamu hii haikuuzwa kwa dinari mia tatu, wakapewa maskini?"* (mst 5) Hawa wanasema wanawafikiria maskini, lakini hasa wanajifikiria. Wanaosaidia maskini ndio wanaompenda Yesu na kumshuhudia kwa kazi zao na sadaka zao za upendo.
e) Sadaka zilizo kuu, tena za kweli zinatoka katika mioyo inayomshukuru Bwana Yesu kwa ajili ya upendo wake. **1 Yoh 4:19.** Kwa hiyo ni lazima upendo wa Bwana Yesu uwe kisima cha kweli cha upendo wetu.

*3) Pengine ushuhuda wa Mkristo utaonekana katika sadaka iliyo kubwa mno.*

a) Kwa kweli Mariamu huyu hakuweza kutoa sadaka ya thamani kubwa kama hii mara nyingi. Labda alikuwa ameweka akiba marhamu hii ya nardo tangu siku nyingi. Labda alisitasita mara nyingi kama aliweza kutoa ama siyo. Siku hii aliitoa tu, pasipo kusitasita, tena kwa furaha. Alishurutishwa moyoni mwake na furaha yake na shukrani yake.
b) Ndivyo ilivyo katika mioyo ya Wakristo wa kweli. Kwa ajili ya kumpenda Kristo wako tayari kumshukuru na kumtukuza kwa sadaka kubwa mno.
c) Walimwengu wanaona ni hasara tu, ama ujinga. Kwa maana wana mawazo mengine juu ya mambo hayo (mst **4–6**).

*Application.* Nawe unaweza kuupima upendo wako kama ni wa kweli. Yule mtu aliye tayari kutoa sadaka kubwa, hata yote yaliyomo katika mikono yake, **Mk 10:21**, huyu anampenda Yesu. Lakini ni lazima sadaka hii itolewe kwa furaha ya moyo, si kwa kushurutishwa. Umwombe Bwana Yesu aumbe upendo wa namna hii katika moyo wako. Anaweza, kwa ajili ya upendo wake, kwa maana yeye alitoa sadaka iliyo kuu kwa ajili yako.

# IJUMAA KUU, YAANI SIKU YA KUKUMBUKA KUFA KWAKE YESU KRISTO

**(Lk 23:33–48)**

Huko Golgotha ilikuwako misalaba mitatu. Kila msalaba una maana yake ya pekee. Kwa hiyo yote mitatu inaweza kutufundisha juu ya mambo makuu ya siku hiyo.

## MISALABA MITATU

*1) Msalaba wake Yesu unaonyesha ya kuwa Mungu anaihukumu dhambi, bali anataka kumsamehe mwenye dhambi.*

a) Anwani ile (mst 38) inaonyesha ya kwamba alikuwa Mfalme wa Kweli na ya kuwa alihukumu dhambi zote, hata zile za watu waliojisifu wenyewe. Kwa hiyo walimchukia, ikampasa kuteswa na kufa.
b) *"Aliokoa wengine"* (mst 35). Hakuweza kurudi nyuma. Kwa hiyo ali–endelea mbele, hata kufani, akiombea watesaji wake.
c) Kwa hiyo msalaba wa Yesu unafumbua haya katika nyakati zote: Hu–kumu ya Mungu juu ya dhambi zote, tena nia na uwezo wake wa kumtolea msamaha mwenye dhambi.

*2) Msalaba wa mnyang'anyi (mhalifu) mmoja unaonyesha ya kuwa tunaweza kuupoteza wokovu wetu kwa kutokutubu tu.*

a) Hatuna habari za mtu huyu, kama jina lake nani, ama alitoka wapi, ama amefanya nini. Lakini msalaba wake uliwekwa kando ya msalaba wake Yesu. Kwa hiyo amepata jina lake litakalodumu sikuzote: *"Mhalifu asi–yetubu"*.
b) Jina hilo linasema amekuwa mtu wa namna gani: katika njia panda za maisha yake amechagua vibaya, na katika njia panda ya mwisho akachagua vibaya tena, akamfukuza Yesu kama Mwokozi.
c) Ndivyo ilivyo kwetu. Tukiupita msalaba wake Yesu kwa kutojali ('indifference') tunajipatia hukumu na alama hii: mtu asiyetaka kupokea msamaha.

*3) Msalaba wa mnyang'anyi (mhalifu) mwingine unaonyesha ya kuwa atubuye anaweza kusamehewa na kusimamishwa tena.*

a) Hatuna habari za mtu huyu, kama jina lake nani, ama alitoka wapi, ama amefanya nini. Lakini msalaba wake uliwekwa kando ya msalaba wake Yesu. Kwa hiyo amepata jina lake litakalodumu sikuzote: *"Mhalifu aliyetubu"*.
b) Jina hilo linaonyesha imetokea nini katika maisha yake. Katika njia panda za maisha yake labda alifuata watu wabaya, akawa mtu mbaya, yaani mhalifu. Lakini katika njia panda ya mwisho alipata neema kuchagua vizuri, yaani akamchagua Bwana Yesu, akampokea kama Mwokozi.
c) Ndivyo ilivyo hata kwetu. Tukisimama kwenye msalaba wake Yesu, na kuupokea msamaha na ondoleo la dhambi kwa ajili ya toleo lile kuu la Yesu, basi tutasamehewa na kusimamishwa, hata milele.

*Application. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao."* **2 Kor 5:19.** Hayo yalifanywa kwa ajili yako.

# PASAKA, YAANI SIKUKUU YA KUKUMBUKA UFUFUKO WA YESU KRISTO

**(Mk 16:1–7)**

## JINSI BWANA YESU ALIVYOISHINDA MAUTI

*1) Rafiki zake hawakungoja ya kuwa ataishinda mauti kwa njia hii.*

a) Biblia inatoa habari za kweli juu ya watu, hata maarifa haya ya kuwa wanafunzi na rafiki zake Yesu hawakungoja ya kuwa atafufuka. Wanawake hawa walikwenda *"kumpaka"*, maana yake: kuutengeneza mwili wake usiharibike upesi kaburini (mst **1**). Walifikiri alibaki humo (mst **3**).
b) Ingawa walikwenda kumwangalia mwili wake, walimheshimu kama mtu aliyekuwa amefariki.
c) Ndivyo watu wengi wanavyomheshimu Bwana Yesu: kama mtu mwema sana aliyeishi zamani sana, lakini sasa hayupo, kwa maana amekufa na kuwekwa kaburini.

*2) Mambo yote yalibadilika kabisa katika hali ya watu, Yesu alipofufuka.*

a) Yesu alishinda mawazo yote ya watu alipofufuka: *"Waliona ya kuwa lile jiwe limekwisha kuvingirishwa"* (mst **4**).
b) Malaika kutoka mbinguni aliwaambia ya kuwa Yesu alikuwa amefufuka.
c) Tangu wakati wa Adamu mauti ilikuwa imetawala kati ya watu. **Mwa 3:19.** Sasa Adamu wa pili ameishinda mauti. **1 Kor 15:20–23.**
d) Tendo hili la kumfufua Yesu ni kubwa mno, hata lifanane na lile la kuumba ulimwengu. Kwa hiyo mambo yote yamebadilika kabisa, au yaweza kubadilishwa. **2 Kor 5:17.**

*3) Ufufuko wa Yesu ni msingi wa tumaini letu la milele.*

a) Kweli watu wote watakufa kimwili, lakini ni kama kulala usingizi tu, **Yn 11:11**, kwa maana watafufuliwa katika kurudi kwake Kristo.
b) Ufufuko wa Yesu ni hakika yetu ya kuwa anaweza kutufufua nasi, na kweli atafanya hivyo.
c) Baada ya kufufuka kwake Yesu alipaa mbinguni, na kutoka huko analiongoza Kanisa lake na rafiki zake. Tena anawaombea. **Ebr 1:3; 7:25; 1 Yoh 2:1.**
d) Mkristo anaweza kungoja siku yake ya kufa kwa furaha, tena anaweza kuzika wapendwa wake kwa tumaini kubwa, ikiwa wanamwamini Yesu Kristo, kwa maana tumaini letu ni imara kwa ajili ya ufufuko wake Yesu. **Tit 1:2; 2:13.**

# SIKU YA 2. YA UFUFUKO WA YESU KRISTO (EASTER MONDAY)

**(Lk 24:13–35)**

## KRISTO KAMA ASIYEJULIKANA NA KAMA MWOKOZI ANAYEJULIKANA

*1) Kristo anatembea pamoja nasi, ingawa labda sisi hatumjui.*

a) Inaonekana ya kuwa wanafunzi hawa walikuwa wa namna ya kumjua Yesu kwa uso wake na mafundisho yake (mst **16,18,21**). Kwa hiyo iliwapasa kumjua kwa kweli.
b) Lakini hawakumjua kweli kweli. Walimfahamu kwa njia ya maarifa tu, si kwa njia ya moyo, wala imani.
c) Ingawa ilikuwa hivyo, Yesu alitembea pamoja nao. Aliyafungua maan–diko, akawasha mioyo yao, akawaonya kwa ajili ya kutokuamini kwao.
d) Ndivyo ilivyo hata kwetu. Wengi ni kama wanafunzi wa Emau, yaani wanafundishwa na kuhubiriwa na kushirikiana na wanafunzi wengine Kanisani, pasipo kumjua Bwana Yesu kwa imani ya kweli. Ingawa anatembea pamoja nao hawamtambui. Kazi yake na mbaraka zake ni kama matendo ya Kigeni kwao (mst **18**).
e) Ni neema kubwa sana ya kuwa Yesu haachi wanafunzi namna hii. Ana–wavumilia na kuwaonya na kuendelea kuwafundisha hata waamke, ikiwezekana (mst **25–27**).

*2) Kristo anataka kuwa Mwokozi anayejulikana kwetu.*

a) Huko Emau alipata kuwa Mwokozi aliyejulikana. Ilitokea hivyo ali–poyaeleza Maandiko (mst **27**), na wanafunzi walipomwomba kuendelea kukaa nao (mst **29**) na Yesu kuwamegea mkate (mst **30**). Ndipo walipomtambua (mst **31**).
b) Ndivyo ilivyo hata kwetu. Pengine tunaweza kukaa katika ushirika wa Kanisa pasipo kumjua Yesu kama Mwokozi wetu. Lakini kama

*tunatumia Maandiko* na kumtafuta Yesu humo, na
*kuendelea katika maombi* yetu pasipo kuchoka *("kaa pamoja nasi"),*
na *kukitumia Chakula chake Kitakatifu,*

ndipo atakapojifunua kwetu, tutambue ya kuwa ni Mwokozi wetu aliye hai.

*Application.* Labda somo hili limefunua hali ya moyo wako na imani yako. Kama ni hivyo limefunua vile vile ya kuwa Yesu anataka kuwa Mwokozi wako anayejulikana. Sasa ni kazi yako kuchagua kama unataka kumjua kweli kweli kama Mwokozi wako. Angalia asikuambie wewe: *"Wewe usi–yefahamu, mwenye moyo mzito wa kuamini yote waliyoyasema manabii!"*

# SIKU YA BWANA YA 1. BAADA YA PASAKA (QUASIMODOGENITI)

**(Yn 20:19–31)**

## JINSI BWANA YESU ANAVYOJIFUNUA

*1) Bwana Yesu alijifunua kwa wanafunzi wake, hata wakauona mwili wake uliotukuzwa.*

a) Alikuwa yeye yule aliyekufa msalabani, kwa maana aliwaonyesha mikono yake na ubavu wake (mst **20**).
b) Lakini ingawa alikuwa yeye yule alikuwa mwenye tofauti, hata akaweza kupitia milango iliyokuwa imefungwa (mst **19**). Linganisha na hayo: **Yn 20:17** (*"usinishike"*) na **1 Kor 15:40**.
c) *"Wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana"* katika mwili wake wa utukufu (mst **20**).

*2) Bwana Yesu anajifunua kwetu katika Kanisa lake.*

a) Amekwisha toa Roho yake katika Kanisa lake (mst **22**). **Mdo 2; Yn 16:7,13–15.**
b) Katika Roho huyu Kanisa linaendelea kukaribisha watu wote (**Mt 28:18–20**) na kuwalisha kwa Chakula kilichoshuka mbinguni. **Yn 6:33,52–58.**
c) Kwa hiyo Kanisa linaendelea kuutoa ushuhuda ule wa Yesu (mst **21**). Kwa hiyo ungamo hili linaendelea katika Kanisa lake: *"Bwana wangu na Mungu wangu"* (mst **28**).

*3) Bwana Yesu anajifunua kwa kila mwenye dhambi atubuye.*

a) Katika Kanisa lake anatoa ondoleo la dhambi. **Lk 24:47; Mdo 2:38; Kol 1:14.**
b) Ondoleo hili linapatikana kwa kila mtu aaminiye (mst **29**).
c) Ondoleo la dhambi linaleta amani ile ambayo ni kipaji chake Yesu. **Yn 20:19; 14:27; Efe 2:14; Flp 4:7; 2 The 3:16.**

# SIKU YA BWANA YA 2. BAADA YA PASAKA (MISERICORDIAS DOMINI)

### (Yn 10:11–16)

### MCHUNGAJI MWEMA

*1) Mchungaji mwema ni nani?*
a) Ni Yesu Kristo tu, yeye peke yake. Hasemi ya kuwa ni mmojawapo katika wachungaji wema. Anarudia habari za **Zaburi 23** na utabiri mwingi wa manabii juu ya mchungaji mwema, kama **Eze 34:11–16**. Sasa anasema: Mimi ndimi niliye (mst **11,14**).
b) Tena anatuonyesha kazi zake za uchungaji: anawaangalia kondoo zake (mst **12,14**).
c) Anaonyesha hata kazi yake iliyo kuu kwa ajili ya kondoo zake, yaani kuwafia (mst **11,15**).
d) Hapa ingeonekana ya kuwa ameshindwa, kwa maana maadui walimwua. Lakini Yesu anapotoa habari za kufa kwake anakueleza *kushinda kwake*. Yaani kufa kwake kulikuwa kumefikiriwa tangu mwanzo ili kumshinda Nyoka ama Mbwa–mwitu. **Mwa 3:15; Isa 53:4–12.** Mchungaji huyu amelinunua kundi lake kwa damu yake. **Ebr 13:20; Ufu 1:5; 5:9.**

*2) Mchungaji mwema anatusaidia kwa njia gani?*
a) Anatupatia salama. Anawajua kondoo (mst **14**). Anawalinda na kuwa–okoa. **Lk 15:4–7.**
b) Anampiga adui. Anaishika fimbo yake na gongo lake. Anampiga adui kwa fimbo yake.
c) Kondoo wanamkusanyikia mchungaji wao, watoke zizi lao, warudi tena chini ya ulinzi wake (mst **9**).
d) Pasipo mchungaji kondoo wanatapanywa (mst **5,10,12; Mt 9:36**). Chini ya ulinzi wa Yesu watu wanakusanywa kutoka makabila yote, wawe kundi moja (mst **16**). **Yn 17:20–21; Ebr 13:20.**

*3) Mchungaji huyu anataka nini kutoka kwetu?*
a) Anataka utii wetu. Kama kondoo wanakimbia, kila mmoja upande wake, itakuwaje? Kondoo zake Yesu wanaisikiliza sauti yake (mst **3**).
b) Wakristo walio kondoo katika kundi lake Yesu wanaisikiliza sauti yake katika Neno, nyumbani na kanisani. Mchungaji mkuu ana wachungaji wasaidizi walio na wajibu huu wa kulilisha kundi. **1 Pet 5:4; Yn 21:15–17.**
c) Wakristo (kondoo wa kundi) na wasaidizi ni lazima wamtii Mchungaji mkuu. Kwa hiyo ni lazima waijue sauti yake anaponena (mst **4,14**). *"Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu."* **Yn 18:37.**
d) Utii huo, maana yake ni ya kuwa tuache mapenzi yetu ya pekee, tujiweke chini ya mapenzi yake Mungu. **Yn 21:18; Mt 26:39; Yn 6:38; Ebr 5:5–10.** Pengine inatakiwa tutoe matoleo makuu kwa ajili yake Yesu Kristo, lakini toleo lililo kuu limetolewa naye mwenyewe, alipojitoa kwa ajili yetu. **Yn 10:18; Gal 2:20; Tit 2:14.**

# SIKU YA BWANA YA 3. BAADA YA PASAKA (JUBILATE)

**(Yn 16:16–22)**

Huzuni na furaha zabadilika ulimwenguni, tena katika maisha ya kila mtu pia. Kujumlisha twaweza kusema ya kuwa furaha ya ulimwengu huu itakoma kwa huzuni, bali furaha iliyo na kisima chake katika Mungu na ufalme wake, kweli inaanzia huzuni, lakini itatimilizwa, hata isiwe na mwisho, katika furaha ya milele.

## HUZUNI NA FURAHA

*1) Katika maisha na imani ya Kikristo ni lazima kupitia huzuni fulani.*

a) Wanafunzi hawakumfahamu Yesu aliponena juu ya shida na huzuni.
b) Walikuwa hawajaona bado huzuni juu ya kuondoka kwake, kwa hiyo hawakuijia furaha juu ya kurudi kwake.
c) Ndivyo ilivyo katika maisha ya kila Mkristo: asiyeijua huzuni ya kweli, hawezi kuijua furaha ya kweli. **Mdo 14:22; 2 Kor 7:10.**
d) Pengine mtu mmoja anaweza kuona huzuni fulani, na mwingine kidogo tu, mmoja anaweza kuona furaha nyingine, na mwingine kidogo tu, kwa maana tumehitilafiana, na maisha yetu yamehitilafiana.
e) Lakini huzuni moja imetupasa kuona sote: huzuni juu ya dhambi zetu. Na furaha moja imetupasa kuona sote: furaha juu ya ondoleo la dhambi zetu, linalotolewa naye Mwokozi wetu.

*2) Furaha ile iliyopitia huzuni ya kweli, ndiyo itakayodumu milele.*

a) Si huzuni zo zote zilizo na tumaini zuri namna hii. Kwa maana tunaweza kuhuzunika katika dhambi zetu pasipo kutubu. Huzuni ile haina ahadi. **Mk 10:22; Yn 13:30; 1 Pet 2:20.**
b) Kama mtu anamwendea Yesu, mara nyingi Yesu anamhuzunisha kwanza. Kweli hakuna imani isiyotanguliwa na huzuni. **Mt 15:26; Yn 11:6** (Yesu alijicheleweshа, hata akafa Lazaro); **1 Pet 5:6.**
c) Kama Yesu anahuzunisha mwenye dhambi, kweli anamwinua baadaye. **Mt 5:4; 23:12.** Kwa hiyo Yesu anaweza kuwapatia wanafunzi wake ahadi ya furaha (mst 22).
d) Furaha hiyo ni ya namna nyingine kuliko ile ya ulimwengu, kwa maana inapatikana hata katika dhiki na taabu na mateso. **Rum 5:3; 8:18; Kol 1:24; Ebr 10:32–36; 1 Pet 4:13.**
e) Furaha ile iliyopata msingi wake katika kazi ya Kristo haina mwisho, bali itadumu milele (mst 22). **Isa 35:10; 1 Pet 1:8; Mt 5:12.**
f) Kwa wale wanaofika kwenye utukufu wa mbinguni ni hasara gani, kama wameona huzuni na mateso siku chache duniani? Hakuna, kwa maana huzuni ile ndogo iliwaongoza kwake aliyeshinda huzuni zote na badala yake kuleta furaha inayodumu milele. **1 Kor 15:26; Ufu 21:4.**

# SIKU YA BWANA YA 4. BAADA YA PASAKA (CANTATE)

### (Yn 16:4b–15)

### YESU KRISTO NA ROHO MTAKATIFU WAKE

*1) Roho Mtakatifu anaiendeleza kazi yake Yesu Kristo.*

a) Wanafunzi wa kwanza hawakufahamu jinsi Bwana Yesu na Roho Mtakatifu walivyohusiana, kwa hiyo walihuzunika sana (mst **6**).
b) Yesu anawafundisha juu ya kutoka kwake (mst **5–7**): *"Yawafaa ninyi mimi niondoke."* Kweli itakuwa lazima kuipitia huzuni (juu ya kufa na kuondoka kwake Yesu) ili kuifikia furaha (juu ya kufufuka kwake na kupaa kwake mbinguni na kutolewa kwa Roho Mtakatifu).
c) Kama Yesu ameimaliza kazi yake ya kutengenezea watu haki, anaweza kutoka hapa; itakuwa kazi ya Roho kuiendeleza kazi yake katika watu (mst **7–11**).
d) Mipango hii (juu ya kazi yake Kristo na kazi yake Roho Mtakatifu) ilifanywa mwanzoni kabla ya ulimwengu kuwapo. **Efe 1:7–10.** Kwa hiyo hakuna sababu ya kuona huzuni juu ya kuondoka kwake Yesu. Ataiendeleza kazi yake kwa kumtuma Roho Mtakatifu.

*2) Roho ni Kiongozi katika njia ya kweli.*

a) *"Atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu."* Ni habari za kweli juu ya dhambi zetu, na juu ya haki ya Mungu, na juu ya hukumu kali ambayo Mungu Mtakatifu ataitoa juu ya dhambi zote za watu.
b) Kuna dhambi mbalimbali, lakini dhambi iliyo kuu, ndiko kutokuamini kwetu (mst **9**). Dhambi nyingine ni sehemu ama mifano ya dhambi kuu.
c) Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuionyesha dhambi yetu na kutusaidia tuione nasi. Anaifanya kazi hii anapotuongoza katika ibada, na maombi yetu na kutusaidia kusoma vizuri Neno la Mungu.
d) Anauonyesha ulimwengu (yaani watu wanaokaa ulimwenguni) haki ya Kweli. Si ya watu, bali ni ile ya Yesu Kristo tu. Kweli Yesu ameitimiza Sheria ya Mungu na masharti yote. **Mt 5:17; Rum 10:4.** Kwa hiyo Roho Mtakatifu ni Kiongozi wa kutuleta kwake Kristo. **Gal 3:24.**
e) Ili kuifanya kazi hiyo Roho atafanya kazi ya hukumu, kwanza katika mioyo yetu, ili tutubu na kumgeukia Mungu, pili kutukumbusha juu ya hukumu ya mwisho, itakayotokea kwao wasiomwamini Yesu (mst **9,11**). Anayeamini kweli anakaa salama, asiiogope hukumu, kwa sababu hukumu imempitia hata hapa. **Yn 5:24.**

*3) Kazi ya Roho inamtukuza Yesu Kristo.*

a) Maana yake si ya kuwa Yesu Kristo ana kazi moja, Roho ana kazi nyingine. La! Kazi zote za kugeuza watu na kuwasaidia watu katika njia ya imani, ni kazi ya Mungu aliye mmoja tu. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuiendeleza kazi aliyoifanya Yesu hapa duniani, kwa hiyo anatukuzwa katika kazi ya Roho.
b) Kwa hiyo Roho anatufundisha hasa juu yake Kristo na haki yake na wokovu unaopatikana katika yeye.
c) Kwa hiyo anatufundisha katika Maandiko Matakatifu, *"kwenye kweli yote"* (mst **13**).
d) Usitegemee "watu wenye busara" ama "sauti fulani" ndani yako, isipokuwa inapatana kabisa na Neno. Kwa maana Roho Mtakatifu *"atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari"* (mst **14**).
e) Yote ni kwa sifa ya Yesu Kristo na Mungu aliye mmoja tu. **Zab 66:2; Rum 11:33–36; Ufu 4:11.**

# SIKU YA BWANA YA 5. BAADA YA PASAKA (ROGATE)

**(Yn 16:23b–30)**

**OMBENI, NANYI MTAPATA**

*1) Ombeni! Ndiyo mapenzi ya Baba.*

a) Mawazo ya watu juu ya maombi ni ya kuwa kwa maombi yetu tutamshawishi au kumshurutisha Mungu kufuata mapenzi yetu.
b) Lakini Mungu ni Muumba wetu na Baba yetu. Anataka kututunza na kutupatia mahitaji yetu. **Mt 6:32; Zab 55:22.**
c) Yesu anaonyesha ya kuwa hata watu wabaya watatusaidia, kama tuki–omba kwa bidii. Mungu je? **Mt 7:7–12.**
d) Kama Mungu ni mwema na mwenye upendo kuliko wazazi wote, anataka tumwombe na kumwambia mahitaji yetu, tukiomba sana (mst **23**).

*2) Ombeni kama Yesu alivyoomba.*

a) Ametuonyesha mfano mzuri katika kuomba kwake. Ingawa alikaa karibu na Baba wa mbinguni katika moyo wake kila siku, aliomba kwa taratibu kila siku. **Mk 1:35; 6:46; Lk 11:1.**
b) Shida na mahangaiko yalipomtukia, ndipo alipoomba zaidi. **Mt 26:36–46.** Ndipo watu wengi wanaposahau au kuacha kuomba. **Yak 4:3; 5:13.**
c) Mfano wa Yesu unatuonyesha ya kuwa tunaweza kuomba kwa maneno yetu ama kwa maneno yaliyotungwa na wengine. Yesu aliomba mara nyingi kwa maneno ya Zaburi. Tena ametupatia sala yake *"Baba yetu uliye mbinguni ..."*

*3) Ombeni kwa jina lake Yesu.*

a) Jina la Yesu ni lenye nguvu. Jina hilo lina nguvu hata juu ya pepo wabaya. **Mk 16:17.**
b) Anayeomba katika jina lake Yesu anaomba kama vile Yesu alivyoomba. **Mt 26:39; Yn 16:23,26.**
c) Anayeomba katika jina lake Yesu anaona upesi ya kuwa maneno men–gine na mapenzi mengine hayafai. Hawezi kuomba ya kuwa Yesu atamsaidia katika matendo mabaya au tamaa mbaya. Basi, *"kuomba katika jina lake Yesu"* ni msaada mkubwa kufuta yaliyo mabaya na kuingiza yanayofaa katika maombi yetu.

*4) Ombeni! Ndilo agizo lenye ahadi kubwa.*

a) Yesu alisema: *"Ombeni, nanyi mtapata"*.
b) Hapa tunaweza kukosa katika ufahamu wetu, tukifikiri ya kuwa tutapewa kila mara kwa njia iliyo sawa na mapenzi yetu. Si hivyo. Watoto wanaomba vitu vingi visivyofaa wakati ule au hata kidogo. Wazazi wanatoa vitu vile wakati mwingine unaofaa, au wanatoa vitu vingine kabisa vinavyowafaa watoto.
c) Ndivyo Bwana Mungu anavyofanya. Anajua yote kuliko sisi, anajua ni mambo gani yanayotufaa zaidi. Kwa hiyo tuweke mashaka na mapenzi yote mbele yake anayejua. **Rum 8:26–27.**
d) Tukiomba kwa bidii tunapewa jambo fulani lililo kubwa kuliko vipaji vyote. Ndiyo amani ya moyo, na amani ya kweli. Ndiyo furaha timilifu (mst **24**). Inaweza kupatikana hata katika taabu na shida kubwa (mst **24**). Ndilo kusudi lake Yesu kutupatia amani hii: *"Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu."* **Yn 16:33.**

# SIKU YA KUPAA KWAKE YESU KRISTO

**(Mdo 1:1–11)**

## NJIA KUTOKA DUNIANI KUFIKA MBINGUNI

*1) Yesu ndiye aliyeitengeneza njia hii.*

a) Amefika mwenyewe kutoka mbinguni ili kutengenezea watu wapotevu wokovu. Ilikuwa kazi kubwa, kwani ilimpasa kujitoa mwenyewe hata kifo-ni.
b) Wakati alipokuwa amefufuka tena kutoka kwa wafu, zilibaki kazi mbili: kurudi mbinguni na kumtuma Roho yake Mtakatifu (mst **4–5**).
c) Kama yeye amerudi mbinguni na kumtuma Roho, basi kazi ya wokovu itakuwa tayari. Wanafunzi wake wataweza kuutangaza wokovu na ufalme wa Mungu pote duniani (mst **8**).

*2) Sasa njia hii inaonekana na kupatikana katika Kanisa lake Yesu Kristo.*

a) Upande mmoja kazi ya Yesu ni tayari kabisa, kwa maana ametufia na kufufuka tena kwa ajili yetu na baadaye kupaa mbinguni. Basi, upande *wake* kazi ni tayari.
b) Lakini upande wa watu kazi ya wokovu bado tayari. Ni lazima ushuhuda ule (mst **8**) usikiwe duniani katika watu wa kila kabila. **Mk 16:15.**
c) Si kazi yetu kujua ama kukaza, ya kuwa kazi itakwisha lini (mst **6–7**), ila kueneza habari njema tu. **Yn 21:21–23.**
d) Yote yanayotakiwa kwa kazi hiyo yamewekwa tayari katika Kanisa la Yesu: Neno, Roho, sakramenti, maombi, ushirika wa Kikristo n k. **Yn 8:31; Mt 28:18–20; Lk 22:19; Yn 16:13, 23; Mdo 2:46.**
e) Neno la Mungu linakaza ya kuwa Ukristo ndio mwendo wa kwenda mbinguni. **2 Kor 5:1; Flp 3:20; Ebr 13:14.** Kwa hiyo ina maana sana ya kuwa Yesu ametutengenezea njia inayofaa alipotangulia kwenda kwa njia ile.

*3) Yesu ataitumia tena njia ile atakaporudi duniani.*

a) Wanafunzi walisimama wakitazama juu, kwa sababu hawakufahamu sana kuondoka kwake (mst **11**).
b) Lakini sababu yao ya kuhuzunika ilikuwa sababu kubwa zaidi kufurahi, kwa maana atapewa utukufu mbinguni kwa ajili ya kushinda kwake, tena ataweza kuwaombea mbinguni na kurudi kwa njia ile aliyoitengeneza (mst **11**).
c) Kanisa la Kristo linazidi kumngoja hivi, likitazama mbinguni. Likifanya hivi litajua kutofautisha vizuri baina ya mambo ya dunia na mambo ya mbinguni. Ni hatari sana kugandamia vitu vya dunia, hata tuyasahau mambo ya mbinguni. Wakristo wakitazama mbinguni kama watu wa Galilaya wa kweli, wataendelea kumngoja Bwana Yesu mpaka atakaporudi, ama atakapowaita wakutane naye mbinguni.

# SIKU YA BWANA YA MWISHO KABLA YA PENTEKOSTE

**(Yn 15:26 - 16:4)**

*Maelezo juu ya somo.*
Kama maneno haya yalivyonenwa na Yesu, yanatoa habari za wanafunzi wake walioitwa mitume. Aliwafundisha juu ya kuja kwa Roho Mtakatifu na kazi yao ya kumshuhudia Yesu, tena juu ya mateso yatakayowajia.
Katika kulihubiri somo hili tunaweza *ama* kueleza mambo yalivyowahusu wanafunzi wale, *ama* kueleza mambo yanavyotuhusu sisi, *ama* kueleza mambo kama yalivyokuwa siku zile na kama yalivyo sasa, yote mawili. Katika maandalio yafuatayo tunafuata njia ya tatu, yaani kueleza pamoja mambo ya wakati ule na mambo ya wakati huu.

## USHUHUDA WA KIKRISTO

*1) Ni ushuhuda wa Roho.*

a) Yesu alipotembea duniani aliwaongoza wanafunzi wake katika kazi yao ya kufundisha na kuhubiri. Kwa hiyo aliweza kusahihisha makosa yao na kuwalinda hatarini. **Mt 16:23; 17:17; Yn 18:8–9.**
b) Siku nyingine ilikuwa lazima waende peke yao, pasipo msaada unaoonekana kwa macho. Siku ile wataongozwa na Roho Mtakatifu. **Yn 14:26; Mt 10:19–20.**
c) Msaada huo wa Roho haupatikani pasipo Neno, wala kwa njia ya kupinga Neno la Mungu. Yanayokazwa na kuhuishwa, ndiyo maneno ya Baba na ya Mwana, kwa maana Roho anayaeleza kwa kila msikilizaji.
d) Haya yote yanafanywa hata sasa, ijapokuwa Yesu hatembei kati yetu kama alivyofanya siku zile. Sisi tunao ushuhuda wa kutosha katika Maandiko Matakatifu. Yesu asema: *"Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami."* (mst **27**) Ushuhuda huo Maandikoni unatosha (**Lk 10:16**), kwa maana ni Neno la Mungu, linaloshuhudiwa na Roho (mst **26**). **Yn 14:26.**

*2) Ni ushuhuda wa Mkristo kwa maneno na matendo.*

a) Yesu aliwaonyesha wanafunzi ya kuwa imewapasa kumshuhudia kwa maneno, yaani mazungumzo na mafundisho na mahubiri (mst **27**).
b) Ndivyo walivyofanya katika siku zilizofuata. **Mdo 2:7; 4:1; 5:42; 7:2; 18:9; 22:1.**
c) Haikutosha kutoa maneno tu. Katika kazi yao mitume na wanafunzi wengine walipata nafasi kutoa ushuhuda hata kwa matendo yao.
d) Ndivyo ilivyo katika nyakati zote. Ushuhuda wa Kikristo si lazima uwe ushuhuda wa kuhubiri. **Yak 3:1.** Bali uwe ushuhuda wa kusoma Neno la Mungu, na kuabudu, na kuomba, na kushirikiana Mezani. **Mdo 2:46.** Tena katika matendo mazuri na ukweli. **1 Pet 2:12; 3:15–17; Yak 1:23,27.**

*3) Ni ushuhuda hata katika wakati wa mateso.*

a) Yesu aliwafundisha sana wanafunzi wa kwanza juu ya jambo hili, ili wasistaajabu litakapofika (mst 4). **Mt 10:16–33.**
b) Ilikuwa lazima kuwa tayari kupokea hata haya. **Mt 20:22–23; Yn 21:18–19.**
c) Ndivyo ilivyotokea kabisa. *Matendo ya Mitume* yamejaa habari namna hii. **Mdo 5:40–41; 7:59–60; 12:1–3; 16:19–24; 2 Kor 11:23–28.**
d) Ndivyo ilivyo hata siku hizi katika Kanisa la Yesu. Si kila wakati ama kila mahali. Lakini hakuna karne yo yote ambapo Wakristo wengi waliteswa ama kuuawa kwa ajili ya imani yao kama katika karne yetu. Haya yanaonyesha tena ya kuwa maneno ya Yesu ni ya kweli. Upendo utapoa katika wengi, lakini rafiki za Yesu watateswa na kupata shida nyingi, labda kuuawa. **Mt 24:12.**
e) Je, ni vibaya? La! **Mt 10:24; Yn 15:20.** Yesu ametuambia ili tujue, shida zinapofika, na kutoa ushuhuda wa kweli, nafasi inapofika. **2 Tim 4:6–8.** Ndio ushuhuda wa Mkristo asiyeogopa kitu. Kufa kwa ajili yake Kristo si hasara, bali ni faida. **Flp 1:20–21.** Yeye alitufia kwa ajili ya wokovu wetu. Basi tuwe tayari kufa kwa ajili yake kama ushuhuda wetu ya kuwa yeye ni Bwana na Mwokozi wa kweli. **Yn 15:13.**

# SIKU YA BWANA YA PENTEKOSTE

## (Yn 14:23–31a)

## UZIMA UNAOFANYIZWA NAYE ROHO WA MUNGU

*1) Msingi wa uzima huo.*

a) Ni upendo wa Mungu: *"Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake"* (mst **23**).
b) Upendo huo umefunuliwa naye Yesu. Hatuwezi kuujua upendo wa Mungu pasipo kuyatazama maisha ya Yesu na kufa kwake. **Yn 3:16; 15:13.**
c) Upendo huo unaelezwa naye Roho (mst **26**).
d) Roho huyu anaendelea kuueleza upendo wa Mungu katika Neno na sakramenti. Ndivyo anavyotukumbusha yote (mst **26**).

*2) Maonyesho ya uzima huo:*

a) ni ya kuwa tutapata ushirika naye Mungu: *"... tutakuja kwake, na kufanya makao kwake"* (mst **23**).
b) ni ya kuwa tutapata amani na kukaa katika amani: *"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa"* (mst **27**).
c) ni ya kuwa tutapewa nguvu kwa maisha yetu: *"Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga"* (mst **27**).
d) ni ya kuwa tutakuwa na furaha ya kweli katika maisha yetu: *"... mngalifurahi kwa sababu naenda kwa Baba"* (mst **28**).

*3) Jinsi nasi tutakavyoweza kupewa uzima huo.*

a) Njia ni kuamini: *"... kusudi litakapotokea mpate kuamini"* (mst **29**).
b) Njia ya *kupewa* imani ni kulipokea Neno. Njia ya *kukaa* katika imani ni kushikamana na Neno. Ndiyo njia ya kufundishwa na Roho na kuokolewa: *"Mtu akinipenda, atalishika Neno langu"* (mst **23**).

*Application.* Kama wanafunzi wa kwanza walivyohuishwa kwa kazi ya Roho Mtakatifu, ndivyo inavyokupasa kufundishwa na kuhuishwa hata wewe, ili Roho aitimilize kazi ya Yesu katika moyo wako.

# SIKU YA 2. YA PENTEKOSTE (MONDAY IN WHITSUN WEEK)

**(Yn 3:16–21)**

**HABARI ZA WOKOVU**

*1) Upande wa Mungu.*

a) Msingi wa wokovu ni upendo wa Mungu: *"Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu ..."* (mst **16**).
b) Upendo huo umeonekana hasa katika Yesu Kristo: *"... hata akamtoa Mwanawe pekee"* (mst **16**).
c) Hakupenda kidogo tu, wala watu fulani tu, wala watu wachache: *"... ulimwengu .. ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"* (mst **16**).

*2) Upande wetu.*

a) Ni lazima tuupate wokovu huo. Tusipoupata, tutapotea (mst **16, 18–20**).
b) Ni vibaya sana kupotea, kama wokovu namna hii ni tayari hata kwetu (mst **16–18a**).
c) Kama Mungu alivyoutayarisha wokovu huo katika Yesu, na kwa njia ya neema, ametengeneza tuupokee kwa imani, na kwa imani tu (mst **18–19**).
d) Anayekataa kuamini anajiweka nje (mst **18b**).
e) Kama imani iko, iko nafasi kwa matendo mema (mst **21**), lakini matendo haya ni matunda ya imani. Matunda hayawezi kuutangulia mti unaoyazaa. Lakini kama mti uko, wenye uzima, basi matunda yaweza kuanza kupatikana.

# SIKU YA BWANA YA UTATU

**(Yn 3:1–15)**

## KUZALIWA MARA YA PILI

*1) Ni lazima kuzaliwa mara ya pili.*

a) Nikodemo hakufahamu haya, kwa kuwa alikuwa amefungwa katika mawazo ya Kiyahudi na Kifarisayo ya kwamba kila mmoja anayefuata masharti ya Sheria ataokoka.
b) Watu walio wengi, naam, karibu wote, wamefungwa katika mawazo namna hii. Hawaifahamu kweli hii ya kuwa ni lazima kuzaliwa mara ya pili. Nikodemo aliuliza kama mama yake atamzaa tena (mst **4**).
c) Yesu anaonyesha ya kuwa pasipo kuzaliwa mara ya pili hatuwezi kuuona ufalme wa Mungu (mst **3**). Yesu anaithibitisha kweli hii kwa njia tatu.
i) Hakuna mtu aliyepaa mbinguni. Hakuna anayeweza.
ii) Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili.
iii) Kwa hiyo ni lazima kuzaliwa kwa maji na Roho.
d) 'Mwili' ni ile hali ya watu wote baada ya anguko dhambini. Ingawa tunajaribu sana sana, hata kwa matendo yetu yaliyo mazuri mno, hatuwezi kujiinua mbinguni (mst **13**). Twaendelea kuwa 'mwili' tu. Wote waliozaliwa na baba na mama hapa duniani wataendelea kuwa wenye dhambi, wasiweze kujiokoa ama kuacha dhambi zote.
e) Hata Wayahudi na Mafarisayo, waliokuwa na bidii sana katika kuishika Sheria, walikosa wote. Aliyekuwa mtu mzuri sana, bila shaka, aliambiwa naye Yesu: *"Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?"* (mst **10**).

*2) Inawezekana jinsi gani kuzaliwa mara ya pili?*

a) Haiwezekani kwa nji ya 'mwili', iliyo njia ya kisheria. Baba na mama wote wanazaa watoto wa 'mwili' tu.
b) Inawezekana kwa maji na Roho (mst **5**).
c) Maji haya ni maji ya Ubatizo Mtakatifu. Roho ndiye Roho wa Yesu anayefanya kazi pamoja na maji ya Ubatizo na katika Neno Takatifu. Maji tu hayatoshi, yaani kubatizwa kwa maji pasipo kulitumia Neno la Mungu haina maana. Kusema au kusoma maneno tu, pasipo kutumia maji, si ubatizo.
d) Anayefanya kazi hii kubwa, ndiye Roho Mtakatifu, aliye Roho wa Baba na Mwana. Huyo Roho ni kama upepo. Huwezi kuu*ona* upepo, lakini unaweza kuiona kazi yake, upepo unapotikisa miti na majani. Huwezi kumwona Roho, bali unaweza kuangalia anapofanya kazi yake katika watu, yaani katika maisha na mioyo yao.
e) Je, tutaweza kuyafahamu kabisa mambo haya? La, siyo hapa duniani. Yalimshinda mwalimu mkubwa wa Wayahudi. Lakini aliyeshuka kutoka mbinguni, ndiye anayeweza kutueleza kadiri tunavyohitaji (mst **11–13**).

*3) Maana ya kazi hii ni nini?*

a) Ni wokovu wa kila mtu katika ulimwengu mzima. Tazama "Biblia Ndogo" katika **Yn 3:16**!
b) Watu hawakuweza kufanya lo lote kujiokoa (mst **6**).
c) Yesu tu aliweza kuwaokoa. Kazi yake kuu ndiyo kazi yake msalabani, alipowekwa kama mnyang'anyi (**Mt 27:38**) ama kama nyoka mbaya mtini (mst **14**). **Hes 21:9.** Yule mwema alitendewa kama mbaya, **2 Kor 5:21**, ili sisi tukimtazama juu ya mti na kumwamini, tuwe na uzima wa milele katika yeye (mst **15**).
d) Je, tunaweza kuacha sasa matendo ya sheria? Tuyaache kama njia ya kujiokoa wenyewe, lakini tuendelee katika matendo mema yote kama watoto wapenzi wa Mungu. Kama tumeokolewa kwa neema, basi matendo yetu ya upendo yawe kwa shukrani yetu, tunapomwinua Mwana wa Adamu (mst **14**), si katika mti wa laana (**Gal 3:13**) tena, bali katika sifa na maombi na shukrani zetu za kila siku.
e) Itakuwaje, kama tunakosa sana tena, na labda kuondoka tena kwa kutokuamini? Itakuwa lazima kuzaliwa kwa upya, lakini siyo kwa ubatizo! Ubatizo wetu wa kwanza unafaa: *"Karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake."* **Rum 11:29.** Lakini ni lazima kutubu na kumgeukia tena Mungu yule yule wa neema. Neema tunayopewa kwa upya, ndiyo ile ile tuliyopewa tulipozaliwa mara ya pili katika ubatizo wetu.

# SIKU YA BWANA YA 1. BAADA YA UTATU

**(Lk 16:19–31)**

*Maelezo juu ya somo.*
Hatari iliyo kuu hapa ni kushtaki wote wenye utajiri na kusifu wote walio maskini. Tukihubiri kwa njia hii tunasahau ya kuwa kuna watu tajiri walio Wakristo wenye imani ya kweli; wanautumia utajiri wao kwa kazi ya Mungu na kusaidia wenzao na kuendesha mambo mengi ya wananchi. Kama tukisifu maskini wote tunasahau ya kuwa wengi ni maskini kwa ajili ya uvivu wao na upurukushani ('carelessness') wao; wakiwa na kitu, wanakipoteza mara moja. – Nia ya Yesu *si* kushtaki walio tajiri na kusifu walio maskini. Nia yake *ni* kutuonya sote juu ya ***hatari za ulimwengu huu,*** yaani sote tunaweza kukamatwa na mambo ya ulimwengu huu, hata tuzisahau roho zetu. Tena anakaza ya kwamba ni wajibu wa kila mtu kuuangalia wokovu wake wa milele.

## UTAJIRI NA UMASKINI

*1) Utajiri.*

a) Utajiri wenyewe si dhambi. Si dhambi ya kuwa mtu huyu tajiri alikuwa na mali nyingi, kama amezikusanya ama kuzirithi kwa njia safi. Lakini mtu huyu alikosa alipozitumia mali zake kwa *umalidadi* na *anasa*. Tena alikuwa na *kiburi*. Hatuna habari ya kuwa alikuwa mfalme, lakini alivaa mavazi ya kifalme (zambarau).
b) Alipoteza nafasi nzuri. Angaliweza kusaidia na kufurahisha wengi. Angaliweza kuisaidia hata kazi ya Mungu kwa pesa zake zote. Lakini ali–shindwa katika haya yote, kwa sababu mungu wake alikuwa tumbo. **Flp 3:19.**
c) Utajiri ulimshinda huyu, kwani utajiri ni wenye *hatari kubwa*. Kwa kujipenda kwake alikuwa mkali sana, yaani ni kama hakumwona maskini mlangoni. Lakini alimsahau maskini, kwa sababu alikuwa amemsahau Mu–ngu, mwenye kutoa vipaji vizuri vyote.
d) Utajiri ulimtega yule tajiri, hata akapoteza wokovu wake wa milele.
e) Ni neno kwako! Ujiulize: *"Mimi ni huyu tajiri?"* Usiseme: *"Nina mali kidogo kidogo tu."* Unaweza kuipoteza roho yako hata kwa ajili ya mbuzi mmoja ama shilingi moja, kama unaipenda mali hii kuliko Mungu, au ku–angalia mali hii kuliko wokovu wako. Tena, unaweza *kufikiria utajiri wa wengine,* kwa tamaa na tamani, kila siku na labda kila saa, hata usahau kuufikiria wokovu wako.

*2) Umaskini.*

a) Umaskini *si* mzuri kuliko utajiri. Zote zinaweza kuwa nzuri, tena zinaweza kuwa mbaya na kuleta hatari.

b) Umaskini unaweza kuiba nguvu yako. Ukifikiri kila siku na kila saa, *"Nitapata wapi chakula changu"*, utashindwa kufikiria roho yako na wokovu wako. Tena, maskini anaweza kupoteza nguvu zake ndogo kwa kupigana na wale tajiri wanaomtesa, na kwa kuonyesha hasira na uchungu wake. Haya ni mizigo mikubwa miwili: Umaskini wenyewe, na uchungu ule unaofuata umaskini na njaa.
c) Lakini kuna faida mbili upande wa umaskini: mwenye umaskini anasaidiwa kuwa mnyenyekevu, kwa hiyo anaweza kuwa tayari kupokea msaada kutoka kwa watu na kutoka kwa Mungu. Tajiri labda atajitoshea tu.

*3) Wewe ni tajiri ama maskini?*

a) Shauri kuu leo *si* kama una mali nyingi ama kidogo tu. Tajiri anaweza kupotea, naye maskini anaweza kupotea pia. Tajiri anaweza kuokoka, naye maskini anaweza kuokoka pia.
b) *Shauri kuu ni kama umefanywa maskini mbele ya Mungu* katika unyenyekevu wa kweli na katika kuzijua dhambi zako. Yaani ni lazima tuwe sote kama waombaji maskini mbele yake Mungu. **Lk 18:35–38.**
c) Shauri kuu tena ni *kupata utajiri wa kweli* unaofaa mbele yake Mungu. Si ule wa pesa na mali, wala ule wa malidadi na anasa, bali ni ule unaohesabiwa mbinguni. **2 Kor 8:9; Ufu 3:17–18.**
d) Lazaro aliokoka, *siyo* kwa sababu alikuwa maskini kwa njia ya pesa; *siyo* kwa sababu alikuwa na shida nyingi duniani. Shida zetu haziwezi kutuokoka, kwa sababu shida nyingi zinatufikia kwa ajili ya dhambi zetu. Lazaro aliokoka kwa sababu alikuwa amemwendea Mungu kwa maombi na imani. Jina lile 'Lazaro', maana yake ni 'Mungu anasaidia'.
e) Wewe je? Iko njia moja tu kuokoka: *ni kufanywa maskini* kwa njia ya kweli (ni njia ya toba) na *kufanywa tajiri* kwa njia ya kweli (kuipokea haki na neema ya Kristo). Haya yawezekana kama unalisikiliza Neno ("Musa na manabii"). Kuyakataa Maandiko na kuomba ufunuo mwingine (mst **27–28**) ni kiburi cha ajabu. Njia ya wokovu ni kupokea mafundisho ya Neno (mst **31**).

# SIKU YA BWANA YA 2. BAADA YA UTATU

### (Lk 14:15–24)

### MWITO WA MUNGU NA JIBU LETU

*1) Mwito wa Mungu.*

a) Mungu anatuita kwa njia nyingi, kwa Neno lake, kwa ibada ya Kanisa, kwa wachungaji na wainjilisti, kwa wazazi Wakristo, kwa marafiki wema wanaosema: *"Njoo, uone."* **Yn 1:46.**
b) Anatauita kwa nini? Anatuita tuingie ufalme wake. Kuwapo katika ufalme huo kunafananishwa na karamu kubwa. Huko ni furaha kubwa. Kweli mawazo yetu ya kidunia hayawezi kuifahamu furaha hii. Lakini si lazima kwetu kujua kabisa itakuwa namna gani humo mbinguni, ila ni lazima kujua vizuri njia ya kufika mbinguni. Ni lazima kujua, Mungu anatuita kwa njia gani, na sisi tuupokee mwito wa Mungu kwa njia gani.
c) Ingawa tumesaidiwa na watu wengine (taz a) juu), ni Mungu mwenyewe anayetuita kwa ufalme wake. Tunaitwa kwa msaada wa Kanisa lake. Mwito ulio mkuu unafanywa katika ubatizo wetu.
d) Mwito wa Mungu unaendelea. Pengine waliobatizwa wanamwacha Mungu na kutoka. Kwa hiyo anaendelea kuwaita, ili watubu, warudie nyumba ya Baba.

*2) Jibu letu.*

a) Mfano wa Yesu unatuonyesha waziwazi jinsi tulivyo. Wale walioitwa na kukataa walikuwa wa namna mbalimbali, lakini walikataa mwito wa yule bwana.
b) Wote walikuwa na kizuizo fulani. Kama hawakuwa nacho, walifanya haraka kutafuta kizuizo, wasiende karamuni.
c) Yesu anaonyesha ya kuwa vizuizo vile si vya kweli. Yaani mwenye shamba angaliweza kulitazama siku nyingine. Mwenye ng'ombe angaliweza kuwajaribu siku nyingine. Je, alinunua ng'ombe jozi tano pasipo kuwapima kwanza? Kweli alikuwa mjinga! Mwenye mke, alikuwa mjinga vile vile, kwa maana angaliweza kwenda naye karamuni na kupata bure karamu kubwa ya arusi!
d) Ndivyo tunavyotafuta vizuizo mbalimbali, tunapoitwa naye Mungu. Tunasema moyoni: *"Kazi yangu au jambo langu ni la haraka, linanizuia, siwezi kusoma Neno la Mungu, siwezi kwenda kanisani Jumapili hii, siwezi kuwa Mkristo sasa, labda kesho ama siku nyingine."* Yaani wanaoshindwa kufika kanisani siku hizi, ama kuomba, ama kukipokea Chakula cha Bwana, wanazuiwa na mambo gani? Je, si yale ya zamani, yaani mashamba, na ng'ombe, na ndoa n k?
e) Labda kuna mmoja aliyekuwa Mkristo zamani, lakini baadaye alioa au kuolewa. Na sasa je? Yule mke au mume anamzuia.

*3) Je, itatukia nini, ukikataa?*

a) Si vigumu kufahamu. Anayekataa kuupokea mwito, hataingia karamuni (mst **24**). Badala yao walioitwa kwanza wataalikiwa wengine, ili nafasi zote zijazwe.
b) Ndivyo ilivyo katika Kanisa. Wengine wanaacha, wakichoka kuwa Wakristo. Mungu anaita wengine, wazishike nafasi zao. Chumba cha karamu hakiwezi kuwa kitupu.
c) Mungu anaendelea kuita. Usifikiri: Ni vizuri ya kuwa watu wanaitwa na kuingia karamuni. La, imekupasa kujiuliza hivi: Nafasi ile iliyotengenezwa kwangu, je, itashikwa na mimi mwenyewe, au itashikwa na mwingine? – Kwa maana ukibaki nje, ni kwa sababu umejiona nafsi yako kuwa hukustahili uzima wa milele. **Mdo 13:46.**

# SIKU YA BWANA YA 3. BAADA YA UTATU

**(Lk 15:1–10)**

## YESU AMEKUJA KUTAFUTA NA KUOKOA KILE KILICHOPOTEA

*1) Yesu amekuja kutafuta kilichopotea.*

a) Watu wa ulimwengu ni *"kama kondoo wasio na mchungaji"*. **Mt 9:36.** Lakini hapa Yesu anaonyesha zaidi upendo wake, kwani anaangalia *kila kondoo* aliyepotea. Mchungaji mwema anahuzunika sana *"akipotewa na mmojawapo"*.
b) Vile vile mwanamke anahuzunika, *"akipotewa na moja"* katika shilingi zake kumi.
c) Kwa mfano huu wa mwanamke Yesu ametoa hata habari za Kanisa lake, yaani imelipasa Kanisa kuangalia sana watu, kila mmoja peke yake, kama mwanamke anavyoangalia kila shilingi. Kila roho ina thamani kubwa mno. **Mt 16:26.** Kwa hiyo mtumishi wa Kanisa ana wajibu mkubwa juu ya kila roho aliyewekwa katika uchungaji wake.

*2) Yesu amekuja kuokoa kilichopotea.*

a) Kweli anataka kuokoa wote. **Mt 28:19–20; Mk 16:15.** Lakini wengine hawakubali kuokolewa. *"Hawana haja ya kutubu."*
b) Anayeungama ya kuwa ni mwenye dhambi anakubali kuokolewa, kama yule kondoo aliyepotea, na yule mwana mpotevu (mst **17**).
c) Huyu anayechukuliwa nyumbani (mst **5–6**) anaokolewa. Anarudishwa alipotoka.
d) Hiyo ndiyo furaha ya wokovu. Ilikuwa huzuni kubwa alipopotea, sasa ni furaha kubwa mno hata mbinguni (mst **7, 10**).

*3) Anayeendelea kukaa katika mikono yake aliyemwokoa, ndiye atakaye–okolewa milele.*

a) Aliyeokolewa kwa neema ya Mungu anaweza kutoroka na kupotea tena. **Yn 6:66.**
b) Ni lazima kukaa naye Yesu, kama tumetafutwa na kuokolewa naye. **Lk 21:19; Ufu 2:10.**
c) Tukiokolewa kwa njia kamili, maana yake: tukifa kwa imani, itakuwa furaha kubwa zaidi mbinguni (mst **7, 10**).

*Application.* a) Nawe ni mwenye dhambi, yaani kondoo aliyepotea. b) Ukitubu, basi wengine watanung'unika, ni wale wanaofikiri ya kuwa tuji–takase sisi wenyewe kwanza, na baadaye kufika kwa Kristo. *"Hawana haja ya kutubu"*. c) Lakini ukitaka kuokolewa, iko njia hii tu, kumpokea yeye aliyefika hapa kukutafuta na kukuokoa. d) Akikuchukua nyumbani, kweli utafika nyumbani. e) Furaha itakuwa kubwa mbinguni juu ya mwenye dhambi huyu, yaani malaika wataufurahia wokovu wako.

# SIKU YA BWANA YA 4. BAADA YA UTATU

**(Lk 6:36–42)**

**HURUMA YA MUNGU NA HURUMA YA WATU**

*1) Huruma yetu mara nyingi ni ndogo kabisa.*

a) Labda tunayo desturi ya *kunena* juu ya huruma. Lakini tusijiite mafundi katika jambo hili, *"maana mwalimu wenu ni mmoja"*. **Mt 23:8.** Yesu tu ni mwalimu katika ufundi wa huruma.
b) "Huruma" ya watu ni kama yule mwenye boriti jichoni mwake, aliyetaka kumsaidia mwenzake kuondoa kibanzi (mst **41**).
c) "Haki" ya watu ni kama wale makadhi (waamuzi) waliomkamata mwanamke katika tendo la uzinzi. Yesu alisema: Basi, ni vizuri kuifuata sheria, lakini tuifuate kabisa, kwa hiyo wasio na kosa wenyewe walitupe jiwe la kwanza. **Yn 8:1–11.** Wakatoka wote, kwa maana walikuwa na kosa wenyewe, labda kosa la kuzini, labda la kuzini pamoja na yule mwanamke. Lakini walitaka kumwua, kwa ajili ya sheria na haki! Ndivyo watu walivyo!
d) Kwa hiyo Yesu anafundisha sana: *"Iweni na huruma!"* (mst **36**).

*2) Huruma ya Mungu ni kubwa.*

a) Yesu anasema neno hili *"Iweni na huruma"* kwa makusudi mawili. Kwanza tuone ukosefu wetu na dhambi zetu, tumwendee Mungu kuipokea huruma yake. Pili, kama tumeipokea huruma ya Mungu, tukae katika skuli ya huruma yake, yaani tuanze kufanana na mwalimu wetu, aliye fundi peke yake (mst **40**).
b) Haina maana kuanza kubadili matendo yetu sisi wenyewe, kwa maana Yesu anasema ya kuwa sisi wenyewe ni wabaya. **Mt 12:34; Rum 7:18.**
c) Huruma ya Mungu ilionekana kwa jinsi ile alivyompeleka Mwana wake wa pekee ili kutuokoa sisi wenye dhambi. **Yn 3:16; Rum 5:6.**

*3) Huruma ya Mungu inaweza kufanya hata watu wawe na huruma.*

a) Mungu anataka huruma ile tuliyopewa sisi ionekane hata katika maisha yetu. *"Iweni na huruma kama Baba yenu alivyo na huruma"* (mst **36**).
b) Kama sisi tunakataa kuhurumia wenzetu, Mungu atanyima hata huruma ile tuliyokwisha pewa. *"Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyo–wasamehe waliotukosea." "Achilieni, nanyi mtaachiliwa"* (mst **37**). Mfano ulio mkubwa hapa ni yule mtumishi aliyeachiliwa talanta kumi elfu na baadaye kumkamata mwenzake kwa ajili ya deni dogo mno. **Mt 18:28.**
c) Sisi tukikataa kuhurumia wenzetu kama Mungu alivyotuhurumia sisi, basi madeni yetu yote yatahesabiwa tena, tutendewe kwa ukali wote wa Mungu.

*Application.* a) Ni nani aliye fundi sasa wa huruma, ni wewe ama Yesu? b) Iko njia moja tu kwako, ndiyo ya kumkimbilia yeye na kuomba neema kwa ajili ya huruma yake kuu. c) Tena uombe neema ile ya kupewa kipimo kikubwa cha huruma (mst **38**), ili uwe na kipimo kilichojaa katika matendo yako yote unaposhirikiana na wenzako.

# SIKU YA BWANA YA 5. BAADA YA UTATU

**(Lk 5:1–11)**

## JINSI BWANA YESU ANAVYOONGOZA WATU WAKE, HATA KATIKA UVUVI WA WATU

*1) Anaita wasaidizi.*

a) Hakuna anayeweza kusaidia katika ufalme wa Mungu, isipokuwa ameitwa kwanza. **Yn 15:6.**
b) Kuna kazi mbalimbali, zile za wanafunzi, mitume, manabii, wachungaji, wahubiri, n k, kwa hiyo watumishi wote hawafanani, lakini *ni lazima wote waitwe*.
c) Hawawezi kumtumikia Mungu mara moja kama walivyo. Ni lazima awafundishe, labda masomo mengi, labda masomo magumu.

*2) Anawaonyesha njia zinazofaa.*

a) Anaonyesha: usikate tamaa, ingawa umefanya kazi wakati mrefu pasipo kuona matunda yo yote.
b) Anaonyesha: *"Tweka mpaka kilindini"* (mst **4**). Maana yake: Nenda chini katika mambo ya ufalme wa Mungu. Kufanya kazi kwa haraka na kijuujuu tu, haileti baraka. Hapa wengi wanakosa. Ingawa wamekabidhiwa kazi ya Mungu, hawaifanyi kwa bidii. Wanaifanya kwa kipimo cha kutosha, ili kuepuka kushtakiwa, si zaidi. Lakini usifanye kipimo kilicho kidogo kuliko uwezo wako, bali fanya kilicho sawa na uwezo wako. **Lk 17:10.**

*3) Kushinda kazini, si jambo la uwezo wetu, bali ni jambo la uwezo wa Mungu.*

a) Hata wavuvi hodari walishindwa katika kazi yao, lakini Yesu alipoingia kuwaongoza, ndipo walipofaulu kabisa.
b) Kama wafanya kazi wa Mungu katika Kanisa lake, hatutashinda kwa ajili ya uwezo wetu ama uhodari wetu; tutashinda kwa njia iyo hiyo tu, ya kuwa Yesu ni pamoja nasi.
c) Kutweka mpaka kilindini, maana yake ni kufuata uwezo wote wa Mungu, *"awezaye kufanya mambo ya ajabu mno."* **Efe 3:20.**

*4) Tunapotaka kujitukuza, tutashindwa; tunapomtukuza Mungu, tutafaulu.*

a) Petro na wengine walishindwa walipojaribu katika jina lao na uwezo wao wenyewe.
b) Yesu alipoingia kazini, Petro alishikwa na ushangao: *"Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi."* Aliponyenyekezwa, ndipo alipoweza kukwezwa. **Mt 23:12.**
c) Baada ya kumfundisha sana mwanafunzi wake, Yesu alimfanya mvuvi wa watu (mst **10**).

# SIKU YA BWANA YA 6. BAADA YA UTATU

**(Mt 5:20–26)**

**HAKI KAMILI**

*1) Haki kamili ni nini?*

a) Haki kamili inapatana kabisa na mapenzi matakatifu ya Mungu na sheria yake takatifu.
b) Watu wanaojaribu kuifuata sheria ya Mungu hujiita watakatifu, lakini utakatifu wao hautoshi (mst **20**).
c) Kwa maana watu hufuata maagizo na amri za nje. Labda wanajaribu kuondoa makosa yao ya nje, yaani makosa yanayoonekana kwa watu wengine. Lakini ni kutafuta usafi wa nje tu. Bali haki kamili inadai utakatifu hata wa mawazo, na maneno, na matendo. **Ebr 4:12–13.**
d) Watu husema: "Usifanye hivi ...", "usiguse ...", n k. Ndiyo *maagizo ya kukataza*. Bali haki ya Mungu inadai *tufanye yaliyo mema*, yaani haitoshi kuacha yaliyo mabaya. Sheria inadai: *"Upende ..."*, *"Usaidie ..."*, n k. *"Hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache."* **Mt 23:23.**
e) Kwa hiyo haki yote ya watu inashindwa na kupunguka, kama
inachagua amri fulani, na kuacha nyingine,
inakaza masharti ya matendo, na kuacha moyo na nia zake,
inakataza makosa, na kusahau matendo mema.

*2) Ni nani aliye na haki hii kamili?*

a) Mafarisayo na waandishi hawakuwa nayo (mst **20**).
b) Wewe mwenyewe huna haki hii. Huwezi kujipatia haki hii kwa uwezo wako. Tazama k m habari za hasira (mst **22**), *"neno la ndugu juu yako"* (yaani umemkosea kwa njia fulani) (mst **23**). Kwa nini unakosa haki hii? Maelezo ndiyo haya: **Mt 5:18–20** na **Rum 7:17–21**.
c) Huyu anayetufundisha katika somo hili anayo haki hii. Anadai haki kutoka kwetu, kwa sababu yeye ni mwenye haki. **Yn 8:46; Mt 5:48; Yn 17:19.**
d) Anapoieleza Sheria yake, si kama masharti ya ukali au nguvu, kama watu wanaponena kisheria, bali anatoa habari za ufalme wake na nafsi yake mwenyewe, kwa maana yeye anataka kuitoa haki yake kama anavyotoa upendo.

*3) Bwana Yesu anataka kufanya nini nayo haki hii kamili?*

a) Anataka kuitoa kwetu. Kwa hiyo alifika ulimwenguni. **Rum 3:26.**
b) Kwa hiyo anatuonyesha ya kuwa sisi wenyewe hatuna haki. Kwa hiyo anatumia sheria yake juu yetu kwa ukali kabisa. **Mt 5:17; Lk 10:28.** Sheria yake itatuongoza kwake, tunapoona ya kuwa tunashindwa sisi. **Gal 3:24.**
c) Kama kwa Neno lake na Roho wake Mtakatifu amefumbua ukosefu wetu mkubwa na dhambi zetu nyingi, anaweza kuumba ndani yetu njaa na kiu ya haki. **Mt 5:6.** Yeye mwenyewe, ndiye anayeweza kutushibisha kwa haki, yaani kutupatia haki yake. Inawezekana tunapompokea kwa imani. **Rum 3:28.**
d) Kama tumehesabiwa haki na Kristo, tungewezaje kuishi dhambini? **Rum 6:2.** Kama tumeunganishwa naye Kristo, basi uzima wake na haki yake zitakaa ndani yetu. **1 Kor 6:15.** Zitaendelea kubadili maisha yetu siku kwa siku. Tutatakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele. **Rum 6:22.**

# SIKU YA BWANA YA 7. BAADA YA UTATU

**(Mt 17:1–9)**

## PAMOJA NAYE YESU MLIMANI

*1) Pamoja na Yesu ni wakubwa wa Agano la Kale.*

a) Mkubwa wa Sheria, yaani Musa. Kufuatana na ahadi Yesu ni mfuasi wa Musa. **Kum 18:15–18; Yn 5:46.**
b) Mkubwa wa Unabii, yaani Eliya. **Lk 24:44; Yn 1:45; Mdo 3:18–26.**
c) Sheria na Unabii ndiyo mafundisho kamili ya Kikristo, kwa hiyo inaelezwa hapa ya kuwa Yesu kwa kweli ndiye Masihi, yaani Kristo atakayekuja ulimwenguni kuokoa watu.

*2) Pamoja na Yesu ni wanafunzi watatu.*

a) Ni neema kubwa kwao, kwa sababu neema hii haikutolewa kwa mwanafunzi mwingine ama mtume mwingine.
b) Sisi hatuwezi kungoja maono kama hayo, kwa sababu wale mitume watatu ni wajumbe wa Wakristo wote wa nyakati zote. Kama hawa watatu wamepata habari zinazotosha, kweli tumezipata nasi. Wanatoa ushuhuda wao (**2 Pet 1:16–18**), kwetu inabaki kuamini. Linganisha: Yesu alifufua watu watatu, inabaki kwetu kuamini ya kuwa anaweza kutufufua nasi katika siku ya mwisho.
c) Hatuna ruhusa kuomba maono makuu kama yale mlimani. Yesu amesema inatutoshea kutegemea Neno lake na neema yake. **Yn 20:29; 1 Pet 1:8; 2 Kor 5:7.**

*3) Nasi twaweza kuwa pamoja naye Yesu.*

a) Si uso kwa uso kimwili. Si kwa njia ya maono mlimani.
b) Kwa mikono ya mitume wake ametupatia sisi Neno lake takatifu na ahadi kubwa na ushuhuda mwaminifu. Yanasema kwa sauti moja: "Msikieni" (mst 5).
c) Utukufu wa Yesu unaonekana po pote duniani katika Kanisa lililo na kazi hii tu: Kuonyesha utukufu wa milele na kuwaingiza watu humo.

# SIKU YA BWANA YA 8. BAADA YA UTATU

### (Mt 7:15–21)

### MANABII WA UONGO

*1) Manabii wa uongo wako kweli.*

a) Watu wengine husema manabii wa uongo hawako. Wanasema hivi, kwa sababu wao wenyewe hawajisumbui na Neno la Mungu ama wokovu wao hata kidogo.
b) Wasikilizaji wengine wengine husema: "Ni vizuri kumsikiliza kila mmoja anayehubiri. Kila mmoja ana ruhusa kutoa maono yake." Ndiyo, kufuatana na sheria nyingi za kidunia ni hivyo, lakini kama mhubiri ana-kosea Neno la Mungu, hana ruhusa kujiita Mkristo.
c) Desturi nyingine ya manabii wa uongo ni kufikiria faida yao. **Yn 10:13.**
d) Tunaposikiliza manabii wa uongo wana uso mzuri. Kama tumefumbua hila yao na kutaka kuwashtaki kwa ajili ya udanganyifu wao, kumbe wa-metoroka au kujificha.

*2) Manabii wa uongo wanaleta hatari sana.*

a) Hatari ni ya kuwa ubaya wao na hila yao hazionekani wazi. Waonekana kama Wakristo, yaani kondoo wa kundi (mst **15**).
b) Hatari ni ya kuwa wanasema: "Hapa ni Neno la Mungu", ingawa wana-leta maneno mengine na maono yao ya uongo. Wasikilizaji wanafikiri: Hu-yu hawezi kutudanganya, *kwa sababu anasema ya kuwa analeta Neno la Mungu*. Je, unafikiri ya kuwa mdanganyifu ama mwizi ama mbwa–mwitu atapiga kelele na kusema: "Msifike hapa kuniangalia, kwa maana mimi ni mdanganyifu (ama mwizi, ama mbwa–mwitu)"? La, *ubaya unajificha kila wakati katika mavazi ya wema!*
c) Kwa hiyo hatari inapatikana kwetu sisi sote. Hatujui hatari yetu inajificha wapi sasa.
d) Basi, tunaweza kufumbua jinsi gani manabii wa uongo? Yesu asema: *"Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua"* (mst **20**). Matunda ni nini? Je, ni matendo mema? La! Matunda ambayo yanaweza kupimwa ni imani ya kweli. Kama nabii (au mchungaji, au mhubiri) anatuonyesha kwa Kristo na Neno lake na njia ya kupata imani ya kweli na ya kumwamini Kristo na kuitegemea haki yake, basi anatoa matunda mema. Roho huyu ametoka kwa Mungu. **1 Yoh 4:1–3; 2 Yoh mst 7–11.**

*3) Kwa hiyo, jihadharini na manabii wa uongo.*

a) Si mhubiri fulani anayesema hivi, kwa sababu anamchukia mwenzake. La, maneno haya ni ya Yesu mwenyewe (mst **15**).
b) Tunaweza kujihadhari kwa njia gani? Kwa kulishika Neno la Mungu, kuitafuta kweli iliyomo katika Neno la Mungu tu, na kujipatia hekima na mafundisho na silaha zinazopatikana katika Neno tu.
c) Tena tunahitaji maombi. **Mk 9:29; Kol 4:2; 1 The 5:17.**
d) Haya yote yataumba ndani yetu unyenyekevu na utii. Hatutataka mafundisho mengine kuliko yale ya kweli. **2 Tim 3:14–17.**

# SIKU YA BWANA YA 9. BAADA YA UTATU

**(Lk 16:1–9)**

*Maelezo juu ya somo.*
Hilo ndilo somo ambalo watu wengi hufikiri ya kuwa ni gumu kuliko mengine yote. Wanasema: "Je, Yesu anatufundisha hapa kufanya matendo mabaya?" – La, hafundishi vile, lakini tuangalie sana anafundisha nini!
Yesu anasema tufanane na wakili yule katika jambo fulani. Katika jambo lile yule wakili anashinda hata Wakristo wengi. Lakini katika jambo jingine tusifanane na yule wakili, kwa maana alikuwa mwizi. Hata siku nyingine Yesu anatumia mifano ya watu wabaya, ili atufundishe neno fulani. Tazama rafiki aliyesaidia, **Lk 11:7**, na kadhi asiyemcha Mungu, **Lk 18:2**. Maana yake ni ya kuwa: *Tunaweza kujifunza mambo fulani hata katika watu wabaya, lakini mambo fulani tu, si yote!*

## WAKILI MBAYA ANATUFUNDISHA NINI?

*1) Tusimfuate katika matendo yake mabaya.*

a) Tukumbuke ni vitu gani vilivyo vyetu, na vitu gani vilivyo vya mwenzetu, tusiibe mali ya mwingine. – Huyu wakili alisaidia wengine, lakini aliiba mali ya bwana wake na kumdanganya sana.
b) Tukumbuke ya kuwa vitu vyote vinatoka kwa Mungu, na ya kuwa siku moja vitakwisha na kumalizika. – Huyu wakili alifikiri ya kuwa vitu vyote ni vya watu na kwa hiyo inawezekana kujipatia tu.
c) Tukumbuke ya kuwa siku moja tutatoa hesabu ya vitu vyote tulivyo-kabidhiwa. Tuwe tayari kila siku kutoa hesabu iliyo sawa. – Huyu wakili alishikwa na haraka, alipopata habari za hesabu, kwa hiyo alijiingiza katika udanganyifu mkubwa zaidi.

*2) Tumfuate katika kufikiria siku zijazo.*

a) Aliona ya kuwa hakuweza kujisaidia mwenyewe. Kwa hiyo alitengeneza apate msaada katika siku za shida. Ndivyo wanavyofanya watu wa ulimwengu: wanafikiria siku zitakazokuja. – Lakini Wakristo je? Mara nyingi wanasahau kufikiria siku ya mwisho na siku ya hukumu. Basi, tuwe tayari kwa siku zijazo, lakini kwa msaada wake anayeweza kutusaidia kweli kweli.
b) Alipopata habari za hesabu, alifanya shauri kwa haraka, ili awe tayari. – Lakini sisi, tunapofikiria siku ya hukumu, tunachelewa kwa nini? Nasi, tujiweke tayari kwa hesabu, kwa haraka, lakini pasipo udanganyifu!
c) Wakati mfupi uliobaki aliutumia sana sana. – Nasi, tutumie vizuri wakati wetu mfupi, ulio wakati wa neema.

*Application.* Wakili mbaya aliujua ulimwengu huu tu, lakini alikuwa na akili ya kutosha kufikiria siku zijazo. Alitengeneza awe na marafiki watakaokuwa tayari kumsaidia katika siku mbaya. Kwa kusudi hilo alitumia hila na wizi, kwa maana alikuwa mwizi na mtu mbaya. Hakujua njia nyingine.

Lakini wewe je? Akili yako inashindwa na ile ya mtu mbaya? Umeanza kuifikiria siku ya hesabu, yaani siku utakapoondolewa kazini na kufanya hesabu mbele ya Mungu? Wapi rafiki anayeweza kukusaidia siku ile? Marafiki wa duniani hawawezi. Vyeti vya udanganyifu haviwezi. Rafiki mmoja tu, yaani yule anayeondoa dhambi zako hapa duniani. Yeye akiwa Mwokozi wako utaweza kusimama mbele ya mwamuzi mkuu. Ndivyo inavyokupasa kufikiria siku ya hesabu. Uwe na akili ya kweli.

# SIKU YA BWANA YA 10. BAADA YA UTATU

**(Lk 19:41–47)**

*Maelezo juu ya somo.*

Yerusalemu una maana sana katika historia takatifu. Ndipo Ibrahimu alipofika kumtoa mwana wake, Isaka. **Mwa 22:2.** Ndipo Daudi alipojipatia kiwanja cha kujenga Hekalu, ndipo Sulemani alipolijenga. Ndipo manabii wengi walipohubiri Neno la Mungu. Kweli watu wa Yerusalemu walikuwa wamepewa neema nyingi. Lakini waliipokea jinsi gani? Jibu linapatikana katika somo hili: Yesu anaulilia mji huu. Watu hawakuipokea neema ya Mungu.

Watu wa Yerusalemu walionyesha dharau yao kwa njia nyingine: Hawakuiheshimu nyumba ya Mungu, bali ikafanywa nyumba ya biashara. Kwa hiyo Yesu anawaonya watu, anawalilia. Tena anatoa habari za hukumu itakayowafikia kwa ajili ya kukataa neema katika wakati walipojiliwa.

## WAKATI WA KUJILIWA KWETU

*1) Tumekuwa na nyakati nyingi namna hii.*

a) Wayahudi walikuwa wamejiliwa na watumishi wengi wa Mungu walioleta Neno la kweli.

b) Mji wa Yerusalemu ulikuwa umejiliwa na neema ya Mungu kuliko miji yote.

c) Nasi tumejiliwa na neema ya Mungu, kwani wahubiri wa Neno Takatifu wamefika hapa. Tumepata nafasi nyingi kulisikia Neno la wokovu.

*2) Nyakati nyingi namna hii zimepita bure.*

a) Watu wa Yerusalemu waliokuwa na manabii na walimu wengi kuwapatia Neno la Mungu hawakusikiliza. **Mt 23:37.**

b) Nyakati zile za neema zilipita bure. Hawakuangalia majira ya kujiliwa kwao. Wasiposikiliza hawakujua yapasayo amani (mst **42**). – Kwa hiyo hawakuweza kuepuka hukumu inayofuata uasi na dhambi (mst **43–44**).

c) Nyakati za neema zimepita hata kwetu, kwa maana Neno halikupokewa na wengi. Au, kama wamelipokea, wamelipokea kwa ajili ya faida itakayofuata. Ni kufanya biashara Hekaluni! – Kama tumelikataa Neno la neema, ama tumelipokea kwa ajili ya faida ya kidunia tu, basi itafika hukumu juu yetu.

*3) Labda tunaweza kupewa wakati mwingine wa kujiliwa.*

a) Yesu alifika Yerusalemu siku hii ya mwisho, ingawa walikuwa wamekataa maneno yake siku nyingine nyingi. Sasa aliwapatia nafasi nyingine tena. Alifanya hivi kwa ajili ya upendo wake.
b) Alilisafisha Hekalu. Ndilo tendo la ajabu la Masihi (Kristo) ili kuwapa maonyo ya mwisho.
c) Labda Mungu anatupatia sisi nafasi nyingine ya kulisikia Neno lake lililo la wokovu. Kama itapatikana nafasi nyingine tena, hatujui. **2 Kor 6:2.**
d) Kwa hiyo ni lazima kuangalia nafasi hii inayopatikana. **Ebr 3:15.** Yaani Yesu ametumia mafundisho makali (mst **45; Yn 2:15–17**) na machozi, yote mawili, ili kuishinda mioyo yetu migumu, tusichelewe kulipokea Neno linaloweza kuziokoa roho zetu. **Yak 1:21.**

# SIKU YA BWANA YA 11. BAADA YA UTATU

**(Lk 18:9–14)**

*Maelezo juu ya somo.*
Pengine inaonekana ni kazi nyepesi kuhubiri juu ya somo hili. Lakini ni vigumu, kwa maana mambo ya somo hili yanachanganywa sana katika mahubiri mengi. Wahubiri wengi wanachora farisayo kama mtu mbaya sana, na mtoza ushuru kama mtu mwema. Lakini katika mambo yaliyo mengi farisayo alikuwa mwema, tena mfano mzuri, bali mtoza ushuru alikuwa mbaya katika mambo mengi. Lakini hapa Yesu anaangalia mambo matatu tu: hawa wawili wanaungama nini? Wanaomba nini? Wanamtegemea nani? Ndiyo mambo makubwa katika Ukristo. Kwa hiyo mfano wa watu hawa wawili unaweza kutufundisha juu ya

## HAKI YA KWELI

*1) Farisayo anafikiri ya kuwa anaweza kuifanya haki hii mwenyewe.*

a) Farisayo alikuwa mtu mzuri katika mambo mengi. K m aliomba mara nyingi na kwa taratibu. Aliikubali Sheria takatifu ya Mungu, akafanya bidii kuifuata. Haya yote ni mazuri. Imetupasa kufanana naye katika hayo.
b) Lakini farisayo alifikiri ya kuwa ameitimiza Sheria ya Mungu na ya kwamba amejipatia haki kwa njia ile. Baadaye akaanza kuitegemea haki ile. Hapo ni mwanzo wa makosa yake makuu.
c) Baadaye yakafuata makosa mengine. Alianza kujilinganisha na watu wengine, kama yule mtoza ushuru, akaona ya kuwa aliwashinda kwa wema na haki. Baadaye akasahau makosa yake na dhambi zake mwenyewe. Mwishowe hakutoa ungamo la dhambi, kwa maana hakuona la kuungama. Aliona makosa katika wengine tu. Katika maombi yake hakuomba kupewa mambo fulani. Alifikiri alikuwa nayo. Maombi yake ni kujisifu tu.

*2) Mtoza ushuru anakata tamaa juu ya nafsi yake.*

a) Mtoza ushuru si mtu mzuri. Kwa hiyo si vizuri kufanana naye katika mambo mengine mengine. Mwenendo wake ulikuwa mbaya kwa njia karibu zote. Kwa kawaida watoza ushuru walikuwa wezi na wadanganyifu.
b) Hakuangalia Sheria ya Mungu, wala maombi, wala ibada. Labda amesahau na kudharau kila jambo takatifu.
c) Lakini sasa yupo Hekaluni. Ni mwema sasa? Ni mwenye haki? La! Lakini dhamiri imempiga, na Sheria ya Mungu inaendelea kumpiga sana. Sasa anaona waziwazi dhambi zake. Anaona hana haki, ila hatia kubwa sana tu.
d) Katika shida yake kuu anaungama dhambi zake, na kwa ajili ya dhambi zake anaomba msaada na masamaha mbele ya uso wa Mungu.

*3) Haki ya kweli ni kipaji kinachotolewa na Mungu kwa ajili yake Yesu Kristo.*

a) Yesu ameitimiliza Sheria kwa ajili ya watu wote, mafarisayo na watoza ushuru, kwa maana wote wamekosa. **Rum 3:21–26; 5:18–19.**
b) Wanaojitegemea na kujipatia haki wenyewe wanajitenga na Mungu. **Gal 3:10–14.**
c) Wanaokata tamaa juu ya haki yao na kuungama dhambi na kuombamsaada kutoka kwa Mungu, basi wanapewa haki ya Yesu Kristo.**Flp 3:7–11.**
d) Kwa hiyo mtoza ushuru, anayeungama dhambi zake, anaweza *"kwenda nymbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule."* – Yesu anataka kila mmoja anayelisikiliza Neno lake leo awe mtoza ushuru namna hii, yaani anaye–ungama, na kupewa ondoleo la dhambi, na kurudi nyumbani, akiwa na haki ya YESU KRISTO.

# SIKU YA BWANA YA 12. BAADA YA UTATU

**(Mk 7:31–37)**

## EFATHA – NDIVYO BWANA YESU ANAVYOTUTENDEA KWA UPENDO

*1) Kutoka ushirika wetu tunapokaa peke yetu anatuongoza tupate kuingia katika ushirika wake na rafiki zake wengi.*

a) Yule kiziwi mwenye utasi hakusikia kitu, wala hakuweza kushirikiana na watu kwa njia ya mazungumzo. Kwa mwili tu alikaa katika ushirika wa watu. Mambo yote yalinyamaa kwake. Alishirikiana na nafsi yake mwenyewe tu katika mawazo yake.
b) Waliomwongoza huyu mtu kwa Yesu walimwondoa kutoka ushirika ule wa unyamavu, wakamwingiza katika ushirika ule wa Yesu. Upendo wa Yesu ulianza kumtendea mema.
c) Watu wanaweza kutuongoza, tufike karibu naye Yesu, lakini hawawezi kutupatia ushirika wa kweli naye. Hiyo ndiyo kazi yake mwenyewe.

*2) Yesu anatusaidia kujijua wenyewe, tuanze kutamani wokovu wetu.*

a) Kwa matendo yake Yesu alimwonyesha kiziwi ya kuwa shida yake ilikuwa kubwa sana. Ingawa mtu huyu amekwisha fika kwa Mwokozi, *anaanza kufahamu* shida na dhambi jinsi zilivyo kubwa!
b) Yesu alipomwonyesha shida na dhambi alimsaidia kiziwi kutamani zaidi na zaidi wokovu wake.
c) Ndivyo Yesu anavyotutendea sisi sote katika Kanisa lake, au anataka kututendea hivyo, ikiwa anapewa nafasi, kwa maana anatusaidia kufahamu dhambi zetu na kutubu (ndiyo kazi ya Sheria), tena anatuita na kutukaribisha kuipokea neema yake na wokovu wetu (ndiyo kazi ya Injili = Utume mwema).

*3) Yesu analifungua sikio la roho na kuulegeza ulimi wa moyo.*

a) *"Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikalegea, akasema vizuri."* Ndivyo Bwana Yesu alivyompatia mtu huyu kama uzima mpya kabisa, ndio uzima wa kweli, na uzima wa furaha kuu.
b) Matendo makuu ya Yesu Kristo, alipotuokoa sisi, yaani maisha yake, na kufa kwake, na ufufuko wake, ndilo neno la Efatha kwetu, yaani

anayafungua masikio yetu, tuyasikie maneno ya Uzima wa milele,

analegeza ndimi zetu, tuwe tayari kuomba na kushukuru na kusifu, kwa sehemu tu hapa duniani, lakini kwa njia kamili kati ya watakatifu wote mbinguni. **Ufu 7:13–17.**

# SIKU YA BWANA YA 13. BAADA YA UTATU

**(Lk 10:23–37)**

*Maelezo juu ya somo.*
Shida katika kuhubiri juu ya somo hili ni ya kwamba twaweza kuhubiri *kisheria* pasipo kujua ya kuwa tumefanya vibaya na kuongoza watu vibaya. Maana ya somo hili *si hii*: wengine wanafanya vibaya, lakini wewe angalia utende vizuri.
Tuangalie hapa mambo machache yanayoweza kutusaidia kulifahamu somo hili.
a) **Lk 10:22–23**: *"Nimekabidhiwa vyote na Baba."* – *"Heri macho yaonayo mnayoyaona ninyi."* Maneno haya yahusiana na mfano wa mistari **30–37**. Kama sisi bado kuufahamu uhusiano huu, basi mfano utakuwa somo la kisheria tu, linalosema: Fanya matendo mazuri kama huyu Msamaria!
b) Mara nyingi Yesu aliwashtaki viongozi wa watu ya kuwa ni viongozi wabaya na mifano mibaya. Lakini yeye mwenyewe ni mfano mzuri. **Yn 10.** Mara nyingi inaonekana ya kuwa anawaza juu ya **Eze mlango 34**. Tazama hasa **34:4**. Kila mmoja aliyeyasikia maneno yake Yesu alikumbuka maneno haya kutoka kitabu cha **Eze** na kufahamu ya kuwa aliwashtaki makuhani na wakuu wa watu.
c) Yesu aliitwa "Msamaria" kama neno la dharau. **Yn 8:48.** Huyu anayeitwa kwa jina la dharau, ndiye anayeshinda kabisa wakubwa wa watu na viongozi wa dini katika kufuata na kutimiza amri za sheria!
d) *"Mtunze huyu, na cho chote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."* Inaonekana ya kuwa mafundisho ya Yesu ndiyo haya: Mtunzaji wa juu wa watu katika shida zao, ndiye Yesu; sisi twatunza wenzetu kwa amri zake Yesu tu. Anayefuata amri za Yesu katika kuwatunza wenzake hataona ukosefu. Yesu hatakuwa na deni. Anawarudishia rafiki zake yote waliyoyatoa.

.– – – – –

Basi, kwa njia hii inaonekana ya kuwa Yesu mwenyewe ni mkubwa katika mfano huu. Watu wameshindwa, wakubwa kwa wadogo, katika matendo ya upendo. Yesu ndiye aliyempenda yule aliyepigwa. Yesu hapiti mtu ye yote, ingawa ni mtu maskini kabisa, au mwenye vidonda vibaya au mtu anayelala katika damu yake. Nasi tuhubiri hivi, kumtukuza Yesu, yule mwenye upendo, aliyeitwa "Msamaria".

## HURUMA NA WOKOVU

*1) Habari za mtu aliyekwenda Yeriko.*

a) Alipata hasara kubwa, hata akawa kama amekufa.
b) Waliokuwa na kazi ya kusaidia watu, walikosa wote, wakampita tu.
c) Aliokoka kwa ajili ya huruma ya MMOJA tu, asiyetaka kumpita njiani.
d) Wokovu wake uliwezekana kwa njia ya huruma tu.

*2) Habari zetu.*

a) Nasi tumepata hasara kubwa, kwa maana tumepigwa na maadui, yaani Shetani, na dhambi na mauti. Sisi tumekufa dhambini. **Efe 2:1.**
b) Watu, walio wakosaji na wenye dhambi wenyewe, hawawezi kutuokoa.
c) Anapatikana MMOJA, ambaye anatuhurumia kweli, ndiye aliyeitwa MSAMARIA na watu wale waliokataa kuokolewa naye. **Yn 8:48.**

*3) Wokovu na huruma katika maisha yetu.*

a) Tunao wokovu kwa ajili ya huruma yake Yesu Kristo tu.
b) Wokovu huo unazaa furaha ya kweli katika mioyo yetu.
c) Kwa ajili ya upendo wake Yesu anatuhurumia sisi, na katika furaha yetu kubwa tutahurumia wengine, kama Yesu alivyotuhurumia sisi. **Mt 10:8; 1 Yoh 4:7–11.**

# SIKU YA BWANA YA 14. BAADA YA UTATU

**(Lk 17:11–19)**

**KUMSHUKURU MUNGU**

*1) Ni kazi ya shida.*

a) Inaonekana kuna mazuio mengi. Lakini zuio lililo kuu limo katika moyo wa mtu mwenyewe. Kwa maana mtu aliye mgeni mbele yake Mungu hataki kujinyenyekeza na kumshukuru yeye.
b) Kama mtu anakubali moyoni kumshukuru Mungu, kuna mazuio mbalimbali, k m ugonjwa, mavuno mabaya, "bahati mbaya" katika biashara n k.
c) Mtu anapojitazama na kutazama watu wengine, anaona mara nyingi ya kuwa wamepewa mengi kuliko yeye, kwa hiyo anawaonea husuda.
d) Haya yote yanaonekana katika wale tisa wenye ukoma. Baada ya kupona walirudia maisha ya walimwengu, pasipo kumshukuru Yesu, kwa maana wakati wa ugonjwa wao wametamani maisha ya watu wazima ulimwenguni. Baada ya kupona labda walisema: "Kwa nini kushukuru? Si haki ya kila mtu kuwa na uzima wa mwili wake?"

*2) Ni kipaji cha neema.*

a) Wale tisa hawakufikiri hivyo. Hawakuona sababu yo yote kumrudia Yesu kumshukuru.
b) Ndivyo watu wengi sana walivyo! Katika shida wanalia sana, wakisema: "Nikipata nafuu kidogo tu, nitamshukuru Mungu sana sana." Au wanatoa ahadi nyingine nyingine. Wanapopona au kupokea msaada mwingine, wamesahau ahadi zote. Wanasema: "Hii ni haki yangu tu!"
c) Kwa yule mtu wa kumi ilikuwa kipaji cha neema kuweza kumshukuru Bwana Yesu. Labda wengine walimwambia: "Si lazima kushukuru, wengine hawafanyi hivyo." Lakini alishinda mazuio yote, akamwendea Yesu kumshukuru, akapewa baraka kubwa zaidi.
d) Alipomshukuru Yesu kwa ajili ya neema ile mpya alipewa baraka kubwa tena. Hiyo ndiyo sheria fulani katika ufalme wa Mungu: *"Kwa maana mwenye kitu (imani, shukrani n k) atapewa, naye asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa."* **Mk 4:25.**

*3) Ni njia ya kupewa baraka nyingi.*

a) Wale tisa walijinyima baraka nyingi kwa ajili ya kutokuwa na shukrani ya kweli. Hawakupewa wokovu wa roho zao.
b) Yule wa kumi alishukuru, akapewa hata ondoleo la dhambi zake na wokovu wa roho yake.
c) Ndivyo shukrani inavyofungua vijito vya uzima wa mbinguni.

*Application.* a) Shukrani imo kweli katika usharika wetu na katika mioyo ya Wakristo wa hapa? b) Kama Mungu ameyasikia maombi yako, na wewe kupewa msaada mkubwa katika shida zako, je, unafanya haraka kurudia wenzako katika ulimwengu huu, au unafanya haraka kupiga magoti mbele yake Mungu kumshukuru kwa neema yake? c) Labda unasema mara nyingi ya kuwa umepewa kidogo kuliko wengine, lakini ni uzito gani unaozuia vijito au mito ya furaha na baraka na neema kuingia moyoni mwako? Je, sababu kuu si ya kuwa umesahau kumshukuru Mungu, yeye anayetoa vipaji vyote na neema yote? Kwa maana wanaosahau kushukuru wanajinyima wenyewe baraka nyingi na vipaji vingi. Anayebarikiwa hasa ni yule anayekumbuka kumrudia Yesu kumshukuru.

# SIKU YA BWANA YA 15. BAADA YA UTATU

**(Mt 6:24–34)**

*Maelezo juu ya somo.*
Kwa maneno haya Yesu hataki kufurahisha ama kutegemeza watu walio wavivu ama wapurukushani. Yesu anakubali kabisa mafundisho mengine ya Biblia juu ya bidii kazini. **Mit 6:6–11.**
Lakini hapa Yesu anafundisha watu wanaojisumbua mno juu ya chakula na mahitaji mengine ya maisha. Anaona ya kuwa usumbufu huu ni ukosefu wa imani, kwa maana mtu wa imani anamtegemea Mungu katika kila jambo.

## MSISUMBUKIE MAISHA YENU

*1) Msingi wa imani hii ni kukaa katika ushirika naye Mungu.*

a) Ni lazima kuwa na Bwana mmoja tu. Haiwezekani kutumikia mabwana wawili (mst **24**).
b) Ni lazima kutumia kwa taratibu fulani vipaji vile vinavyotoka kwa Mungu. *"Maisha je! si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?"* (mst **25**).
c) Mtu anayeshirikiana na Mungu kwa imani ya kweli atatakaswa siku kwa siku (mst **33**).

*2) Faida ya imani hii ni ya kuwa masumbufu ya kila siku hayatakusumbua sana.*

a) Imani hii inaona waziwazi ya kuwa masumbufu hayana maana (mst **27**).
b) Imani hii inaona kazi ya Mungu katika viumbe vya ulimwengu kwa njia nyingi. Inaona ya kuwa kujisumbua mno ni kazi bure (mst **26–30**).
c) Imani inamtegemea Mungu kwa habari ya mahitaji. Kujisumbua mno ni kutokuamini (ukosefu wa imani). Kwa maana Mataifa, wasiomjua Mungu wa kweli, hawana imani, kwa hiyo wanajisumbua na mahitaji ya mwili hasa.

*3) Matokeo ya imani hii ni ya kuwa hata mengine yatatolewa kwake mwenye imani.*

a) Aliye na imani ya kweli anapewa ufunguo wa ghala kubwa ya Baba yetu: *"Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote."* (mst **32**). *"Hayo yote mtazidishiwa"* (mst **33**).
b) Maisha yote ya Mkristo yatakuwa na njia moja na nia moja: *"atashikamana na huyu"* (Mungu).
c) Utangoja siku zako moja moja kutoka mkono wa Mungu. *"Kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe"* (mst **34**).

*Application.* Ukitazama kwa njia hii masumbufu yako ya kila siku unaweza kufahamu kama unatumikia mabwana wawili, au kama ni mmoja tu, na huyu ni nani? Basi, umchague na kumtegemea yeye aliye na mamlaka kukulisha na kukuangalia katika mambo ya mwili na mambo ya roho, yote mawili.

# SIKU YA BWANA YA 16. BAADA YA UTATU

**(Lk 7:11–17)**

**BWANA YESU NA KUFA KWETU**

*1) Kufa kunatutembelea kila wakati hapa duniani.*

a) Neno la Mungu halizifichi habari za kufa, bali linatukumbusha mara nyingi ya kuwa tutakufa sote.
b) *"... hapo palikuwa na maiti anachukuliwa nje."* Ndivyo zilivyo habari za miji na vijiji karibu kila siku hapa kwetu.
c) Kama hii ni hali yetu, basi watu wanatafuta msaada gani? Ama wana-jaribu kusahau habari za kufa kwao, ama wanatafuta njia zitakazoweza kuongeza siku zao hapa duniani, ingawa ni kazi bure. **Mt 6:27; Lk 12:20.**

*2) Yesu ana mamlaka juu ya kufa.*

a) Somo letu linaonyesha ya kuwa Yesu ana mamlaka juu ya kufa.
b) Lakini Yesu hakuondoa kabisa kufa kwetu. Tutakufa sote. Yesu aliona watu wengi wakifa pasipo kuwafufua. Hata Lazaro na binti Yairo na mwana wa huyu mjane walikufa tena. Mara ile ya pili Yesu hakuwafufua.
c) Kwa nini Yesu aliwafufua wale watatu tu? Alitaka kuwaonyesha watu ya kuwa Masihi amekwisha fika na ya kuwa yeye alikuwa na mamlaka juu ya kifo. Kama alivyofufua wengine, yeye mwenyewe atafufuka baada ya kufa kwake msalabani.
d) Kwa hiyo, tendo la ajabu huko Naini si ahadi ya kuwa ataondoa kabisa mauti kutoka ushirika wa watu. Bali alitaka kuonyesha ya kuwa maneno yake yalikuwa kweli aliposema: *"Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima."* **Yn 11:25.**

*3) Kwa hiyo watu wanaoamini wanaweza kujipa moyo hata mbele ya mauti.*

a) Yesu ananena nasi leo, kama alivyonena huko Naini. Neno lake lina nguvu hata leo kama lilivyokuwa siku ile.
b) Hasemi: Hutakufa wewe, bali anasema: Ingawa utakufa mwili wako, mimi nitakufufua siku ya mwisho. **Yn 6:39–40.**
c) Kama wewe ni mzee, ama kijana, hakuna tofauti. Wote watakufa kwa njia ya mwili, kama Yesu anakawia kurudi. Anaporudi ataifufua miili yote, inayolala makaburini, na siku ile shauri kuu ni ya kuwa utawekwa upande gani. **Mt 25:33.** Yesu atabagua jinsi gani? Ataona kama watu wamekuwa na imani ama siyo, kama wamemfuata Yesu au kumdharau.
d) Kwa somo la leo Yesu anataka kuamsha imani katika mioyo yetu. Kama tunamwamini yeye, haina maana kuuogopa mauti. **Yn 11:40.** Kwa maana Yesu ameushinda ulimwengu (**Yn 16:33**), hata mauti. **1 Kor 15:55–57.**

# SIKU YA BWANA YA 17. BAADA YA UTATU

**(Lk 14:1–11)**

*Maelezo juu ya somo.*
a) Juu ya masomo yenye sehemu mbili zilizohitilafiana sana, taz juu, mlango IV.
b) Katika somo hili ni lazima kufahamu ya kuwa Yesu hafundishi adabu nzuri katika karamu za watu. Anafundisha tuwe na nia gani tunapokaribishwa kwenye karamu kuu ya ufalme wa mbinguni. Ili kutufundisha juu ya mambo yale anafanya mfano wa karamu ya watu.

## UKUBWA NA UDOGO KATIKA UFALME WA MBINGUNI

*1) "Lililotukuka kwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu."* **(Lk 16:15)**

a) Kama mtu anajifanyia ukubwa mbele yake Mungu kwa njia ya matendo mema tunauita ukubwa huo Ufarisayo (mst **7**). **Lk 18:11–12.**
b) Walionyamaza (mst **6**) katika karamu hii walifikiri ya kuwa waliishika Sheria vizuri kuliko Yesu (mst **3–6**).
c) Watu wanaofikiri ya kuwa ni wenye haki na kujitegemea (**Lk 18:9**) wanadhani ya kuwa wanastahili kiti cha mbele katika ufalme wa mbinguni (mst **7**).
d) Mawazo haya ni kukosa upendo. Sheria ilikubali kuokoa ng'ombe ama punda hata siku ya sabato (mst **5**), lakini watu walimkataza Yesu, asiponye mtu katika sabato (mst **2–4**).

*2) "Heri walio maskini wa roho".* **(Mt 5:3)**

a) Kama mtu anaona na kuungama ukosefu wake na dhambi zake, kwa matendo na nia na kila kitu, tunauita udogo na umaskini huo toba, kama katika mtoza ushuru. **Lk 18:13.**
b) Mtu namna hii, asiye na njia ya kujisifu, ni huyu *"mwenye ugonjwa wa safura"* (mst **2**). Hana kitu ambacho anaweza kukitegemea. Ana shida na ukosefu tu. Akifika kwa Yesu, labda alichukuliwa na wengine. Umaskini huo unamshurutisha kumpokea Yesu kwa imani.
c) Watu walioona umaskini wao wanafikiri hawastahili kitu. Wanajiweka mlangoni (ndani ya nyumba, lakini karibu na mlango), wakififikiri hawastahili nafasi iliyo nzuri. **Lk 18:13**: *"... alisimama mbali."* Na hapa: *"Nenda ukaketi mahali pa nyuma"*, maana yake: usifikiri wewe ya kuwa unastahili nafasi ya heshima!
d) Hapa kuna nafasi kwake Yesu kuponya aliye mgonjwa, ama kuondoa dhambi za mtu, ndiko kusema: *"Rafiki yangu, njoo huku mbele zaidi"* (mst **10**).

*Application.* Kama umejiweka juu (huzijui dhambi zako) kweli utadhiliwa. Kama unajiweka chini (yaani unaungama dhambi zako) kweli utakwezwa. Maisha yako yote kama Mkristo yawe kujidhili (kuungama dhambi na kuomba masamaha kila siku), nawe utakwezwa katika siku ya mwisho, Yesu atakaposema: *"Rafiki yangu, njoo huku mbele zaidi."* Ndio wokovu wa mbinguni.

# SIKU YA BWANA YA 18. BAADA YA UTATU

**(Mt 22:34–46)**

*Maelezo juu ya somo.*
Somo hili lina shida za pekee. a) Lina sehemu mbili zinazohitilafiana. Hapa hatuwezi kuhubiri sehemu moja na kuacha nyingine. Tungeweza kuihubiri sehemu ya pili na kuiacha ya kwanza pasipo hatari kubwa. Lakini tukiiacha ya pili na kuihubiri ya kwanza, tutaona shida kubwa na kuingia hatari kubwa. Kwa maana, b) katika sehemu ya kwanza Yesu anapatana nao Mafarisayo juu ya sheria ya kuwa inaagiza nini. Lakini sheria haiwezi kutuokoa. Mafundisho ya sehemu ya kwanza si mafundisho kamili ya Kikristo. Ni kama mwanzo tu. – Kwa hiyo ni lazima tujaribu sana kufahamu mambo yaliyomo katika somo hili.

## MAFARISAYO NA KRISTO

*1) Jinsi Mafarisayo wanavyofundisha juu ya Sheria.*

a) Mafarisayo walisema ya kuwa kila neno katika Agano la Kale ni takatifu. Yesu anakubali. **Mt 5:17.**
b) Mafarisayo walisema ya kuwa ni lazima mtu afanye bidii kuifuata Sheria na kutimiliza kila amri. Yesu anakubali. **Lk 10:25–29.**
c) Mafarisayo walitaka kujumlisha amri zote za Sheria katika amri moja au amri mbili fupi. Naye Yesu alifanya hivyo (mst **35–40**). **Mt 7:12.**
d) Mafarisayo walitaka kufikia haki ya kweli, kwa hiyo walifanyiza amri nyingine nyingine zilizokuwa za juu, ingawa hazikuagizwa na Mungu. Kuzitimiza amri hizi kutamletea mtu haki. Yesu haikubali njia hii, kwa maana watu walipojaribu njia ile walisahau, hata wakaacha amri zilizokuwamo katika Sheria. **Mt 23:3–7; 23:23–28.**
e) Katika somo la leo mazungumzo yao si juu ya amri za Mafarisayo wen–yewe, ni juu ya Sheria tu kama ilivyo katika Neno la Mungu. Yesu ana–jumlisha yote, na Mafarisayo wanakubali kabisa. **Mk 12:32–34.**

*2) Jinsi wanavyofundisha juu ya Kristo.*

a) Mafundisho juu ya Sheria hayatoshi kuokoa watu. Mafarisayo walitaka mazungumzo naye Yesu juu ya Sheria tu. Walimpima, kama alitosha katika mambo ya Sheria ama siyo. Kwa Mafarisayo Sheria inatosha kwa wokovu, maana yake, wanafikiri ya kuwa wanaweza kuitimiliza Sheria wenyewe. **Mt 19:20; Yn 7:49.**
b) Mafarisayo walipokomesha mazungumzo juu ya Sheria, Yesu alianza kuuliza juu ya Kristo. Alitaka kuwaonyesha ya kuwa Sheria haitoshi kwa wokovu, bali anahitajiwa Masihi (Kristo).

c) Kwa Mafarisayo Masihi ni mfalme wa Kisheria, tena atakuwa mkubwa kama Daudi, kwa maana ni wa ukoo wake (mst **42**). Kristo atawapa utukufu ule walioustahili.
d) Hapa Yesu hakukubali. Alifundisha ya kuwa Masihi ni Mwana wa Mungu, kwa maana hata Daudi alimwita 'Bwana'.
e) Aliye Mwana wa Mungu, ndiye mkubwa kuliko watu. Ndiye anayeweza kuwapa haki yake, wanaposhindwa kujipatia haki wenyewe kwa njia ya Sheria. **Gal 4:4.**

*Application.* a) Kama unafanya bidii kujipatia haki ya Sheria, unaendelea katika njia ya Mafarisayo tu. Hakuna wokovu katika njia ile. b) Kama umemtambua Masihi (Kristo) kama mkubwa kuliko Mafarisayo na Daudi, umemwona yule anayeweza kuitimiliza Sheria, yeye peke yake. **Mt 5:17; Ebr 9:26; 10:10.** c) Kumwamini huyu na kujiweka mikononi mwake, ndio wokovu. d) Sheria uliyoshughulika nayo ni Kiongozi kwake Kristo. Haiwezi kukuokoa. Lakini unapokaa katika imani, Sheria itaendelea kukuongoza kwa Kristo na kukufundisha juu ya mapenzi yake. Mkristo anahitaji Sheria na Injili, zote mbili. Hawezi kuokoka kwa Sheria tu, lakini hata akiokolewa kwa neema (Injili ni habari za neema) ni lazima Sheria iendelee kumfundisha ya kuwa yeye ni mwenye dhambi anayehitaji kwenda kwa Kristo kila siku ili kuipokea neema yake.

# SIKU YA BWANA YA 19. BAADA YA UTATU

**(Mt 9:1–8)**

## MAMBO YANAYOIZUIA KAZI YA YESU

*1) Kuna mambo mengi namna hii.*

a) Mtu huyu alishindwa na ugonjwa wake. Hakuweza kutembea mwenyewe kumwendea Mwokozi.
b) Mtu huyu alishindwa tangu zamani kwa ajili ya mawazo yake. Mawazo yake yote yaliuzunguka ugonjwa wake, na waganga, na dawa, na njia nyingine za kupona.
c) Mgonjwa anaweza kuizunguka–zunguka nafsi yake. Pengine hakumbuki shida za wengine.
d) Ndivyo tulivyo sisi sote katika nafsi zetu. Tunafikiria shida zetu na mambo yetu. Tumefungwa ndani ya mioyo yetu. Ingawa tunatembea–tembea na kuonekana kama watu wazima, tumefungwa na ugonjwa huo wa kupooza katika roho zetu. Ni lazima tuchukuliwe kwake Yesu, kwa sababu hatuwezi kwenda sisi wenyewe.
e) Kama watu wa jamaa zetu ama rafiki hawafahamu shida zetu, labda hatufiki kwake Yesu. Wanaweza kutubeba kwa mikono yao (tukiwa watoto wadogo) ama kwa maneno yao (ushuhuda wa Kikristo) ama kwa maombi. Lakini kama hakuna Wakristo namna hii karibu nasi, labda tutazuiwa siku nyingi kumjua Kristo na kufika kwake.

*2) Mazuio haya yanaweza kuondolewa.*

a) Hiyo ndiyo Injili nzuri sana leo.
b) Labda yule mtu aliwaomba sana wenzake kumchukua kwa Kristo. Labda walikataa siku nyingi, lakini kwa ajili ya maombi yake walikubali.
c) Kama mtu mwenyewe anakataa kupokea msaada, tunaweza kumshinda kwa maombi. Si kwa kumwomba yeye, lakini kwa kumwomba Mungu. Kama Neno la Mungu linatumiwa nyumbani, na watu wa nyumba ile kuomba nyumbani na kwenda kanisani, mazuio mengi yataondolewa: anayehitaji Mwokozi atachukuliwa kwake Kristo.
d) Hatuna mamlaka sisi kuondoa yale mazuio katika moyo wa mtu. Ni Kristo tu. Anafanya kazi ile kwa Neno lake (mst **2**) na kwa Roho yake. Watu wanaweza kusaidia watu wengine kufika karibu naye Yesu.
e) Kama Yesu ataanza kusamehe dhambi (mst **2**) na kuendelea kumponya mtu kwa kweli (mst **6–7**) au kufuata taratibu ya kinyume ni tofauti. Pengine mtu anaanza kuziona dhambi zake kuu, kama Mungu anamponya mwili. Pengine tunasamehewa dhambi, na mwili dhaifu utaendelea kutusumbua. **2 Kor 12:9.** Ni lazima Mkristo mnyenyekevu awe tayari kuchukua masumbufu na mateso namna hii. Auchukue mzigo huo kama njia moja ya kumsifu Mungu.

*Application.* a) Ama ukitaka mwenyewe, ama wengine wakikuongoza, ni lazima ufike kwa Yesu. b) Kuna mazuio mengi ambayo ni lazima yaondolewe. Lililo kuu ni mapenzi yako ya kinyume moyoni. c) Msaada ulio mkuu wa kukuongoza kwa Yesu ni Neno na maombi, yako na ya wenzako wanaokuombea. d) Jambo kubwa ni kuponywa mwili, lakini lililo kuu kabisa ni kuondolewa dhambi zako. e) Yuko hapa hata sasa aliye na nguvu kusema: *"Jipe moyo mkuu, mwanangu; umesamehewa dhambi zako."*

* * * * * * *

# SIKU YA BWANA YA 20. BAADA YA UTATU

**(Mt 22:1–14)**

**ARUSI YA MBINGUNI**

*1) Wengi wameitwa.*

a) Walioalikwa kwanza, ndio Waisraeli, watu wa pekee wa Mungu (wateule).
b) Watu wa ulimwengu mzima wameitwa. **Mt 28:19.**
c) Walipokataa wengine, Mungu ameendelea kuita wengine tena.

*2) Wengine wamekataa kuupokea ule wito kutoka kwa Mungu.*

a) Wameshindwa kwa ajili ya mambo ya ulimwengu, kama mashamba, na ng'ombe, na biashara, na ndoa.
b) Wamefuata mifano ya wengine. Mmoja akikataa, mwingine anaufuata mfano wake mbaya.
c) Wote wanaokataa wanaonyesha ugumu wa mioyo yao.

*3) Mfalme ameendelea kuita.*

a) Ameita wa kwanza mara nyingi.
b) Anaendelea kuita wengine, na wengine tena.
c) Kwa sababu chumba cha karamu hakina budi kujaa.

*4) Ingawa anaita watu wo wote, yanatakiwa mavazi ya arusi.*
**(Ufu 3:5,18)**

a) Hata mavazi ni zawadi ya mfalme.
b) Mavazi yanayofaa mbinguni, ndiyo haki ya Yesu Kristo.

# SIKU YA BWANA YA 21. BAADA YA UTATU

**(Yn 4:46–53)**

*Maelezo juu ya somo.*
Jambo lililo kuu hapa ni imani imara ya diwani. Aliamini hata Yesu alipoonekana ya kwamba atamfukuza (mst **48**). Kuna masomo mengi kidogo yanayoonyesha imani imara namna hii, hata katika watu wa mataifa. **Mt 8:5–13; 9:20–22; 15:21–28.** Lakini somo hili ni la aina ya pekee, kwa jinsi inavyoonyesha hata hatua za imani imara. Linaonyesha jinsi imani inavyoanza katika shida na hatari, jinsi inavyoondoa mazuio na kujipa moyo, na jinsi inavyoshuhudia Mwokozi.

## JINSI IMANI YA KWELI INAVYOZALIWA NA KUENDELEA

*Dibaji.* Kuna neno moja, **Kol 2:7**, linaloonyesha kama hatua tatu za kuamini kwetu, yaani *"wenye shina katika yeye"*, na *"kujengwa katika yeye"*, na *"kufanywa imara kwa imani"*. Na wanaoamini kwa njia hii, kweli watazidi kutoa shukrani. Hatua hizi zinaonekana vizuri katika somo la leo. Tunaweza kujifunza njia ya kuamini kweli katika diwani huyu.

*1) Jinsi inavyozaliwa.*

a) Pengine hatujui mwanzo wake. Hatujui diwani alianza lini kupata habari za Yesu au kuamini ya kwamba Yesu ana nguvu.
b) Katika Wakristo walio karibu nasi hatujui imani ilianza siku gani. Mwanzo umefichiwa macho yetu.
c) Lakini hakuna mwanzo wa imani pasipo Neno la Mungu, wala hakuna mwanzo pasipo kazi ya Roho Mtakatifu.
d) Huyu diwani aliponena na Yesu *"akamsihi ashuke na kumponya mwanawe; kwa maana alikuwa kufani."* Hapa imani ya kwanza ipo. Neno na Roho wamefanya kazi fulani katika moyo huu. Neno la Mungu limeingia katika moyo wake. Imani ina *"shina katika yeye"* (Yesu).
e) Shina hili halina nguvu. Imani hii inaweza kuondolewa upesi. Kama imani itakuwa imara, ni lazima ipimwe na kuongezewa nguvu.

*2) Jinsi inavyojengwa.*

a) Labda tumeona Wakristo wapya, jinsi walivyokuwa dhaifu. Maneno makali machache kutoka wenzao yangaliweza kuwaondoa kutoka njia ya Kikristo. Je, ni vizuri kuwaangalia kabisa, wasiingie katika shida zo zote? La, wangewezaje kupata nguvu na kujengwa?
b) Diwani alionekana ana imani, lakini Yesu alitaka kuimarisha shina lake na kuijenga imani yake zaidi. Yesu alimwambia kwa ukali: *"Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa?"* Maneno haya ni kushtaki watu wote wasioamini siku nyingine, yaani wanaamini katika siku za shida tu, na wanapoona matendo ya ajabu.

c) Diwani alizidi kumsihi Yesu (mst **49**). Shina la imani likaenda chini zaidi moyoni mwake. Imani yake si ya midomo tu, ni jambo la moyo. Imekwisha pimwa.
d) Yesu alikubali maombi yake. Diwani aliona ya kuwa imani ni njia salama ya kumtegemea Yesu. Basi, akajengwa, akaimarishwa zaidi katika imani yake.

*3) Jinsi inavyoendelea kuwa imara.*

a) Alipomwacha Yesu hakujua neno juu ya hali ya mtoto. Alikuwa na ahadi ya Yesu tu (mst **50**). Akaenda nalo neno lile tu. Ni imani safi na ya kweli. **Yn 20:29.**
b) Alipokwenda nyumbani, alipokea habari ya kuwa mwana wake amepona. Ndipo alipokazwa zaidi katika imani yake. *"Akaamini yeye"* (mst **53**).
c) Kwa ajili ya imani yake na matokeo ya imani yake (pasipo imani yake asingaliweza kuipokea neema ile kuu ya Yesu), alitoa ushuhuda mzuri mbele ya watu wote wa jamaa yake, wakaamini hata wao (mst **53**).
d) Ndivyo shina la kwanza (kuamini ya kuwa "labda Yesu anaweza kunisaidia katika shida yangu") linavyoenda chini na kukua na kuleta matunda. Haya ndiyo kazi ya Neno. **Rum 10:8.**
e) Matunda mengine ni shukrani kuu. **Kol 2:7.**

# SIKU YA BWANA YA 22. BAADA YA UTATU

**(Mt 18:21–35)**

## KUHESABU KWA NJIA YA WATU AU KWA NJIA YA MUNGU

*1) Kuhesabu kwa njia ya watu.*

a) Watu huhesabu kwa njia ya ajabu. Wakishindwa katika biashara fulani wanafikiri: Nikipata msaada leo, nitafaulu kesho ama mwaka ujao. Basi, wanakopa pesa. Wakishindwa tena, wanakopa tena. Ndivyo mtu huyu alivyofanya deni la Sh 50 000 000!
b) Hata baada ya kufanya deni kubwa mtu ni mpurukushani kabisa. Anasema: *"Nipe wakati fulani tu. Nitalipa."* Je, mtumishi huyu anaweza kurudisha Sh 50 000 000? Akiweka akiba Sh 1000/– kila mwaka, kwa kusudi la kulipa deni, itachukua muda wa miaka 50 000 kulipa yote! (Ikiwa tunahesabu ya kuwa alipe "interest", itachukua muda wa miaka mingi zaidi!) Basi atahitaji kuishi, kuzaliwa na kufa, mara 1 000 hapa duniani ili kuweza kulipa yote!
c) Kweli mtu ni wa ajabu. Inatokea ya kuwa deni lote linafutwa kabisa, si kwa njia ya kulipwa, bali kwa neema na upendo wa bwana tu. Anafanya nini sasa? Je, anasema: Sasa mimi ni mtu mpya, nimshukuru bwana wangu, nimtumikie yeye na watu wengine kwa furaha siku zangu zote? La, anapofika darajani tu anamkamata mwenzake kwa ajili ya deni la Sh 75/–, hana huruma yo yote. – Ndivyo tulivyo sisi watu. Ndivyo ilivyo akili ya hesabu mioyoni mwetu.

*2) Kehesabu kwa njia ya Mungu.*

a) Sasa tungefikiri juu yake Mungu ya kuwa anafuta madeni tu, akisema "si kitu"! Lakini si hivyo. Mungu anahesabu kwa njia yake ya pekee, si kwa kufuata mawazo yetu.
b) Hata katika kufuta madeni Mungu ni *"Mungu wa taratibu (amani), si wa machafuko"*. **1 Kor 14:33.** Deni la watu wote tangu mwanzo (**Mwa 3**) halikuweza kutoroka tu. Ilikuwa lazima lilipwe. Kama Mungu angalilifuta tu na kusema haliko, machafuko makubwa zaidi yangalitokea. Kwa hiyo maandiko yashuhudia: Mungu aliliweka juu yake mwenyewe, alilipe. Njia ya kulilipa ni Yesu Kristo. Anajua ukubwa wa deni hili. Kwa hiyo anataja jumla ile kubwa, kwa maana hakuna mtu duniani anayeweza kulilipa deni la dhambi.
c) Mungu anapofuta deni kubwa anasema: nawe ufanye vile vile kwa habari ya mwenzako aliye na makosa. Si kama sharti: "Kama wewe unaonyesha upendo mzuri, nami nitakufanyia upendo mzuri." La, Mungu anatangulia kabisa, nasi tufuate kwa shukrani mfano wake. **1 Yoh 4:19.**

*3) Kwa hiyo, jinsi anavyohesabu Mungu, tuhesabu nasi.*

a) Ndiyo njia ya kushukuru. Yule mtumishi angaliweza kushukuru huko darajani, kwa kumfanyia huruma mwenzake.
b) Yote tuliyo nayo ni zawadi kutoka kwa Mungu. **Mt 10:8.** Kwa hiyo tutoe zawadi kwa wenzetu, yaani maneno na matendo ya huruma na upendo.
c) Kuishi kwa njia hii ni ushuhuda ya kuwa Mungu ni hai na ya kuwa anatenda kazi yake kati yetu. **Yn 5:17; Flp 2:13.**

# SIKU YA BWANA YA 23. BAADA YA UTATU

**(Mt 22:15–22)**

## KUWA MWANANCHI KATIKA NCHI MBILI

*1) Kama wananchi wa ufalme wa Mungu imetupasa kumtii kabisa.*

a) Somo letu la leo linajibu swali la Wakristo wengi katika nyakati zote: Je, imetupasa kutii wakubwa wa dunia hii kadiri gani? Katika somo letu waliouliza swali hili walijaribu kumtega Yesu, lakini yeye alijibu kwa njia inayofaa watu wa nyakati zote.
b) Imetupasa kumtii Mungu kabisa, kwa sababu yeye ni Muumba wetu. Je, mtu ana kitu gani ambacho ni chake kabisa? Hana. Vyote ni vipaji.
c) Zaidi ya kutuumba Mungu ametufanya wananchi kwa Ubatizo. **Yn 3:3–5.**
d) Walio wananchi wa nchi fulani imewapasa kuzitii sheria za nchi ile.
e) Hatujui sheria ya ufalme wa Mungu isipokuwa kwa Neno lake takatifu. Kumpa Mungu yaliyo yake, ndiko kutembea katika nuru ya Neno lake. **Zab 119:105; Isa 49:6.**

*2) Kama wananchi wa nchi fulani hapa duniani imetupasa kuzitii sheria za nchi yetu.*

a) *Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari."* Walio wakubwa wetu wamewekwa chini ya sheria ya nchi. Tusipowatii tutaharibu kazi yote ya sheria, na nchi itabomoka.
b) Haya si kusema ya kuwa Mungu hana shauri na Kaisari. *"Hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu."* **Rum 13:1–7.** Mungu anautawala ulimwengu huu kwa njia ya mamlaka ya sheria na wafalme na maliwali na wakubwa wengine. Mungu anaangalia hata mataifa wasio Wakristo kwa njia hiyo.
c) Haina maana Mkristo akisema: *"Ni ya ulimwengu tu, si ya kiroho."* Yaani ulinzi wote na taratibu ya sheria ni vipaji kutoka Baba yetu wa mbinguni. **1 Pet 2:13–17.**
d) Kwa hiyo ni lazima Mkristo awe mwaminifu hata katika mambo ya ulimwengu (kazi, pesa, taratibu, kodi, vyeti vya baisikeli na redio n k). Tukishindwa katika mambo haya madogo, je, tutafaulu katika makubwa ya ufalme wa Mungu? **Lk 16:10–12.**

*3) Kama wananchi katika nchi mbili, ni lazima tugawie kila mfalme yaliyo yake.*

a) Ni vibaya kukataa kumpa Kaisari yaliyo yake, kwa maana ni kukana ya kuwa Mungu ni mtawala wa juu, yaani Muumba wa yote.
b) Ni vibaya kukataa kumpa Mungu yaliyo yake, kwa maana ni kuukubali ulimwengu huu tu.
c) Kwa hiyo ni taratibu ya Kikristo kumlipa Kaisari yaliyo ya Kaisari na kumpa Mungu yaliyo ya Mungu.
d) Mkristo anayefuata sheria hii ndiye atakayekuwa raia mwema.

Lakini kuna shida fulani.
i) Ikiwa wakubwa wa nchi hii watakosea sheria ya Mungu, yaani kukosea Neno la Mungu kwa njia iliyo wazi, ni lazima Mkristo amtii Mungu kwanza. **Mdo 5:29.**
ii) Tena ni lazima kwa ajili ya Neno la Mungu na dhamiri kumtii Mungu kuliko wanadamu. Kama Mkristo atapigwa kwa ajili ya hayo, ni vizuri aipokee adhabu yake kwa furaha. **Mdo 7:60; 25:6–12; 1 Pet 2:18–21.**
Sheria iliyo kuu kwa Mkristo: Kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake. **Mt 6:33.** Ndipo yote yatakapokuwa sawa.

# SIKU YA BWANA YA 24. BAADA YA UTATU

## (Mt 9:18–26)

### UGONJWA, MAUTI, NA IMANI

*1) Ugonjwa na mauti ni wageni wanaotutembelea mara nyingi.*

a) Si lazima kulisoma Biblia kupata habari za magonjwa na kifo. Kuna habari nyingi katika vijiji vyetu.
b) Tunapata msaada gani katika shida hizi zote? Watu wa kawaida hufikiria waganga na dawa na hospitali.
c) Watu wenyewe hujaribu kutusaidia ama kutufariji. Wanatoa hasa maneno mengi, k m: "Utapona bila shaka." "Jaribu kusahau shida zako. Fikiri mambo ya furaha tu." Ndiyo maneno ya midomo na faraja iliyo karibu bure.
d) Neno la Mungu linatoa habari za magonjwa mengi na habari nyingi za kifo. Lakini hakuna faraja iliyo maneno–maneno tu. Yesu alifukuza watu wale waliofariji vibaya au kuongeza huzuni tu (mst **24**). Hapendezwi na michezo namna ile. Haileti msaada.

*2) Hata ugonjwa na mauti zinaleta utume fulani kwetu.*

a) Yesu alipofukuza wale waliopiga filimbi na waliofanya maombolezo alifanya hivi ili kuanza kutenda mwenyewe.
b) Pengine inaonekana hataki kutenda lo lote, au anachelewa sana. **Mk 7:27; Yn 11:6; 11:21.** Ni vizuri ya kuwa hasaidii mara moja kila wakati, kwa maana tungeacha kusumbukia faida yetu ya kweli, tena tungeacha kuomba. **Ebr 12:7.**
c) Yesu alichelewa ili apate kuonyesha utukufu wake zaidi. Yesu aliingia nyumbani wakati mauti ilipokuwapo.
d) Anaweza kukawia (si kuchelewa kweli, kwa maana anajua wakati unaofaa) kutusaidia nasi. Ni kwa sababu mbili hasa: Anataka kutufundisha jambo fulani linalofahamika katika shida tu. – Hatufufui sisi ama watu wa kwetu, kwa maana ameweka ushuhuda wa kutosha katika Neno lake (**Mt 9; Lk 7; Yn 11**) na katika ufufuko wake, lakini atatufufua sote siku ya mwisho.
e) Ni moyo mnyenyekevu tu unaoweza kupokea ugonjwa na kifo kama utume kutoka kwa Mungu. **Rum 8:38; 1 Kor 3:22; 2 Kor 4:7–18; Flp 1:20–26.**

*3) Katika shida zote za ugonjwa na kifo iko njia ya imani.*

a) Si njia nyepesi. Pengine inaonekana ni njia iliyo ngumu kuliko nyingine.
b) Kama iko njia ya imani, si kwa ajili ya nguvu ya imani. Ni kwa ajili ya uwezo wa Neno lake Yesu: *"Jipe moyo mkuu"* (mst **22**) ama *"Mimi sikukuambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?"* **Yn 11:40.**

c) Msaada wake Yesu ni mkubwa kweli. Lakini tena ni kielelezo cha msaada wake huko ng'ambo ya kifo na kaburi ya kuwa atashinda magonjwa yote na kifo kabisa. **Ufu 21:1–4.**

*Application.* a) Kama umeona sasa ya kuwa umelia mara nyingi katika ugonjwa na katika kufiwa na wapendwa, labda unaona ya kuwa umetafuta msaada wa nje tu kutoka kwake Yesu. b) Sasa uanze kuomba msaada wake ulio mkuu, yaani kukufundisha uwe tayari kwa uzima wa milele katika ufalme wake. Kama ni uzima ama kifo hapa duniani, si jambo kubwa. Jambo lililo kuu ni kuruzukiwa *"kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo."* **2 Pet 1:11.**

# SIKU YA BWANA YA 25. BAADA YA UTATU

**(Mt 24:15-28)**

*Maelezo juu ya somo.*
Kwa ajili ya maneno yake Yesu juu ya anguko la hekalu (**Mt 24:1-2**) wanafunzi wake wamemwuliza habari za matokeo yale. Katika mlango wa **24** anaeleza mambo haya, tena anaeleza habari za wakati wa mwisho, atakaporudi kwa utukufu. Shida ya mlango huo ni ya kuwa ni vigumu kidogo kujua habari za Yerusalemu zinakoma wapi, na habari za kurudi kwake zinaanza wapi. Yesu ameweka pamoja habari hizi zote kwa sababu tatu:
a) Anguko la Yerusalemu na wakati wa mwisho zitafanana, kwa sababu zitakuwa nyakati za dhiki kubwa (mst **8,21**).
b) Anayejifunza habari za Yerusalemu na kuzikumbuka, ataangalia vema kurudi kwake Yesu.
c) Yesu hatoi habari kamili za wakati (mst **6,14,33,36**), lakini anatuonya sana (mst **13,15,25,42**).
Kwa ajili ya haya yote ni lazima kuhubiri kwa uangalifu sana somo hili, tusiseme mambo ambayo hatuyajui, ila tunayafikiri au kuyabahatisha tu. Tena ni lazima tulinganishe somo hili na masomo mengine ili kupata mafundisho ya Biblia. Lakini tukaze neno hili sana: *"Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu"* (mst **42**).

## SHIDA ZA MWISHO

*1) Anguko la Yerusalemu ni mfano wa shida zile.*

a) Lilileta shida na taabu nyingi.
b) Watu walikuwa wameonywa naye Yesu juu ya jambo hilo, lakini hawakumsikiliza.
c) Wengi wameongozwa na viongozi wabaya, wakaanguka na kupotea.

*2) Shida zitakuwa kubwa zaidi, Yesu atakaporudi kwa hukumu ya mwisho.*

a) Neno la Mungu lasema hivyo. Kama Neno la Mungu lilisema kweli juu ya anguko la Yerusalemu, lasema kweli hata juu ya shida za mwisho.
b) Machafuko yatakuwa makubwa, watu waende huko na huko kutafuta ama mali zao, ama wenzao, ama msaada.
c) Machafuko yatakuwa makubwa zaidi katika mambo ya dini kwa ajili ya viongozi wabaya na Wakristo wa uongo. Wengine watasema hata maneno haya ya ajabu: *"Mimi ni Kristo"* (mst **24**).
d) Wengi watadanganywa na kuanguka, wapotee.

*3) Ni lazima kuzijua alama za wakati Kristo atakaporudi.*

a) Tusipojua tungeweza kushikwa na ghafula.
b) Tusipojua tungeweza kuongozwa vibaya na kupotea milele.
c) Neno la Mungu ni kiongozi kizuri, kwa maana linatueleza kila jambo linalotakiwa, tena linatuonyesha kila hatari.
d) Neno la Mungu linatuonyesha njia ya wokovu.

*Application.*
a) Yesu ameonyesha mpaka sasa ya kuwa amesema kweli: Hekalu la Yerusalemu lilianguka kabisa (Mwaka 70 A D) baada ya dhiki kubwa kwa watu waliokaa huko. b) Anakuonyesha wewe njia ya wokovu katika Kanisa ambalo halitaanguka. c) Kusikia na kuamini ndiyo njia ya wokovu. Kwa hiyo Yesu anakuuliza leo: *"Atakapokuja Mwana wa Adamu, je! ataiona imani duniani?"* **Lk 18:8.**

# SIKU YA BWANA YA MWISHO KABLA YA MAJILIO

**(Mt 25:31–46)**

*Maelezo juu ya somo.*
Somo hili linaleta hatari ya pekee. Tukilisoma somo hili tu tungeweza kufikiri ya kuwa watu wataokoka kwa ajili ya matendo yao mema, na ya kuwa watakaopotea watapotea kwa sababu wameshindwa kufanya matendo mema ya kutosha. Lakini kulisoma na kulihubiri hivi kungekuwa ajabu sana, kwa maana mafundisho namna hii hayamo katika Agano Jipya, hata mstari mmoja. Kwa hiyo ni lazima kulisoma tena somo hili na kulifahamu kwa njia inayopatana na mafunzo mengine ya Agano Jipya. Yanayofuata hapa chini ni njia moja namna hii.

## SIKU YA HUKUMU YA MWISHO

*1) Siku ile watu watakusanywa.*

a) Mungu ameumba watu wote, kwa hiyo yeye ni Bwana wa watu wote na wa matendo yao.
b) Mungu ametengeneza wokovu wa watu wote. Ni haki ya kuwa yeye apime, wamefanya nini nao, wokovu huo, wameupokea au kuukataa.
c) Mungu ametangaza katika Injili yake ya kuwa anataka kuwaokoa watu wote. **Mt 28:19; Yn 3:16.** Kwa hiyo

*2) Watu watatengwa.*

a) Atawabagua kama vile mchungaji awabaguavyo kondoo na mbuzi.
b) Baada ya kuwatenga watu katika makundi mawili, mfalme atawaonyesha matendo yao, kama tunavyoainisha matunda mazuri ya miti mizuri, na matunda mabaya ya miti mibaya, yaani tukiona matunda, twaweza kuijua hali ya miti iliyozaa matunda haya.
c) Mfalme atawaweka katika makundi mawili, kabla ya kuonyesha matendo yao. Kundi moja linaitwa *'mliobarikiwa na Baba yangu'*, moja linaitwa *'mliolaaniwa'*. Wengine walipata kuwa *'waliobarikiwa'* walipoupokea wokovu katika jina lake Yesu. Wengine walipata kuwa *'waliolaaniwa'*, walipoukataa wokovu katika jina la Yesu.

*3) Kwa nini hawajui matendo yao mema ama matendo yao mabaya?*

a) Wasiojua matendo yao mema wanajua vizuri ya kuwa *matendo yao wenyewe ni mabaya tu*. Lakini Yesu anatazama *haki yake na matendo yake mazuri* katika wale waliookoka. Ndiko kumvaa Bwana Yesu Kristo. **Rum 13:14**.
b) Wasiojua matendo yao mabaya *wanafikiri* ya kuwa matendo yao ni mazuri. Lakini Yesu anaona uchi wao (**Mt 22:12**), yaani hawakuvaa haki yake.
c) Basi, shauri la kukubaliwa au kutupwa katika hukumu ya mwisho ni hilo: tumefanya nini na wokovu ule unaopatikana katika Yesu Kristo?

*Application.* Je, wewe umevaa matendo mema ya Kristo, uweze kukubaliwa naye siku ya mwisho, au utaonekana kwa uchi siku ile?

# SIKUKUU YA MIKAELI MTAKATIFU
**(Mwisho wa Septemba ama mwanzo wa Oktoba)**

**(Mt 18:1–10)**

*Maelezo juu ya sikukuu hii na somo hili.*
Sikukuu hii ni sikukuu ya kukumbuka malaika na kazi yao kama watumishi wa Mungu na kazi yao ya kutulinda hatarini. Kwa ajili ya neno lake Yesu (mst **10**) juu ya malaika na "wadogo" sikukuu hii ni sikukuu ya watoto pia. Wengine wamefahamu maneno haya kwa njia mbaya, yaani wamefikiri ya kuwa watoto ni wema na watakatifu kama malaika. Yesu anaposema ya kuwa watu wazima wawe kama watoto, ili waweze kuingia ufalme wa mbinguni (mst **3**), wengi wameyaeleza maneno haya kwa njia mbaya: wanasema ya kuwa watoto hawana makosa wala dhambi, na kwa hiyo wanaweza kuingia. Lakini siyo mafundisho ya Biblia! Bali Biblia inatufundisha ya kuwa sisi sote ni chini ya hukumu. Watoto wanaona na kuziungama shida zao, wako tayari kupokea msaada na kumtegemea Msaidizi, bali watu wazima wana kiburi, wanajitegemea. Hapo, Yesu anasema, watu wazima wajinyenyekeze, wawe kama watoto, maana yake: waukubali ubaya wao na kuwa tayari kumpokea Mwokozi.

## UKUBWA NA UDOGO KATIKA UFALME WA MBINGUNI

*1) Sisi wenyewe hatuna ukubwa.*

a) Tangu anguko la watu, wote wanazaliwa wenye dhambi na chini ya hukumu ya Mungu. **Zab 51:5; Rum 3:23.**
b) Hatuwezi kujipatia ukubwa sisi wenyewe. **Mt 12:34; 7:11; Rum 7:15–21.**
c) Ingawa Yesu anasema ya kuwa sisi tugeuke, tuwe kama watoto (wadogo), maana yake *si* ya kuwa sisi tungeweza kufanya mema au kujipatia hali ya utoto.

*2) Sisi wenyewe tuna ukosefu na udhaifu.*

a) Ndivyo ilivyo kabisa. Tuna makosa mengi, hatustahili kuitwa watoto wa Baba yetu, kwa maana tumemkosea. **Lk 15:18–19,21.**
b) Iko tofauti kubwa sana baina ya watu: wengine wanauona ukosefu wao na kuungama. Wengine, kwa ajili ya 'ukubwa' wao na kiburi chao, wanakana ukosefu na udhaifu wao, bali wanajisifu kwa ajili ya ule 'ukubwa' ambao hauko! **Yoh 9:41.**
c) Kosa lililo kuu si dhambi hii ama hii, bali kosa lililo kuu linalozuia wokovu, ni kiburi cha mioyo ya watu. Wanajitoshea, wanafikiri ya kuwa wanaweza yote wenyewe. **Mit 16:18; Zab 73:3–12; Mt 20:22; Ufu 3:17.**
d) Hapa watoto wanahitilafiana na watu 'wakubwa'. Labda watoto wanaweza kujiweka kama 'wakubwa' ama 'wafalme' ama 'majemadari', lakini ni katika michezo yao tu! Kwa kweli wanaujua udogo wao na kuungama.

*3) Ni lazima kuuacha ukubwa wetu na kuurudia udogo wetu wa kweli.*

a) Mtoto anaungama kabisa ya kuwa hawezi kushinda mwenyewe, isipokuwa anaweza kulia katika shida zake. Ni tayari kupokea msaada kutoka mtu ye yote aliye karibu, tena anayemhurumia. Hiyo ndiyo faida ya kuwa mtoto, ambayo Yesu anaieleza katika somo (mst **2–4**).
b) Wale wanaojidhania kuwa wakubwa, ni lazima walione kosa lao katika jambo hili. Ndiko kubadili mawazo na nia. Ndiko kunyenyekea, kutubu na kugeuka.
c) Wakitaka kuibadili nia yao kwa njia hii, itakuwa lazima kuyaacha mambo yale ambayo wameyategemea zamani au kuyapenda kupita kiasi. Kuuacha upendo wa utajiri, ama mambo ya tamaa mbaya za mwili, ama ulevi, ama uchawi, ama marafiki wale wabaya kutoka ushirika wa dhambi, kweli kunaleta maumivu sana. Ni kama kukata mkono (mst **8**) au kuling'oa jicho (mst **9**).
d) Lakini kuchagua uzima wa milele na kuacha mambo yale ya zamani ndiko kutubu. Mabadilisho haya katika moyo wa mwenye dhambi ndiyo kazi ya Neno la Mungu na ya Roho Mtakatifu.

*4) Hiyo ndiyo njia ya kufikia ukubwa wa kweli.*

a) Ni kusudi lake Yesu anapofundisha mambo hayo (mst **1**).
b) Katika njia hii tunazuiwa na mambo mengi, kama yale ya juu (sehemu 3c), mengine ni mazuio kutoka watu wabaya na maadui wetu wa kiroho.
c) Hawa wanaoongoza vibaya watoto (wadogo) au watu wengine, wanajitwika wajibu mkubwa mno, watapokea adhabu inayofaa matendo yao (mst **6**). Kosa lililo kuu ni kupoteza wadogo, kwa maana hawa wanaungama udhaifu wao, tena wanakubali kupokea msaada.
d) Tukilindwa katika hatari zote na kushinda majaribu yote, ni neema tu, kwa maana tunaweza kuingia mbinguni kama watoto tu (mst **3**). Ikiwa tunaokolewa kwa njia hii, tutaufikia ukubwa ule uliowekwa akiba kwao waliompokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wao.

# SIKU YA BWANA YA KUKUMBUKA MATENGENEZO YA KANISA
**(= Reformation Day; Jumapili ya mwisho katika Oktoba)**

**(Yn 8:31–36)**

*Maelezo juu ya sikukuu hiyo.*
Kwa ajili ya hali na maana ya sikukuu hii kuna ruhusa kwenda nje ya somo kidogo kueleza

a) Kanisa la kweli ni nini,

b) Kufuata Neno la Mungu katika mambo ya Kanisa ni nini,

c) Tofauti kati ya makanisa mengine mengine kwa habari ya njia ya wokovu ni nini,

d) Sisi kama Wakristo wa Kilutheri tunafundisha nini, tuna wajibu gani?

Kweli inawezekana kuyaeleza mambo haya yote kwa nuru ile inayopatikana katika somo la leo.

## NJIA YA WOKOVU

*1) Si njia yo yote ambayo ungependa mwenyewe kuifuata.*

a) Kwa sababu watu wote ni wenye dhambi (**Rum 3:23**) na *"kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi"* (mst **34**).
b) Kwa sababu watu wengi wanaojisifu ya kuwa ni wenye uhuru hawaoni ya kuwa wao ni watumwa (mst **33–35**).
c) Kwa sababu watu hawawezi kuwaza wenyewe mambo ya mbinguni, kwani wao ni wa chini. **1 Kor 2:14; Yn 8:23–24.**

*2) Ni njia iliyowekwa katika Neno la Mungu.*

a) Makanisa (mausharika, masinodi, wachungaji n k) hayawezi kuweka au kufanya njia ya wokovu, wala hawawezi kuifukuza hii na kuikubali hii.
b) Njia ya wokovu imewekwa kwa nyakati zote. Ni moja tu. **Yn 14:6; Mdo 4:12; 13:26; Rum 1:16–17; 1 Kor 3:11.**
c) Kwa hiyo ni lazima kulitumia Neno la Mungu linalotupatia njia hii ya wokovu na kuieleza kwetu. **Rum 10:17.**
d) Si kulitumia mara moja tu, ila kulitumia siku zote na kukaa daima katika nguvu yake na nuru yake (mst **31**). **Yn 15:5; 2 Tim 3:14; 3 Yoh 1:4; Efe 6:10–17.**

*3) Ni njia ya neema kabisa.*

a) Ingawa kuna masharti, sisi tufanye nini ili kuokoka (kama2 a–d hapa juu) na mashauri mengine ya kuwa tuendelee kwa utii na uaminifu na maombi, matendo yetu siyo yanayotuokoa. Wokovu ni kwa neema tu. **Rum 3:24; 4:4; Efe 2:5,8.**
b) Matendo yanayohesabiwa ndiyo yale ya Yesu Kristo tu. Pasipo upatanisho wake hakuna wokovu wo wote. **Rum 5:11; Efe 2:16.**
c) Kwa hiyo Yesu Kristo tu anaweza kutupa sisi uhuru wa kweli (mst **32**), ndio uhuru wa wana (mst **35–36**). **Gal 4:5; Ebr 2:14–18.**

*Application.*

a) Shauri lililo kuu kwa watu wa makanisa, ndilo shauri la uhuru. Tukiwa na utumwa, basi hatuna uhuru. b) *Kusema* 'uhuru' hakutoshi, ni lazima *kuwa na uhuru*, yaani kuwa na uhuru kweli kweli. c) Ni ajabu sana, lakini *walio huru kweli*, watu na makanisa, *ndio waliofungwa* katika Neno la Mungu na katika Yesu Kristo (mst **31**). **Flp 2:16.** d) Katika nuru ya maneno haya unaweza kujipima mwenyewe na kulipima kanisa lako kama mnakaa katika nuru na uhuru – ama bado.

# SIKUKUU YA WATAKATIFU WOTE
**("All Saints' Day"; Jumapili ya kwanza, mwezi wa Novemba)**

**(Mt 5:1–12)**

*Maelezo juu ya sikukuu hiyo.*

Katika sikukuu hiyo tunakumbuka wote walioamini kweli na kupiga vita vya Kikristo na waliomaliza mwendo wao. Hatuwezi kuwajua hawa wote, wala hatuwezi kujua kwa njia kamili habari za mtu fulani kama yeye amefariki kama Mkristo wa kweli. – Lakini maana ya sikukuu hii ni kuangalia mfano mzuri wa watakatifu na kujifunza sisi mambo ya imani na kushikwa na tamani lile la kuwafuata mpaka kifiko kile cha milele.

## UHERI WA KIMBINGUNI

*1) Uheri huu ni wa namna gani?*

a) Yesu anatufundisha mambo makuu katika somo hili.
b) Ingeonekana ya kuwa anatoa habari mbalimbali, lakini si hivyo, kwa maana wote wanaitwa 'heri', wote wanashirikiana katika neno hilo kuu, 'uheri'.
c) 'Uheri', maana yake ni ya kuwa tutakuwa kama Mungu alivyotaka kutufanya. **1 Yoh 3:2.**
d) Kazi hii itamalizika na kutimilika mbinguni, lakini inaanza hapa. Hata hapa Yesu anaita wanafunzi wake 'heri'.

*2) Njia ya kufikia uheri.*

a) Kwa wanafunzi wote ni njia inayopitia dhiki na uchungu.
b) Pengine ni mateso kutoka watu (mst **10–11**).
c) Pengine ni huzuni (mst **3–4,6**) kwa ajili ya dhambi na udhaifu. **Mt 26:75; Yak 4:9; 2 Kor 7:10.**
d) Sisi sote hatuna budi kuipitia njia hii ya huzuni. **Mdo 14:22.** Huzuni nyingine ni kwa ajili ya watu wabaya na mateso, nyingine ni kwa sababu tunaona ya kuwa tunakosa mambo mengi kama upole, na haki, na rehema, na moyo safi (mst **5–8**).
e) Labda huzuni iliyo kuu itatokea tunapoona ukali wa Sheria ya Mungu na udhaifu wetu wa kuitimiza. Ndio umaskini wetu wa kuitimiza. Ndio umaskini wa roho (mst **3**). – Lakini kwa ajili ya umaskini huo itakuwa lazima kuipokea neema ya Mungu. Njia ya kufikia uheri ni upendo wa Mungu, yaani neema na huruma tu. **Tit 2:11; Ebr 12:15; 1 Pet 5:10.**

*Application.*

a) Yesu anaposema 'heri' mara tisa, maana yake si ya kuwa walio heri wako wa namna tisa, bali
b) unaweza kujipima katika mambo haya yote na kuuliza: Je, mimi ni maskini kwa njia hii, mimi ni mwenye upole, na rehema, na moyo safi kwa njia hii? Kama bado, basi
c) umwombe Mungu ya kuwa kwa rehema yake akupatie umaskini na huzuni za kweli kwa jinsi ya Mungu **(2 Kor 7:10)** ifanyayo toba.
d) Umaskini na huzuni namna hii zinaleta nafasi kwake Kristo kukupatia neema yake na wokovu wake, hata aweze kukuambia nawe 'heri'.
e) Kama anakuambia 'heri' hapa ulimwenguni, na wewe kukaa katika neema hii siku zako zote, atakusalimia kwa neno lile 'heri' hata mbinguni katikati ya watakatifu wengine. Ndio *"mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana - Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao."* **Ufu 7:9.**

**BASI ATUKUZWE YEYE AWEZAYE KUFANYA MAMBO YA AJABU MNO KULIKO YOTE TUYAOMBAYO AU TUYAWAZAYO, KWA KADIRI YA NGUVU ITENDAYO KAZI NDANI YETU; NAAM, ATUKUZWE KATIKA KANISA NA KATIKA KRISTO YESU HATA VIZAZI VYOTE VYA MILELE NA MILELE. AMINA.**

**EFE 3:20-21**